**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MKUTANO WA NANE**

---

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 9 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):**

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MHE. ANNIA S. CHAUREMBO (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):**

Maoni ya Kambi ya Upinzania kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mipango Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 375

**Bodi ya Michezo ya Kuigiza Nchini**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Bodi ya Michezo ya Kuigiza inakabiliwa na matatizo mengi. Mojawapo ikiwa ni ukosefu wa ofisi za kufanyia kazi na kutumia fedha nyingi kupanga hali ambayo haikidhi haja yao.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kuipatia jengo au kiwanja Bodi kwa ajili ya ujenzi?

(b) Je, mafanikio ya Bodi hiyo yanakuja pasipo ruzuku hiyo ya Serikali. Je, si vizuri wakapewa ruzuku hiyo wajenge ofisi zao?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir kwamba Bodi anayoizungumzia haishughulikii michezo ya kuigiza peke yake, bali pia hushughulikia udhibiti wa maadili katika filamu. Hivyo jina sahihi la Bodi hiyo ni Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza.

Baada ya ufafanuzi huo mfupi, napenda sasa kujibu maswali ya Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Awamu ya Nne ina mikakati ya makusudi ya kuhakikisha Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini inakuwa na ofisi za kudumu. Katika mkakati wake wa muda mfupi Wizara yangu imepanga kuipatia bodi hiyo nafasi ya ofisi katika Jumba la Utamaduni la Taifa ambalo mchachakato wake wa ujenzi tayari umeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mradi huu Serikali katika mikakati yake muda mrefu pia inaendelea kutafuta fedha kadiri hali ya uchumi itakapokuwa nzuri ya kuiwezesha bodi kutafuta kiwanja na hatimaye kujenga ofisi yake ya kudumu.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, alikusudia kuzungumzia uchache wa ruzuku inayotolewa kwa Bodi. Napenda kusema kwamba hali hii inasababishwa na ufinyu wa Bajeti ya Wizara yangu kwa ujumla wake.

Hivyo kadiri Bajeti ya Wizara itakavyokuwa ikiongezeka, ndivyo Wizara itakavyotenga fedha za ruzuku zaidi kwa Bodi ya Ukaguzi wa Filamu na Michezo ya Kuigiza.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo ya nyongeza. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa Bodi hii inashughulikia hasa maadali na utamaduni Tanzania. Je, kuna kesi ambazo zimefikishwa Mahakamani kwa watu ambao wanavunja maadili ya utamaduni wetu?

Je, kuna hatua za makusudi ambazo zimechukuliwa dhidi ya watu ambao wanavunja taratibu na utamaduni wetu wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni kesi ngapi zimefikishwa mahakamani, zimefikishwa kesi nyingi sana katika mahakama zetu na baadhi ya waliotiwa hatiani wamepigwa faini. 200,000, 300,000 hadi 500,000 kulingana na makosa yalivyokuwa. Lakini idadi ya kesi katika nchi yetu zipo Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, kwa kweli idadi yake sasa hivi siwezi kuwa nayo lakini tunaweza kuwa na kumbukumbu hizo ofisini.

Lakini wale wanaovunja maadili wanashughulikia kwa mujibu wa Sheria namba saba (7) ya mwaka 1997.

Na. 376

**Tatizo la Ukosefu wa Maji Safi na Salama**

**MHE. AME PANDU AME** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ina vyanzo vingi sana vya maji; na kwa kuwa Watanzania wengi wana tatizo kubwa la ukosefu wa maji safi na salama.

Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuhakikisha Watanzania wote wanaondokewa na tatizo hilo kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mbunge wa Jimbo la Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba nchi yetu kwa ujumla imebahatika kuwa na vyanzo vingi vya maji juu na chini ya ardhi. Hata hivyo vyanzo hivyo havikuenea kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote nchini. Kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa

sasa ni sawa na mita za ujazo 2,700 kwa kila mtu kwa mwaka. Pamoja na hali hiyo yapo matatizo yanayochangia upungufu wa maji katika baadhi ya maeneo. Kutokana na kadirio la ongezeko la idadi ya watu pekee kiwango cha upatikanaji wa maji kinatarajiwa kushuka hadi kufikia mita za ujazo 1,500 kwa kila mtu ifikapo mwaka 2025 na kuweka nchi katika hali ya uhaba wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Watanzania wote wanaondokana na tatizo la maji kwa haraka Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha vyanzo vya maji vilivyopo vinatumika ipasavyo. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha mashauriano na makubaliano yamefikiwa ili kuanza kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006 - 2025). Katika kutekeleza Programu hiyo, Tanzania imezingatia kufikia malengo ya MKUKUTA ifikapo mwaka 2010, Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015 na Dira ya Maendeleo ya Taifa ifikapo mwaka 2025 pamoja na Mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya MKUKUTA katika uendeshaji wa rasilimali za maji ni kupunguza kiwango cha uchafuzi wa mazingira kutoka asilimia 20 mwaka 2003 hadi asilimia 10 mwaka 2010 na kuwa na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji katika mabonde yote tisa ifikapo mwaka 2010. Aidha programu inalenga kuongeza idadi ya wananchi waishio vijijini kupata maji safi na salama kutoka asilimia 53 mwaka 2003 kufikia asilimia 65 mwaka 2010 asilimia 79 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2025. Hii inahitaji pia kuongeza kiwango cha upatikanaji maji safi na salama kwa wananchi waishio mijini kutoka asilimia 73 mwaka 2003 kufikia asilimia 90 mwaka 2010 asilimia 95 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Programu hii pamoja na Mkakati wa Taifa wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji, utalinufaisha Taifa kwa kuhakikisha kuwa rasilimali ya maji inatumika kwa uendelevu na vyanzo vyake vinalindwa ili kukidhi mahitaji ya maji ya sasa na ya vizazi vijavyo.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Ningependa kujua kwamba mpaka sasa jumla ya asilimia ya Tanzania nzima

Je, Serikali imeshasambaza asilimia ngapi kwa Watanzania na imebakia asilimia ngapi kupatiwa maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimeelezea kuhusu mkakati wa Serikali, jinsi ambavyo huduma ya maji itakavyoongezeka. Kwa hivi sasa kwa vijijini ni asilimia 53 na tunatarajia ifikapo mwaka 2010 tuongeze mpaka kufikia asilimia 65. Kwa mijini hivi sasa ni asilimia 73 na tunatarajia kwamba ifikapo mwaka 2010 ifikie asilimia 90. Tutaendelea kila wakati kwa kuongeza juhudu na hii huduma iongezeke hadi 2025 ambapo mijini itakuwa ni asilimia mia moja na vijijini itakuwa asilimia 90.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Ningependa kufanya marekebisho kidogo katika jibu zuri ambalo amejibu Mheshimiwa Naibu Waziwa wa Maji kwamba tulipofikia sasa hivi kwa takwimu za Wizara ni kwamba kwa wananchi wanaoishi vijijini tumefikia asilimia 55.7 na kwa wananchi wa mijini ni asilimia 78. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Maji ni uhai; kwa kufuatana na uchambuzi unaofanywa na wanamazingira duniani wanasema kwamba ongezeko la joto hivi sasa ni 0.75, lakini ifikapo mwaka 2050 litakuwa limeongezeka kwa asilimia 3 na hivyo kusababisha matatizo ya mito duniani kukauka; na kwamba asilimia 40 ya watu watakwenda baharini kuokoa maisha yao.

Swali, ili kuboresha hatua hizi nzuri ambazo zinafanywa na Wizara na kwa sababu watu wengi hawajui dunia wanayoishi hasa tatizo hili. Je, isingekuwa vizuri Wizara yenyewe kupita katika kila kijiji kila Wilaya na kuweka mipaka hiyo ya maeneo yanayoitwa vyanzo vya maji na kuwa na ukaguzi wa kila mwaka kujua kama hatua hizi zinatekelezwa au vipi ili tuweze kujiokoa na janga hili ambalo limekuwa tishio kubwa kwa uhai wetu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba jinsi hali inavyokwenda na tusipozingatia kuhifadhi mazingira yetu ni kwamba maji yatazidi kupotea. Kwa hali hiyo basi Wizara ya Maji inasheria ambayo imeweka kwamba kuna mipaka ya kuhusu shhughuli za binadamu ziishie umbali gani kutokea kingo za vyanzo vya maji na katika shughuli hizo kuna viwango ambavyo vimewekwa, kuna kiwango cha sehemu za kutokea kwenye bahari na maziwa ni kwamba lazima shughuli za binadamu zianzie umbali wa mita 500 kutoka usawa wa chanzo cha maji.

Hali kadhalika pia kuna kiwango ambacho kimewekwa kwa ajili ya mito na vyanzo vingine kwamba shughuli za binadamu zifivuke kiasi cha mita 200. Pia Wizara ya Mazingira na wenyewe wameweka kwamba isizidi mita 60 kutokea kwenye chanzo cha maji na pia Wizara ya Ardhi na yenyewe imekubaliana kwamba shughuli za binadamu zisizidi mita 60 kutokea kwenye chanzo cha maji.

Kwa hivi sasa Wizara yangu ya maji inarekebisha sheria ya maji ili kuhakikisha kwamba ifuatwe na hali kadhalika adhabu zitatolewa kwa kufuatana na ambaye atapingana na sheria hiyo na adhabu zipo za aina mbalimbali ambazo zitarekebishwa. Sheria tunategemea mwanzoni mwa mwaka ujao itakuwa tayari kuletwa Bungeni.

Na. 377

**Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. ESTHERINA J. KILASI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kwa kuzingatia vigezo mbalimbali iliamua kuwakopesha wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu fedha za kujikimu na asilimia sitini ya *tuition fees* na kuacha asilimia arobaini ilipwe na wanafunzi wenyewe.

(a) Je, ni wanafunzi wangapi wamelipa kiasi cha asilimia 40 kwa wale waliojiunga mwaka 2005/2006?

(b) Je, kuna matatizo yote katika ufuatiliaji wa fedha hizo na kama yapo ni mikakati gani imewekwa kuhakikisha wanafunzi wote wanalipa kiasi kinachodaiwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kilasi Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Kilasi kuwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 Wizara yangu ilitoa mikopo kwa asilimia mia moja na siyo asilimia sitini kama alivyosema.

Hata hivyo katika mwaka wa fedha 2006/2007 wanafunzi walikopeshwa asilimia sitini na kutakiwa kulipa asilimia 40. Katika maeneo yafuatayo:-

(i) Ada ya masomo;

(ii) Mafunzo kwa vitendo; na

(iii) Mahitaji Maalumu ya vitivo.

Aidha katika maeneo ya chakula na malazi utafiti, vitabu na viandikwa wanafunzi walikopeshwa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2007, wastani wa wanafunzi waliolipa asilimia arobaini katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara, Moshi na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na usanifu wa majengo ilikuwa ni asilimia 40.7

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wenye wajibu wa kufuatilia ulipwaji wa asilimia 40 ni Vyuo na Taasisi zenyewe. Hata hivyo Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu zimekumbana na matatizo yafuatayo:-

(i) Wanafunzi wengi kudai kwamba hawana uwezo wa kulipa kiasi hicho cha asilimia 40 na kwamba Serikali iwakopeshe kwa asilimia mia moja.

(ii)Wanafunzi wengi wanaamini kwamba Serikali itabadili sera ya uchangiaji katika elimu ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo au Taasisi za Elimu ya Juu zimeweka mikakati ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanalipa kiasi wanachodaiwa. Mikakati iliyowekwa ni pamoja na:-

Vyuo na Taasisi za Elimu ya Juu kuwaruhusu wanafunzi walioshindwa kulipa asilimia arobaini 40 kuendelea na masomo katika vyuo vyao wakitambua kuwa wao ni wadeni.

Vyuo na Taasisi kuweka mikakati endelevu ya kukusanya kiasi cha fedha ambacho wanafunzi wanatakiwa kuchangia.

Kuelimisha Umma pamoja na wanafunzi kuwa dhana ya uchangiaji gharama za elimu ya juu na dhana ya mikopo hazikinzani bali zinakwenda pamoja.

Kuanzia mwaka wa masomo wa 2007/2008 wanafunzi wa elimu ya juu watapewa mikopo kulingana na uwezo wao kiuchumi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza. Kwa kuwa unapokopa ni lazima urejeshe mkopo ule na kwa kuwa huu ni mkopo wala si zawadi na kuna watu walikopa na hivi sasa tayari wameshamaliza mafunzo katika vyuo. Je, sasa Serikali inasemaje kuhusu kuweka mkakati wa kukusanya madeni hayo ili wanafunzi waweze kunufaika zaidi na mikopo hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa nakubaliana naye kwamba anayekopa ni lazima arejeshe na Wizara yangu kupitia Bodi ya Mikopo tumeshaweka mikakati, tumeshaajiri watu wanaohusika na ukusanyaji wa mikopo na tumeshatangaza kwenye vyombo vya habari umuhimu wa kurejesha hii mikopo ili irudi iweze kukopesha wanafunzi wengine. Hawa ni kuanzia mwaka 1994 mpaka waliokopeshwa mwaka jana na watakaoendelea kukopeshwa, na kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, leo hii tutakuwa na Sherehe kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa wanarejesha mikopo ambayo walikopeshwa wakati wanasoma katika vyuo vikuu na elimu ya juu.

Kwa hiyo leo ni mwanzo wa kurejesha hiyo mikopo na kwa wale ambao watakuwa hawarejesha na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge kuonyesha mfano katika hili na Watanzania wote waige hili warejeshe mikopo hii kwa ajili ya kusomesha wanafunzi elimu ya juu wakiwemo watoto wao na wengine. Kwa hiyo, hilo linatekelezwa na leo ni mfano halisi.

**MHE. DR. WILBROB P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema moja ya mikakati iliyoandaliwa ni pamoja kuwaruhusu wanafunzi ambao hawana uwezo walipie lakini waendelee na masomo lakini watambuliwe kuwa wadeni; na kwa kuwa hivi sasa tunapoongea kuna vijana zaidi ya 400 wa vyuo vikuu vya *St. Augustine* Mwanza na Tumaini ambao ni wanafunzi wa Serikali wa fani ya ualimu na hawa wanafunzi wamenyimwa kufanya mtihani.

Je, Serikali inatoa kauli gani ili hawa wanafunzi waweze kufanya mitahani yao na waendelee kutambuliwa kama wadeni kama walivyo wengine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema taratibu ya kuhakikisha kwamba asilimia 40 iliyobaki ya wanafunzi kwa kweli ni taratibu inayofanywa na vyuo vyenyewe.

Sisi Serikali au Wizara hatuwezi kuwaamulia kwamba wafanye nini na ndiyo maana kwa vyuo vyetu vya umma na hasa kwa vyuo vya binafsi hatuwezi kuingilia suala hilo. Wengi wamefanya hivyo, wamewarudisha kama tu kuwachukulia kwamba hawajalipa. Tumewaomba vyuo wajaribu kuelewana na wanafunzi na wazazi wao hili deni lilipwe kwa sababu wanahitaji hizo fedha kwa kuendeshea vyuo.

Kwa hiyo, tuna hakika kwamba hili litafanyika chini ya uongozi wa vyuo kuhakikisha kwamba wanasoma lakini pia deni linalipwa kwa taratibu walizoweka wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Maswali mengine yote mtayauliza kwenye muswada unaokuja.

Na. 378

**Mazingira ya Kazi kwa Mahakimu na Wanasheria wa Serikali**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa muda mrefu sasa Mawakili wa Serikali pamoja na Mahakimu wa Mahakama zote hawana nyumba za kuishi wala usafiri wa kwenda na kurudi kazini; na kwa kuwa, kazi wanazofanya zinahitajika waishi mahali penye usalama na ulinzi.

Je, ni lini Serikali itamaliza kilio cha Mawakili na Mahakimu hao kwa kuwapatia nyumba na usafiri?

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio cha Mawakili wa Serikali kuhusu nyumba na usafiri kimewasilishwa kwenye Kamati ya Rais ya kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi wa umma mwezi Novemba, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ilishawasilisha ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais namshauri Mheshimiwa Mbunge avute subira tukisubiri maamuzi yatakayotolewa kuhusu ripoti hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu nyumba na usafiri kwa Mahakimu, licha ya kilio hicho kufikishwa kwenye Kamati niliyoitaja hapo juu pia Mahakama ya Tanzania imechukua hatua za makusudi kabisa za kuhakikisha kuwa Mahakimu wanapatiwa usafiri wa uhakika. Hivi sasa kadri uwezo unavyoruhusu magari yamekuwa yakisambazwa katika Mahakama zetu za Wilaya.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu anasema sasa hivi anasambaza magari mpaka kwenye Mahakama za Wilaya. Je, hawaoni kwamba tatizo kubwa zaidi liko kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao wengi hawana nyumba na usafiri na hutembea mwendo mrefu kwenda kwenye Mahakama wanazozihudumia.

**NAIBU WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubalina na Mheshimiwa Msindai kwamba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni wengi na wana matatizo ya usafiri kama ilivyo kwa wafanyakazi wa *level* hizo. Sasa kutatua tatizo lao Serikali imekuwa ikitoa mikopo ya pikipiki kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo lakini pia tunawashauri wao kama watumishi wengine wa Serikali wajitahidi basi kuchukua mikopo hii ya pikipiki au baiskeli ili ziweze kuwasaidia matatizo haya.

Tumeanza kutoa magari kwa Wilaya na kadiri uwezo utakavyoruhusu basi tutafika mpaka huko chini, lakini kwa sasa tupo Wilayani na bado hatujakamilisha Wilaya zote.

Na. 379

**Hali ya Ziwa Nyasa**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwa kawaida Ziwa Nyasa halina rutuba *(Origotrophic)* na kwa sababu hiyo uzalishaji wa Samaki katika Ziwa hilo ni mdogo ikilinganishwa na Ziwa dada Tanganyika; na kwa kuwa Samaki wa Ziwa wamevuliwa sana *(overfished)* na zaidi kwa kutumia uvuvi haramu.

Je, Serikali ina mipango gani kabambe ya kurekebisha hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, ninapenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa kushirikiana na nchi za Msumbiji na Malawi, iliendesha utafiti uliofahamika kwa jina la *Lake Nyasa Pelagic Fish Resource Assessment* katika miaka ya 1990 – 1994. Madhumuni ya utafiti huo yalikuwa ni kufahamu aina ya samaki, makaazi yao na kiwango cha samaki wanaoweza kuvuliwa ili kuhimili uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti ulibaini kwamba kuna samaki wengi katika kina kirefu mbali na ufukwe ikilinganishwa na idadi ndogo ya samaki karibu na ufukwe wa Ziwa. Aidha, utafiti ulibaini kuwepo kwa wastani wa tani 168,400 za samaki katika Ziwa lote. Kutokana na idadi hiyo, tani 81,000 za Samaki zinaweza kuvuliwa katika Ziwa lote bila kuleta athari yoyote. Hata hivyo, kiwango cha Samaki kinachovuliwa hakizidi tani 30,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha 2006/2007, Wizara yangu iliendesha mafunzo kwa vitendo kwa kutumia boti ya mita 4 yenye injini ya kupachika *(outboard engine)* ya *Horse Power 15*, ndoana na mishipi kwa wavuvi 20 kutoka Kata 10 za Wilaya ya Mbinga na wavuvi 12 kutoka Kata 6 za Wilaya ya Ludewa. Mafunzo hayo yaliwawezesha wavuvi kuvua katika maeneo ya mbali yenye kina kirefu cha maji yasiyovuliwa kikamilifu. Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inategemea kwamba baada ya mafunzo hayo, Halmashauri za Wilaya zitawahamasisha wavuvi kuunda vikundi vitakavyowezesha kukopa kutoka vyombo vya fedha na kununua boti, injini, mishipi na ndoana ili kuendesha uvuvi endelevu wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Samaki wanaopatikana katika Ziwa Nyasa huenda kutaga kwenye mito. Husababisha wavuvi ambao wanafahamu tabia ya Samaki wa aina hii kuwavua kwa wingi wakati wakielekea kwenye maeneo ya kutaga na kuathiri wingi wao. Mwaka 2006/2007 wavuvi 458 kutoka vijiji 7 vya Wilaya ya Ludewa na wavuvi 370 kutoka vijiji 6 vya Wilaya ya Mbinga, wamepewa mafunzo kuhusu sheria na kanuni za uvuvi pamoja na usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kuunda vikundi vya kusimamia rasilimali ya uvuvi. Vikundi hivi hatimaye vitashirikishwa katika ulinzi wa rasilimali za uvuvi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru Wizara na hususan Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein Mhita kwa kwenda kutoa mafunzo kwa wavuvi wetu wanaolitumia na kutegemea sana Ziwa Nyasa. Namshukuru kwa kuweza yeye mwenyewe binafsi kwenda na boti lile na kufika mpaka kati kati ya Ziwa ambalo ni Ziwa lililo *rough* sana hapa Ulimwenguni na akajua matatizo wanayoyapata wavuvi na wananchi wanaoishi mwambao mwa Ziwa Nyasa. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza: Moja, baada ya kushukuru kwamba wametoa mafunzo ambayo yalichukua siku moja (na huhitaji siku nyingi naelewa) na kwenda ndani ya Ziwa

kwa ajili ya kutoa mafunzo yale na ni watu wawili wawili kila Kata. Sasa wakirudi majumbani kwao, kwanza, hawana uwezo wa kutoa mafunzo kama yale waliyopewa wao kwa kwenda ndani ya Ziwa kwa sababu hawana vyombo kama vile ambavyo Naibu Waziri alivitumia. Sasa, hapa ombi langu. Je, kwa nini Wizara ya Mali Asili na Utalii haitoi angalau boti moja ikakaa pale Halmashauri itumike katika Mwambao wa Ludewa ili iwasaidie wale waliopata mafunzo wawili kila Kata waweze kuwafundisha wenzao kwa kwenda ndani ya Ziwa mbali zaidi na kutoa elimu kwa vitendo, hili haliwezekani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa vile tumekubaliana kwamba Ziwa Nyasa halina samaki sana na kwamba lazima uende ndani, lakini kando kando huwezi kupata samaki. Je, tutawasaidiaje, ni mikakati gani ya ziada ambayo Wizara inaweka kuchukua ili kuhakikisha vikundi hivyo basi hata vikiundwa, vinaweza kupata samaki kwa kwenda zaidi ndani ya Ziwa? Ahsante sana!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu yawe mafupi, ingawa aliyeuliza swali, ameuliza marefu sana!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimshukuru kwa jinsi alivyonishukuru kwa kufika Ziwa Nyasa. Ni kweli nimefika na nimeona lile Ziwa jinsi lilivyo. Kuhusu mafunzo, yale mafunzo yalikuwa zaidi ya siku moja, mafunzo yalichukua siku 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na boti, boti ambayo tulitumia kwa mafunzo ya vitendo kwa wavuvi, tuliliacha katika Halmashauri ya Mbinga ili liendelee kutoa mafunzo kwa wavuvi wengine. Nakubaliana na Mheshimiwa Prof. Mwalyosi kwamba mafunzo yaliyotolewa kwa kweli yalikuwa ya muda mfupi na wavuvi wanahitaji muda zaidi. Lakini, hata hivyo, ninachomweleza ni kwamba hali ya kifedha ya Wizara ikiwa nzuri, tutawapatia Halamashauri ya Ludewa wao pia boti yenye injini ambayo itatumiwa kwa mafunzo kwa wavuvi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; ni kweli kwamba wavuvi wa Ziwa Nyasa wanatumia zana ambazo kwa kweli ni dhaifu sana na ni mitumbwi inayotengenezwa tu na wanatumia kwenda kuvua karibu na ufukwe. Mitumbwi ile haina uwezo wa kwenda mbali zaidi. Lakini, tuliwashauri wavuvi waunde vikundi ambavyo baadaye wataweza kukopa fedha kutoka vyombo vya fedha ili waweze kununua zana bora zitakazowawezesha kwenda kuvua mbali kutoka kwenye ufukwe ambako kuna kina kirefu cha maji na ambako ndiko kwenye samaki wengi na wakubwa. Lakini, hata hivyo, naomba niupongeze sana uongozi wa Wilaya ya Ludewa ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge Prof. Mwalyosi kwa sababu baada ya mafunzo yale tayari katika Wilaya ya Ludewa vijiji vinne vimekwishakukutana na wamefanya mikutano kuhusiana na ujasiriamali na wameelekezwa jinsi ya kupata mikopo. Kwa hivyo, naamini vikundi vile mpaka sasa vitakuwa vimeishakuwa imara na anaamini watakuwa wameishaanza mchakato wa kutafuta fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umetumia dakika 10 kwa swali moja!

Na. 380

**Utaratibu wa BOT Kujenga Barabara na Madaraja**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. MHE. SIRAJU J. KABOYONGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi nyingi Duniani hutumia utaratibu wa jenga endesha na kabidhi *(Build Operate and Transfer (BOT)* katika ujenzi hususan wa barabara na madaraja; na kwa kuwa kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali na umuhimu wa barabara ya kati kuanzia Manyoni – Itigi – Tabora – Urambo – Kigoma, ni vizuri Serikali ikatumia utaratibu huo wa *BOT* ili kuharakisha ujenzi wa barabara hiyo:

(a) Je, kwa nini Serikali yetu haitumii utaratibu huo katika ujenzi wa baadhi ya madaraja na barabara nchini?

(b) Je, Serikali iko tayari kupokea ushauri kwamba itumie utaratibu huo katika barabara ya kati?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hapa nchini, Serikali inatambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi na wafadhili katika ujenzi wa miundombinu ikiwemo bara bara na madaraja kwa kutumia utaratibu wa jenga, endesha na kabidhi *(Build, Operate and Transfed (BOT)*. Hata hivyo, utaratibu huu haujaanza kutumika hapa nchini kutokana na kutokamilika kwa maandalizi ya kanuni na mwongozo utakaowezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa barabara na madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa sheria mpya ya barabara iliyopitishwa na Bunge mwezi Aprili 2007, inaelekeza kuandaliwa kwa kanuni zitakazotoa mwongozo wa ushiriki wa sekta binafsi *(Public Private Partnership)* katika ujenzi wa barabara.

Hivi sasa kanuni na mwongozo husika zinaandaliwa na Mtaalam Mshauri *(Consultant)* chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia na tayari Mtaalam amekwishawasilisha ripoti ya awali *(Inception Report).*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ushauri wake mzuri ambao tayari umekwishaanza kufanyiwa kazi na ningependa kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote wasaidie kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi yetu wajitokeze kuwekeza katika miradi ya barabara na madaraja mara baada ya

kutungwa kwa kanuni zitakazowezesha kushiriki katika ujenzi wa barabara na madaraja hapa nchini.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi ya kuuliza swali la nongeza. Kwanza, nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Swali langu la nyongeza ni juu ya time *scale*. Kwa sababu haja inafahamika ipo, tumempa huyu *Consultant* muda gani ili atukamilishie kazi hii ili utaratibu huu tuanze kuutumia kwa sababu tunauhitaji?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba utaratibu huu tunaihitaji hapa nchini, lakini kwa sababu ni uatatibu mpya, lazima tuwe makini tusije tukafanya makosa yoyote katika utekelezaji.

Kama nilivyosema, *Consultant* amekwisha wasilisha *Inception Report*, inapitiwa na Wataalam wetu kwa makini ili baada ya hapo tumkabidhi aweze kukamilisha hiyo *report* yake.

Mimi naamini kabisa kwamba kwa sababu Serikali imedhamiria kuangalia kuhakikisha kwamba utaratibu huu unaanza kutumika, basi si muda mrefu baada ya taratibu zote hizi kukamilika na hiyo *report* kuwasilishwa na mamlaka husika vile vile kujulishwa na kutoa idhini, shughuli hii itaanza.

Na. 381

**Barabara ya Welei – Lutindi - Bungu**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya Welei/Lutindi hadi Bungu iko chini ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, lakini kutokana na na uwezo mdogo wa Halmashauri hiyo na pia umuhimu wa barabara hiyo kiuchumi na kibiashara, mara nyingi hufanyiwa matengenezo na *TANROADS*; na kwa kuwa hali ya barabara hiyo kwa sasa ni mbaya sana hadi kukosesha mawasiliano kati ya Welei na Lutindi:-

(a) Je, Serikali kupitia *TANROADS* haioni umuhimu wa kuifanyia matengenezo japo ya dharura barabara hiyo hasa kwa kipindi hiki ambacho haipitiki?

(b) Je, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu kwa ushirikiano na Wizara ya TAMISEMI haioni kuwa sasa ni wakati muafaka kuiweka barabara hiyo chini ya mamlaka ya Mkoa kwa kuzingatia kuwa inakidhi vigezo kama vile kuwa na kiungo muhimu kati ya Wilaya ya Korogwe na Lushoto?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Welei Litindi hadi Bungu ni sehemu ya barabara ya Msambiazi – Lutindi – Bungu (Kwabluu) yenye urefu wa kilomita 19 inayohudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Ni kweli kuwa barabara hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kiuchumi kutokana na kuwepo kwa shughuli za kilimo hasa kilimo cha Chai, Iliki, Kahawa, Hospitali maalum na wingi wa watu wanaoishi maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu spika, kwa kuzingatia hilo, Wizara yangu imekuwa ikitoa pesa za kuzifanyia ukarabati sehemu za barabara hii kama ifuatavyo:- Mwaka 2003/2004 shilingi 52,740,570; mwaka 2004/2005 shilingi 34,856,800 na mwaka 2005/2006 shilingi 45,744,711. Kazi za ukarabati zilizofanyika ni pamoja na kuchonga, kupanua na kuweka changarawe baadhi ya sehemu korofi, kuweka makalvati mapya na kuchimba mifereji.

Kazi hizo zitatekelezwa kwa awamu zikihusisha sehemu tu ya barabara hii na kipindi hicho chote Halmashauri ya Korogwe iliachwa kuendelea na matengenezo ya kawaida. Kwa sasa kwa sbabu ya ufinyu wa bajeti Wizara yangu imeshindwa kuendelea kutoa mchango wa ukarabati wa barabara hii. Namshauri Mheshimiwa Mbunge aishawishi Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe iweke kipaumbele katika ukarabati wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupandishwa daraja au vinginevyo kwa barabara hii, hili litafanywa kulingana na vigezo vilivyomo katika Sheria Mpya ya Barabara, kama ilivyopitishwa na Bunge. *(Makofi)*

Na. 382

**Udhibiti wa Wakimbizi**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kibondo na Kasulu ziko mpakani na nchi ya Burundi; na kwa kuwa Wilaya hizo zimekuwa zikihifadhi Wakimbizi wanaotoka nchi hiyo ingawa Wakimbizi hao wanaendelea kurudi kwao kwa utaratibu wa *Repatriation*:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi dhidi ya udhibiti wa mipaka yetu ili kuhakikisha kwamba watu hao ambao wana tabia ya uharibifu hawarudi tena?

(b) Ikiwa mpango wa uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika utakubalika. Je, si kweli kwamba kundi hilo litarudi tena na pengine wakakataa kuondoka na kuendelea kushikilia ardhi ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mikataba ya Kimataifa, nchi jirani huwajibika kuwapokea wakimbizi kama nchini mwao kuna hali ya vita na mauaji ya wenyewe kwa wenyewe. Kutokana na hali ya aina hiyo Tanzaia tulipokea malaki ya wakimbizi wa kutoka Burundi na iliyokuwa Zaire ambao bado tunao jumla ya karibu 400,000.

Kutokana na hali ya amani kurejea katika nchi hizo baada ya muafaka wa Kitaifa na kuchaguliwa Serikali za Kidemokrasia, sasa tuko katika kipindi cha kuwahimiza wakimbizi wa kutoka nchi hizo kurejea kwao kwa hiari yao. Tumetoka kipindi cha kurejea kwao kwa hiari *(Voluntary Repatriation)* na kuingia katika kipindi cha kuwahimiza warejee kwao kwa hiari *(Promotion of Voluntary repatriation)* kama tulivyokuabnaliana katika Tume ya Utatu ya Burundi, Tanzania na *UNHCR (Burundi Tanzania UNHCR Tripartite Commission)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa kwa ridhaa yako, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhambwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakimbizi hao kuja tena Tanzania haliko mikononi mwetu bali ni wajibu wa Serikali zao na wananchi wenyewe kudumisha hali ya amani na utulivu katika nchi zao ili isiwepo tena aibu ya kuwa na wakimbizi kutoka kwao kuja kwetu. Kuhusu wahamiaji haramu, juhudi inafanywa kuimarisha Vtuo vya Uhamiaji vya Mipakani, kutoa elimu ya uraia hasa kwa wananchi waishio maeneo ya mipakani na kuwahimiza kutoa taarifa za wageni wanaowatilia mashaka. Njia nyingine ni kuandikisha wakaazi wote wa vijiji vya mipakani katika Regista Maalum.

Aidha, njia ya kudumu ya kuhakiki uraia ni mradi wa vitambulisho vya uraia ambao Serikali inaufanyia kazi kama alivyoarifu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi katika hotuba yake ya Bajeti.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika au Afrika Mashariki ni dhahiri kuwa iwapo Shirikisho litaundwa kutakuwapo na taratibu za kiuhamiaji ambazo zitatawaliwa na Sheria na kanuni. Uanzishwaji wa Jumuiya ni jambo linaloandaliwa kwa makini na kwa kuzingatia mambo yote muhimu yakiwemo ya uahamiaji, ajira na uraia.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Napenda kumuuliza Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

La kwanza, sina hakika kama Naibu Waziri anajua kwamba *PALIPEHUTU – NFL* sasa hivi wameingia msituni kule nchini Burundi na hawa watu wakiingia msituni, wakimbizi huwa ndio chanzo chao cha kukimbilia hii Mikoa, Kagera na Ngara. Sasa hivi anaweza akanipa maelezo, Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na hali hiyo? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba Mheshimiwa Waziri alizungumza kwenye vyombo vya habari, vilimnukuu akisema kwamba itakapofika mwezi Desemba mwaka huu, wakimbizi wote watakuwa wameishaondoka katika Mikoa yenye wakimbizi. Sasa kama hawataondoka katika kipindi ambacho Mheshimiwa Waziri alinukuliwa, Serikali imejipanga vipi kupambana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa hapa ndani ya Bunge na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Serikali ya Tanzania inafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba *PALIPEHUTU – NFL* inarudi kushiriki katika Serikali ya Burundi. Serikali yteu haitaruhusu tena wakimbizi kuingia hapa nchini kupitia mipaka yetu na kama tulivyoarifu, tutajitahidi kabla ya mwaka 2008 kuhakikisha kwamba wakimbizi wote wanaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nireje tena kwa sababu katika swali la pili, Mheshimia Mbunge ameuliza kwamba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani amesema kwamba wakimbizi wote wataondoka ifikapo mwisho wa mwaka huu. Naomba kumsahihisha, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba lengo la Serikali ni kuhamkikisha kwamba wakimbizi wote wataondoka hapa nchini ifikapo mwishowa mwaka 2008. *(Makofi)*

**MHE. PHARES K. KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watu wengi wanajiuliza na wana wasi wasi juu ya Shirikisho la Afrika Mashariki; na kwa kuwa hawajui Shirikiho hilo likija ni mambo gani yatakuwa ya Taifa na mambo gani yatakuwa ya Shirikisho, jambo ambalo watu wana wasi wasi kwamba ardhi na mambo mengine yatatwaliwa.

Je, si vyema sasa Serikali ikatoa angalau rasimu ya Muundo wa hilo Shirikisho ili wananchi wakaondokana na wasi wasi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabuye, hilo swali ni lingine kabisa, hili lilikuwa la wakimbizi. Kwa hiyo naendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Na. 383

**Serikali Kumtambua Major General Mayunga**

**MHE. HAROUB SAID MASOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Jeshi letu la Ulinzi chini ya Uongozi wa Luteni Jenerali Mayunga lilifanya vizuri katika kukabiliana na Majeshi ya Nduli Idd Amin Dada katika Vita vya Kagera na kulipatia Taifa letu heshima kubwa:-

(a) Je, ni jambo gani kubwa ambalo Serikali ilimfanyia Mzee Mayunga kama tuzo kwa kazi kubwa?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ipo haja angalau wakati wa Mkutano wa Bajeti ya mwaka huu 2007/2008 wakati Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inapowasilisha Bajeti yake, Mzee Mayunga apewe mwaliko rasmi kupitia Wizara hiyo ili ahudhurie Bungeni jambo ambalo litampa heshima kubwa na faraja?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mbunge wa Jimbo la Koani, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana wakati wa vita vya Kagera yalichangiwa kwa pamoja na viongozi wetu wa kitaifa, makamanda na wapiganaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, watumishi wa vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama na wananchi kwa ujumla. Mafanikio hayo yalipatikana chini ya usimamizi wa Amiri Jeshi Mkuu, Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu ya Jeshi yalisimamia kwa umakini uendeshaji wa vita hivyo. Baada ya vita, washiriki wote wa vita vya Kagera walitunukiwa medali ya Ushujaa, akiwemo pia Luteni Jenerali (Mstaafu) Silas Mayunga, ikiwa kama tuzo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushinda vita hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya utangulizi, Luteni Jenerali (Mstaafu) Mayunga alitunukiwa medali ya ushujaa. Vile vile alipandishwa cheo kuwa Meja Jeneral tarehe 21 Machi, 1979 kabla ya kumaliza rasmi vita vya Kagera mnamo tarehe 11 Aprili, 1979 na tarehe 21 Juni, 1995 alipandishwa tena cheo na kuwa Luteni Jenerali.

Aidha, Serikali ilimpa heshima kwa kumpa kazi ya Ubalozi katika nchi mbalimbali za Afrika pia Serikali inaendelea kumtunza kwa kumpatia haki na maslahi kama wanavyopatiwa viongozi wa juu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania waliostaafu. *(Makofi)*(b)Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni la wananchi wote. Kila Mtanzania ana haki ya kuja katika vikao vya Bunge na kufuatilia mijadala mbalimbali inayoendelea ndani ya Bunge, na sio lazima kupata mwaliko maalumu.

Kwa maana hiyo, hakuna kipingamizi chochote kinachomzuia Luteni Jenerali Mayunga, kuja kufuatilia shughulii za Bunge. Hata hivyo nachukua fursa hii kuwaarifu mashujaa wote wa Vita vya Kagera, akiwemo Luteni Jenerali (Mstaafu) Mayunga kuwa ni ruhusa kuja kufuatilia mijadala ya Bunge na kusikiliza hotuba za bajeti za Wizara mbalimbali ikiwa ni pamoja na hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ulinzi na JKT na watakapokuwepo tutamuomba Mheshimiwa Spika awatambulishe kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mheshimia Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza hapa wakati huo wa vita vya Kagera, Luteni Jenerali Mayunga alikuwa Nafasi gani katika vita hivyo? Kwa kuwa vita vya Kagera ametamka hapa vilimalizwa tarehe 11 Aprili, 1979, kwa nini siku ya mashujaa inaadhimishwa tarehe 25 Julai kila mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJANGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Baba wa Taifa anatangaza Tanzania kuingia vitani tarehe 2/11/1978, Brigedia Generali Mayunga alikuwa ni *Brigade Commander* wa 206. Baadaye wakati vita vinaendelea na ushindi unaelekea kupatikana, *Brigadier General* Mayunga alipewa kazi na kuwa ni *Task Force Commander.*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Mashujaa wa Tanzania siyo wale tu waliopigana vita vya Kagera! Tuna Mashujaa waliopigana vita vya Maji Maji, Vita Vikuu vya Dunia vilivyomalizika tarehe 9 Agosti, 1945, Japan na Marekani kusaini tarehe 2/9/1945 kumalizika kwa vita vile.

Vile vile tuna waliopigana Msumbiji ambao tarehe 25 Mei, 1975 walimaliza na hao wa Kagera ambao wamemaliza vita, hawa wote ni Mashujaa. Serikali yetu ili kuwaenzi Mashujaa wote hawa tukaona siyo vyema tukatoa tarehe ya wale wa Kagera tu. Tumekubaliana tareh 25 Julai baada ya masafisho ya Uganda ndio isherehekewe kuwa ni Siku ya Mashujaa kwa Mashujaa wote wale wa Tanzania.

Na. 384

**Hitaji la Benki ya *NBC* Pemba**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inawapenda watu wake na hivyo katika kila Mkoa na baadhi ya Wilaya kuna mabenki yanayosaidia wananchi kuweka fedha zao na hivyo kuondokana na usumbufu wa kutembea na fedha mfukoni:-

(a) Je, kwa kuwa Pemba kuna Mikoa miwili tu, kwa nini hakuna huduma ya benki ya *NBC*?

(b) Je, ni lini huduma hiyo itafikishwa Pemba ili wananchi waondokane na usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA ( MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2000 Serikali iliuza asilimia 70 ya hisa zake katika Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*) na hivyo kubakiwa na asilimia 30 tu ya hisa katika benki hiyo ambayo sasa inaitwa *National Bank of Commerce Limited*. Kwa hiyo, benki hii siyo Shirika la Umma tena.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huduma za kibenki zinahitajika katika maeneo mengi hapa nchini, hata hivyo *NBC Limited* haiwezi kufungua matawi katika kila sehemu yanayohitajika kwa mara moja. *NBC Limited* itafungua matawi katika maeneo yote Tanzania, ikiwemo Pemba, kulingana na vigezo vyote muhimu vinavyotakiwa.

Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira mwafaka kwa mabenki kufanya shughuli zao kwa ufanisi pamoja na kuishawishi *NBC Limited* kuipa Pemba kipaumbele katika kuamua maeneo ya kufungua matawi mapya.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na sera ya utawala bora katika ubinafsishaji na kulingana na mikataba ya mauzo kati ya Serikali na wawekezaji, Serikali haina nia ya kuingilia mikakati ya kibiashara ya vyombo vilivyobinafsishwa yakiwemo mabenki.

Aidha, kwa kuwa mabenki yanaendesha shughuli zake kwa ushindani Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuwahamasisha wananchi kuanzisha benki zao katika maeneo yao ambazo zitaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kuwapatia huduma za kibenki kwa gharama nafuu zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MGENI J. KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mbali na Benki ya *NBC.*

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea huduma za benki nyingine ili wafaidike wakulima walioko huko Kaskazini Pemba?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, hata hizi benki nyingine *NMB, CRDB* zote hizo zitalinganisha kutazama namna kwa mujibu wa taratibu zao za kuweka benki katika sehemu yoyote ile

kama itakuwa ni ya faida wao na kwamba hii ni sehemu inakuwa na yale yote yanayohitajika.

Kwa hiyo, watapeleka vile vile benki wanapohisi kwamba kuna mahitaji yao na wananchi vile vile wa sehemu hiyo pia kama wakiomba yataangaliwa kwa benki yoyote ile anayehusika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda umekwisha. Sasa nina matangazo ya wageni. Kwanza kabisa nafurahi kutangaza kwamba kwenye *Speakers Gallery* leo tuna mgeni wetu ndugu Patrick Mwangunga, *Director of Finance* katika *TRA* ambaye ni mume wake Naibu Waziri wa Maji na Nishati, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga. Karibu Bwana Mwangunga. *(Makofi)*

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Waziri Seif Khatib Waziri wa Habari utamaduni na Michezo. Kwanza kabisa kuna wahariri Bwana Denis Msaki Mhariri wa Habari wa Mwananchi. Tuna mhariri mwingine Bwana Leonard Mwakalebela. Mhariri wa Habari wa *The Citizen.*

Halafu kuna wageni wake wengine yuko Bwana Vuai Naimu Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Jimbo, Bwana Shaaban Salim Katibu wa Tawi la CCM, Bwana Farush Ali Katibu wa Tawi la CCM, Mitakawani, Bibi Riziki Ramadhan Mwenyekiti wa Tawi la CCM, Pagali na Bibi Pili Khamis, Mjumbe wa Kamati ya Siasa ya Wadi Pambi na D. Mtumwa Ali Katibu Mwenezi wa Wadi ya Bambi. Kwa hiyo, *gender* imezingatiwa karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu Mheshimiwa Shellukindo naye ana mgeni wake bwana Charles Ndege Diwani wa Kata ya Mamba jimbo la Bumbuli. Karibu Mheshimiwa Diwani.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Zuleka Haji ni Bibi Salma Saadati *Programme Officer* wa *Training and Development.* Tuna mgeni mwingine anaitwa Bwana Ramadhan, mume wa Bibi Salma. Kwa maana hiyo, huyo mtaalam amekuja na mume wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu nina wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri Dodoma, simameni wote na walimu kama mpo. Karibuni sana. Wengine wako huku kwa sababu nafasi haikutosha. Tuna wanafunzi 35 kutoka Shule ya Sekondari ya Kisasa, Dodoma pia na walimu wao kama wapo tunaomba wasimame. Ahsante sana karibuni. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 24 kutoka shule ya Sekondari Dodoma na walimu wao kama wapo wasimame. Karibuni sana. Wote tunawatakia mafanikio mema katika masomo yenu. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna wageni hawa nafikiri watakuwa wageni wa Devota Likokola. Kuna Mheshimiwa Hilda Kayombo na Macklina Haule, wote watalaam wa vikoba. Tunafurahi kumwona Naibu Waziri Gaudence Kayombo amerudi Bungeni baada ya kupata matibabu, tunashukuru sana. Tunashukuru umeweza kuja ukiwa salama. *(Makofi)*

Matangazo ya kazi ni kama ifuatavyo: Mheshimiwa Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara anawatangazia wajumbe wa Kamati yake kuwa leo tarehe 9/82007 saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati Ukumbi namba 432.

Halafu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya *CPA* Tawi la Tanzania kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 9 saa tano asubuhi katika ukumbi chumba namba 219.

Halafu Mheshimiwa Juma Killimbah yeye ni Katibu wa *Amani Forum chapter* ya Tanzania anapenda kuwatangazia Kamati ya Utendaji wa *Amani Forum* leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika chumba 231. Kwa hiyo, wajumbe wa vikao hivyo waweze kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaendelea nimeambiwa hapa kwamba tarehe 11 saa tano asubuhi mpaka saa 8 Mzee Chifupa atakuwa na hitima ya mtoto wake Marehemu Mheshimiwa Mbunge Amina Clhifupa Mpakanjia. Nadhani matangazo mengine tutaambiwa jioni. Kwa sababu na Bunge wana kitu kama hicho. Sasa tutatangaza baadaye jioni.

Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee na shughuli za leo. Mheshimiwa Wabunge, sasa mtatambua kwamba tunakaribia mwisho. Sasa Wizara hii, leo ndiyo Wizara yake, wakati ule waliposoma Waziri wa Fedha na Mipango ilikuwa ni mipango ya nchi nzima katika mwaka unaohusika. Leo tunazamia kwenye Wizara ya Mipango na Uwezeshaji.

Kwa hiyo, leo tunazungumzia *vote* ya Waziri huyu. Maana wengine wanasema tutaongea namna gani. Leo mnaongea kama mlivyoongea Wizara zile nyingine. Kesho

tutakuwa na Wizara kama Wizara ya Fedha. Kwa hiyo, mnazungumza kama mnajadili Wizara na Mshahara wa Waziri upo leo. *(Makofi/Kicheko)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima na afya sote hapa Bungeni na hivyo kutwezesha kuhudhuria kikao hiki cha Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwasilishwa leo asubuhi kwa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi iliyochambua makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka 2007/2008, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu lijadili na hatimaye kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya kuchambua mapendekezo ya bajeti hii kwa makini na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali ya Bajeti inayopendekezwa. Ushauri wa Kamati umesaidia sana katika kuboresha bajeti ninayowasilisha leo mbele ya Bunge lako tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu nyingi kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa mchango wake mkubwa katika maandalizi ya bajeti hii. Aidha, napenda kutoa shukrani kwa Katibu Mkuu Balozi Charles K. Mutalemwa na Naibu Katibu Mkuu Bibi Joyce Mapunjo, Wakurugenzi, Viongozi wa Asasi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa juhudi na ushirikiano wao uliowezesha kutekeleza malengo tuliyojiwekea katika kipindi cha mwaka 2006/2007 na pia kukamilisha kwa wakati maandalizi ya makadirio ya bajeti ya mwaka 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na waheshimiwa wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Florence Kyendesya, kwa kuteuliwa kujaza nafasi ya Bunge iliyoachwa wazi na Mheshimiwa Dr. Asha – Rose Migiro.

Vilevile, napenda kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa na Waheshimiwa Mawaziri wengine kwa hotuba zao ambazo zimefafanua kwa kina utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali na kutoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa mwaka 2007/2008.

Kwa ujumla wake, mipango hiyo ina lengo kuu la kukuza uchumi na kupunguza umasikini na hivyo kuleta maisha bora kwa watanzania wote. Aidha, napenda kumpongeza na kumshukuru Jaji Mkuu mstaafu Mheshimiwa Barnabas Samatta kwa utumishi uliotukuka kwa Taifa letu na pia nampongeza Jaji Mkuu Mpya Mheshimiwa Augustino Ramadhani kwa kuteuliwa kushika wadhifa huo na naahidi kumpa ushirikiano kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru kutoka kwenye sakafu ya moyo wananchi wa jimbo la Ulanga Magharibi kwa kuendelea kunipa heshima na dhamana ya kuwa Mbunge wao. Nawahidi kushirikiana nao katika kusukuma maendeleo ya Jimbo letu na Wilaya yetu ya Ulanga na Mkoa mzima wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii pia kutoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia aliyekuwa mwakilishi wa Umoja wa Vijana, CCM. Kifo cha Mbunge huyu kimeleta majonzi makubwa kwa Bunge na Taifa letu kwa ujumla. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji yanalenga katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umasikini (MKUKUTA) na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Katika kufanikisha lengo hilo, Idara na Asasi zilizoko chini ya Wizara hii zinashirikiana katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yafuatayo:-

(i) Kuchambua na kubuni sera za uchumi jumla, kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi, pamoja na kuandaa miongozo ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji;

(ii) Kubuni, kufanya utafiti na uchambuzi wa masuala muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

(iii) Kuratibu, kuhimiza na kufuatilia masuala ya kuondoa umaskini;

(iv) Kuweka mazingira bora ili kuwezesha sekta binafsi kushamiri na kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii;

(v) Kuibua na kubainisha fursa za kuvutia uwekezaji;

(vi) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuratibu shughuli za uwezeshaji na kuongeza ajira;

(vii) Kuchambua na kufafanua sera na mikakati ya kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya kisekta; kama vile kuchambua na kuandaa sera na mikakati ya sekta ya nje; sera za kuendeleza rasilimali watu na sera na mikakati ya maendeleo vijijini;

(viii) Kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa na takwimu za kiuchumi na kijamii; na

(ix) Kujenga uwezo wa Wachumi na Watakwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji Wa Majukumu ya Wizara Kwa Mwaka 2006/2007 na Makusudio ya Mwaka 2007/2008 baada ya kutoa maelezo kuhusu majukumu ya Wizara yangu, pamoja na Asasi zake, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2006/2007 na makusudio ya mwaka 2007/2008 kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA), katika mwaka 2006/2007, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ilikamilisha Mpango Kabambe wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA (MKUKUTA *Monitoring Master Plan)*. Mpango huu unatumika kukusanya takwimu, kufanya uchambuzi na tafiti mbalimbali, pamoja na kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wadau mbalimbali kwa lengo la kupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA. Katika kipindi cha 2006/2007, Serikali imeendelea kuimarisha utekelezaji wa MKUKUTA kupitia bajeti yake kwa kuhakikisha kuwa programu za kitaifa na kisekta zote zinajielekeza katika kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kubaini mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika jitihada za kupambana na umasikini, ripoti mbalimbali ziliandaliwa na kukamilika katika mwaka 2006/2007. Ripoti hizo ni pamoja na: Ripoti ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu (PHDR1-2005); "MKUKUTA *Status Report 2006";* Ripoti ya Utekelezaji ya MKUKUTA 2005/2006; na Ripoti ya Utekelezaji ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2006. Aidha, Tovuti ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA *(www.poverty monitoring.go.tz.)* ilipitiwa kwa lengo la kuipa uwezo zaidi wa kutoa taarifa.

Hii ni pamoja na kuirahisisha kufikiwa na wadau wengi zaidi. Taarifa nyingi zaidi sasa zinaweza kupatikana katika tovuti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2007/08, Wizara yangu itaimarisha uratibu wa utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA kwa kuyawezesha Makundi Kazi *(Working Groups)* kukusanya takwimu na kufanya uchambuzi na tafiti mbalimbali za kupima mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika jitihada za kupambana na umasikini. Aidha, jitihada zitaendelea ili kuwaelimisha na kuwahamasisha wadau wote juu ya matumizi ya taarifa hizo katika kubuni, kupanga, kutekeleza na kufuatilia programu za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Maeneo mengine yatakayozingatiwa katika mwaka 2007/2008 kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa MKUKUTA ni pamoja na usimamizi na utoaji taarifa katika ngazi mbalimbali.

Wizara yangu itaendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali juu ya utayarishaji wa ripoti ya utekelezaji wa MKUKUTA katika maeneo yao kwa kutumia mfumo wa kompyuta (MKUKUTA *Reporting Software).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea kuratibu maandalizi ya Mwongozo wa Kinga ya Jamii *(Social Protection Framework)* kama sehemu ya utekelezaji wa MKUKUTA. Mwongozo wa Kinga ya jamii unalenga makundi ya jamii yenye uwezekano wa kuathirika kirahisi na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Makundi hayo ni kama vile watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI, wazee wasio na uwezo na watoto wachanga. Mwongozo huu utatoa maelekezo ya kutambua namna ya kuyashughulikia makundi hayo katika jamii yetu. Wizara yangu itaendelea kuratibu maandalizi haya katika mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imeendelea kujishirikisha na juhudi za kimataifa katika vita dhidi ya umaskini. Hii ni pamoja na kujenga mikakakti ya kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Katika mwaka 2006/2007, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP2),* iliendelea na utekelezaji wa dhana ya "Mfano wa Kijiji cha Milenia" *(Millenium Village Initiative)* ambayo lengo lake kuu ni kujifunza mbinu za utekelezaji wa malengo ya maendeleo ya milenia katika ngazi ya jamii. Kwa kuanzia, Mpango huu unatekelezwa katika Mkoa wa Tabora. Hadi sasa vijiji 15 vya Wilaya ya Uyui, Tarafa ya Ilolangulu katika Kata za Ilolangulu, Mabama, Ibiri na Usagari vyenye jumla ya kaya 6,000 na wakazi wapatao 33,000 inatekeleza dhana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 Mpango huu uliendelea kutekelezwa kwa kutoa mafunzo ya ujasiriamali na kuiwezesha jamii kiuchumi na kijamii *(community training and empowerment)*. Aidha, shughuli za utafiti wa magonjwa mbalimbali ulifanyika ambapo idadi ya vyandarua 21,000 vilisambazwa katika kaya 6,000 kwa ajili ya kujikinga na malaria. Vilevile, mbolea za kupandia na kukuzia zilisambazwa kwa wakulima na hivyo kuleta ongezeko la mavuno ya mahindi kutoka gunia mbili hadi nane hapo awali na kufikia magunia 15 mpaka 20 kwa ekari.

Vilevile, mradi umetoa ufadhili wa ada, malazi, vifaa vya masomo kwa watoto wanaotoka katika familia masikini, yatima na zisizoweza kujigharimia masomo ya sekondari. Hadi sasa mradi umetoa ufadhili kwa kugharamia masomo ya sekondari kwa wanafunzi 97 ikiwa ni wavulana 54 na wasichana 43 kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Katika mwaka 2007/2008, Mpango huu ukishirikisha jamii husika utaendelea kujenga uwezo wa jamii katika nyanja za ujasiriamali na usindikaji wa vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara iliendelea kuelimisha wananchi kuhusu jitihada mbalimbali za kupambana na umaskini kupitia vipindi vya redio, vipeperushi, majarida na machapisho mbalimbali na kwa kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT*). Wizara pia imetumia fursa zilizojitokeza kama vile semina na mikutano kuwaelimisha wadau mbalimbali juu ya matokeo ya mfumo wa ufuatiliaji wa MKUKUTA. Aidha, itakumbukwa kuwa mwezi Aprili 2007 Wizara yangu ilifanya semina ya mapitio ya bajeti na mafanikio ya utekelezaji wa MKUKUTA kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika semina hiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua Mpango wa Ufuatiliaji wa MKUKUTA na Ripoti ya Maendeleo ya Milenia 2006. Madhumuni ya jitihada hizi ni pamoja na kukuza uelewa na kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge wakiwa ni wawakilishi wa wananchi kushiriki zaidi katika kuboresha mipango na vipaumbele katika kutekeleza MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini – Tiger Plan 2020)* katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kuharakisha Maendeleo ya Tanzania kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji na kujenga miundombinu. Kazi zilizotekelezwa katika mpango huu ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa Eneo Maalum la Uwekezaji la *"Benjamin William Mkapa Special Economic Zone (BWM – SEZ)"* ambalo linatarajiwa kufunguliwa rasmi mwaka huu wa fedha baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha umeme. Jumla ya maombi kumi na tatu (13) ya makampuni ya uwekezaji yamekwishapokelewa ambapo kumi (10) ni ya wawekezaji wa hapa nchini na matatu ni ya wawekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wataalam wetu kwenye nchi zenye uzoefu wa kujenga na kuendesha Vituo Maalum vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*ICT – SEZs*) na upembuzi yakinifu ulikamilika kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha aina hiyo hapa nchini katika eneo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuharakisha maendeleo chini ya Mpango wa *Mini-Tiger Plan 2020*, Serikali ilisaini makubaliano ya pamoja na kampuni za *Oji Paper* na "Marubeni" kutoka Japani ili kuanza tafiti za maeneo yanayofaa kutumika kwa ajili ya kupanda miti ya kutengeneza karatasi na "woodchips" katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Maeneo sita ya vijiji vya Pangatena, Mahumbika na Rondo Mkoani Lindi na Kilombero, Msijute na Naliendele mkoani Mtwara, yameainishwa na mikaratusi isiyonyonya maji sana tayari imepandwa kwa majaribio. Lengo kubwa ni kuwashirikisha wananchi wa maeneo hayo kwenye upandaji miti kwa ajili ya biashara *(commercial afforestation)* ili kuwaongezea kipato na hivyo kupunguza umasikini. Dhana hii imetumika kwenye nchi nyingi za Kusini Mashariki mwa Asia kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, Serikali itakamilisha ujenzi wa Eneo Maalum la Uwekezaji la *BWM – SEZ* hususan kuweka miundombinu muhimu ya maji, umeme pamoja na kuweka samani kwenye majengo pamoja na kuendelea kulitangaza eneo hilo ndani na nje ya nchi ili kuvutia wawekezaji. Vile vile, kwa kuanzia upembuzi yakinifu unatarajia kuanza kwa ajili ya kuanzisha *SEZs* katika mikoa ya Tanga, Kigoma na Pwani.

Programu Maalumu za Kuunga Mkono Nguvu za Wananchi Katika Kupunguza Umasikini

Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo *(Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 *SELF* iliendelea kutoa huduma katika mikoa 14 ya Tanzania Bara na Mikoa yote mitano (5) ya Tanzania Zanzibar. Hadi Juni 30, 2007 mradi umekwishatoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.5 kwa *SACCOS* na *NGOs* zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo kwa wananchi. Jumla ya wilaya 83 zimefikiwa na huduma hii, na walionufaika na mikopo hiyo ni walengwa 52,750 ambao kati yao asilimia 60.1 ni wanawake. Mradi pia uliendelea kujenga uwezo wa asasi husika kwa kuzipatia mafunzo na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, *SELF* itaendelea na majukumu yake ya uhamasishaji, kutoa elimu kwa umma, kujenga uwezo kwa kuzipatia mikopo, mafunzo na vitendea kazi *SACCOS* na *NGOs* zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007 Programu ya Kuongeza Kipato *(Income Generation Programme)* iliendelea kutekeleza miradi yake ya kuboresha kipato cha wananchi katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara (Dodoma, Dar es Salaam, na Pwani) na Tanzania Zanzibar. Programu ilisaidia kuendeleza mashamba ya chumvi na kutoa mafunzo kwa vikundi vya wazalishaji wa chumvi Pemba. Aidha, programu ilisaidia kuunda na kutoa mafunzo katika vikundi vya wafuga nyuki na kununua vifaa vya kutunzia asali Wilayani Rufiji. Programu pia ilisaidia kikundi cha vijana cha Madale kilichoko Dar es Salaam kukarabati bwawa la maji, kununua mashine za umwagiliaji na kununua mashine ya kufyatua matofali inayotumia umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Programu ya Kuongeza Kipato itaendelea kukamilisha miradi ifuatayo:- ujenzi wa kiwanda cha kusindika chumvi na kukarabati mashamba ya chumvi yaliyoko Unguja na Pemba, ukarabati wa soko la Mwanakwerekwe Zanzibar, kuboresha shughuli za mradi wa ufugaji nyuki Rufiji na Dodoma Vijijini, na kuendeleza mradi wa Maendeleo ya Vijana ulioko Madale – Dar es Salaam. Programu ya Kuongeza Kipato itaendelea kufuatilia ufanisi wa miradi yote inayotekelezwa chini ya programu hiyo kabla ya kubuni na kufadhili miradi mipya katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu iliendelea kujenga uwezo wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa kutafuta ofisi na kuanza kukarabati jengo, kuajiri watumishi na kununua vitendea kazi. Pia, mipango mbalimbali inayochangia katika utekelezaji wa Sera ya uwezeshaji iliendelea kutekelezwa. Hii ni pamoja na: Mpango wa Kurasimisha Mali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Programu ya Kuongeza Kipato *(IGP3)* na Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*SELF*).

Kwa kushirikiana na benki ya *NBC,* mafunzo kwa wajasiriamali 360 kutoka mikoa 12 ya Tanzania yanaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu ambao ulitangazwa hapa Bungeni mwezi Agosti 2006 na Mheshimiwa Waziri Mkuu ulianza kutekelezwa rasmi mwezi Januari 2007. Ili kutekeleza Mpango huo, ambao unatekelezwa katika awamu mbili, kiasi cha shilingi bilioni 21 kilitengwa. Katika awamu ya kwanza, kiasi cha shilingi bilioni 10.5 kilitolewa na kutumika kama dhamana kupitia benki za *NMB* na *CRDB* ili kuwakopesha wajasiriamali wadogo, wa kati na *SACCOS*. Katika makubaliano Benki hizo zinakopesha mara tatu ya kiasi cha dhamana iliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa Mpango huu imeonyesha jinsi wananchi walivyo na kiu ya maendeleo kwa namna walivyojitokeza kwa wingi kuomba mikopo kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2007, jumla ya maombi ya mikopo 89,589 yenye thamani ya shilingi bilioni 162.7 yalipokelewa na *NMB*, kati ya hayo maombi 15,895 yenye thamani ya Shilingi bilioni 15.3 yalipewa mikopo. Aidha, katika kipindi hicho *CRDB* ilipitisha maombi 12,176 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.14. Hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2007 benki zote mbili zilikuwa zimekopesha jumla ya shilingi bilioni 25.74, ambazo ni asilimia 82 ya kiasi kilichotarajiwa kukopeshwa. Hadi Juni 30, 2007 hali ya urejeshaji wa mikopo ilidendelea vizuri. Benki ya *NMB* imeweza kukusanya marejesho ya mikopo iliyokuwa imeiva *(installment due)* kwa kipindi hicho kwa asilimia 91.45 wakati benki ya *CRDB* iliweza kukusanya marejesho kama hayo kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango huu changamoto nyingi zilijitokeza ikiwa ni pamoja na kuwepo uelewa mdogo wa wananchi kuhusu dhana ya mikopo hiyo; elimu ndogo ya ujasiriamali; ukosefu wa vitendea kazi; upungufu wa maafisa/wataalam wa mikopo kwenye wilaya na katika matawi ya benki; ukosefu wa matawi ya benki katika baadhi ya makao makuu ya wilaya na ukosefu wa miundombinu. Ili kukabiliana na changamoto hizo Serikali, iliendesha mafunzo maalum kwa maafisa wasiopungua watatu kutoka kila Halmashauri ili waweze kusambaza elimu hiyo na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, Serikali iliwateua waratibu katika kila Halmashauri ili waweze kufuatilia utekelezaji wa Mpango huu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya Pili ya Mpango, huu itaanza mwaka huu wa fedha mara taratibu zitakapokamilika. Katika awamu hii jumla ya shilingi bilioni 10.5 zilizobakia zitatolewa kwa benki zenye mitaji midogo na taasisi za huduma za fedha zitakazoteuliwa na Serikali kwa ajili ya kutoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa. Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali inakamilisha mchakato wa kuzipata benki na taasisi za huduma za fedha zitakazotumika katika mfumo huu. Serikali inaendelea kusisitiza na kuwataka wakopaji wote warejeshe mikopo yao kwa wakati ili fedha hizo ziweze kuzunguka na kukopeshwa wajasiriamali wengine wanaosubiri kukopeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08 utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi utaendelea kwa kuanzisha daftari (*register*) la kuandikisha vikundi mbalimbali vya wananchi vinavyofanya shughuli za kiuchumi kwa lengo la kufuatilia na kufanya tathmini ya maendeleo ya kiuchumi na kutoa msaada utakaohitajika kulingana na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na taasisi zenye uwezo, tafiti mbalimbali zitafanyika katika sekta za kiuchumi ili kubaini maeneo yenye fursa zinazoweza kuleta mafanikio au matokeo ya haraka katika maendeleo ya kiuchumi. Aidha, kazi ya kuieneza na kuifafanua Sera ya Uwezeshaji pamoja na sheria yake itafanyika kwa kutumia vyombo vya habari, mikutano, vipeperushi, n.k. kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanaielewa vema Sera na sheria ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Serikali itaendelea kuelimisha, kuhamasisha na kutoa taarifa muhimu zitakazowezesha wananchi kutambua fursa za uwezeshaji katika vyombo na taasisi mbalimbali. Kwa kushirikiana na taasisi zenye uzoefu katika nyanja ya ujasiriamali, Serikali itatoa mafunzo kwa wajasiriamali kwa kila mkoa wa Tanzania Bara. Lengo ni kuwawezesha na kuwapa wananchi uwezo wa kubuni na kuibua miradi itakayowaletea maendeleo ya haraka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Uwekezaji Rasilimali Nchini, katika mwaka 2006/2007 Wizara yangu kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kushirikiana na viongozi wa kitaifa iliandaa ujumbe wa Watanzania wenye miradi inayofaa kuwekeza kwenda nchi mbalimbali. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kutangaza fursa za uwekezaji na kunadi miradi ya Watanzania kwa lengo la kuwavutia wageni kuja kuwekeza hapa kwetu. Nchi zilizotembelewa ni pamoja na Marekani, China, Japan na Korea ya Kusini. Nchi nyingine ni *Oman, Canada, Thailand, Vietnam*, Urusi, Australia, Nchi za Falme za Kiarabu na Nchi za Scandnavia. Ziara hizo ziliwakutanisha wafanyabiashara wa Tanzania na wenzao katika kukuza biashara baina yao, kutafuta ubia, teknolojia ya kisasa na masoko. Vile vile Kituo kilipata fursa ya kuitangaza Tanzania na vivutio vyake kwa nchi zilizotembelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kuwafuata wawekezaji huko waliko, Tanzania ilipokea wawekezaji kutoka, Japan, Marekani, China, India, Ujerumani, Canada, Korea, Thailand, Afrika Kusini, Zimbabwe, Uingereza na Italia waliokuja kwa lengo la kuangalia mazingira ya uwekezaji hapa Tanzania. Katika mwaka 2006/2007 Kituo kiliidhinisha miradi 592 yenye thamani ya Shilingi milioni 52,764,760 (au dola za kimarekani milioni 43,970) inayokadiriwa kutoa nafasi za ajira 68,238. Mchanganuo unaonyesha kuwa kati ya miradi hiyo, miradi 304 ni ya watanzania, miradi 135 ni ya wageni na miradi 153 ni ya ubia. Sekta ya Utalii ndiyo iliyopata miradi mingi zaidi, ikiwa na miradi 186.

Sekta nyingine zilizovutia wawekezaji wengi ni pamoja na sekta ya viwanda iliyopata miradi 166, sekta ya Ujenzi wa Nyumba za Biashara miradi 83, sekta ya Usafirishaji miradi 68, sekta ya Kilimo miradi 30 na sekta ya Uendelezaji Rasilimali Watu miradi 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea kuimarisha mahusiano na mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha moja kwa moja na masuala ya uwekezaji. Mashirika hayo ni: *MIGA4, UNCTAD5, WAIPA6, UNIDO7, EABC* na Benki ya Dunia. Aidha, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kiliendelea kuimarisha mahusiano na vituo vingine vya uwekezaji barani Afrika (*IPAs*8) kwa lengo la kubadilishana uzoefu. Pia Kituo

kiliendelea kufanya kazi kwa karibu sana na balozi zetu ikiwa ni pamoja na kuandaa mikutano ya uwekezaji iliyofanyika katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha uwekezaji wa ndani Kituo kiliendesha semina katika Mikoa ya Ruvuma, Mara na Rukwa kwa nia ya kuwahamasisha wananchi kuwekeza katika fursa zilizopo ndani ya mikoa yao. Sambamba na kuendesha semina Kituo kimeshirikiana na mikoa hiyo kuandaa *Regional Profiles* zenye kuainisha rasilimali zilizopo kwa uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na uongozi wa mikoa hapa nchini ziliendelea na zoezi la kuainisha maeneo ya ardhi yanayofaa kuwekeza katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Lindi, Mtwara na Dar es Salaam. Aidha, juhudi za kuainisha maneo katika mikoa mingine inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio niliyoyaeleza kuhusu jitihada za Serikali kuwavutia wawekezaji ni ya kujivunia. Mafanikio hayo yamekiwezesha Kituo cha Uwekezaji Tanzania kupata tuzo ya *IPA* kwa kuwa kituo cha kwanza bora kati ya nchi 160 zilizofanyiwa tathmini duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uwekezaji itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje katika sekta ambazo zitalipatia Taifa nguvu ya ushindani na ambazo zitasaidia katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi kwa haraka zaidi kwa kutumia Dhana ya Kulenga Mwekezaji *(Investor Targeting Approach).*

Kituo kitaendelea kutoa huduma madhubuti na za haraka kwa mtindo wa *One Stop Center* kwa wawekezaji wote. Aidha, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini kupitia Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaongeza juhudi katika kutathmini mafanikio ya juhudi za kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kubaini matatizo na vikwazo vinavyowakabili wawekezaji kwa lengo la kuyatatua. Katika hatua za kusogeza huduma karibu na wananchi, Kituo cha Uwekezaji kiko katika hatua za mwisho za kufungua ofisi ya Kanda ya Kusini Mkoani Mbeya.

Ofisi hii itakuwa ya tatu kufunguliwa kikanda baada ya Mwanza na Kilimanjaro na itatoa huduma kwa mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. Ofisi ya kanda ya Mbeya inatarajiwa kutoa huduma mbalimbali kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuwatafutia wabia; kutayarisha michanganuo ya miradi kwa ajili ya kupata mikopo benki; kutoa elimu ya kukuza ujasiriamali na kuwaelimisha wananchi juu ya fursa mbalimbali za kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Serikali itaandaa mikutano miwili ya kuvutia uwekezaji. Mkutano wa kwanza ni *African World Business Congress*

utakaofanyika Arusha kuanzia tarehe 10 – 13 Novemba 2007. Mkutano huo unalenga kuinadi Tanzania kama eneo bora zaidi la kuwekeza na pia kuwavutia wawekezaji. Mkutano mwingine ni ule unaoandaliwa kati ya Tanzania na *Africa - Australia Business Council* utafanyika mwezi Machi 2008 Dar es Salaam. Mkutano huo utajulikana kama *Australia – Tanzania Trade and Investment Conference* unatarajia kujikita kwenye uwekezaji mkubwa wa kilimo, miundombinu ya utalii na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uratibu wa Mashirika Yaliyobinafsishwa na Usimamizi wa Ubinafsishaji wa Mashirika Yaliyobaki, katika mwaka 2006/2007, Wizara yangu kupitia Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma iliendelea kutoa elimu ya ubinafsishaji kupitia vipindi vya redio, televisheni, warsha, makongamano, jarida na vipeperushi.

Aidha, Tume iliendelea kuwafanyia tathmini wawekezaji wote wanaokusudia kuwekeza kwenye mashirika hayo ili kubaini uwezo wao kiutendaji, kibiashara na kifedha. Tume iliendelea kuimarisha ufuatiliaji wa utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa; na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wawekezaji walioshindwa kutekeleza mipango ya uwekezaji kulingana na mikataba ya mauzo.

Vilevile, Tume iliajiri wataalamu wa kukusanya madeni kutoka kwa wawekezaji ambao bado hawajamaliza malipo kufuatana na mikataba; kuajiri mtaalamu wa masuala ya ardhi kwa ajili ya kufuatilia upatikanaji wa hati miliki; na kuuza hisa za mashirika kupitia Soko la Hisa la Dar es Salam ili kuwawezesha wananchi wenye mitaji midogo waweze kununua hisa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa 2006 jumla ya mashirika 10 yalibinafsishwa katika ngazi ya makubaliano ya awali. Aidha, mali zisizo makampuni (*non core assets*) 22 ziliuzwa katika kipindi hicho. Jumla ya mashirika 12 yalibinafsishwa katika ngazi ya mkataba wa mauzo *(Final Sales Agreement).*

Pia, kampuni ya Ndege ya *ATCL* ilirudishwa katika miliki ya Serikali kwa asilimia mia. Hadi Juni 30 2007 jumla ya Mashirika ya Umma 336 na mali za mashirika 660 yalikuwa yamebinafsishwa .

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma inatarajia kukamilisha kazi iliyobaki ya ubinafsishaji katika muda wake unaoisha tarehe 31 Desemba 2007. Kwa sasa Serikali inatafakari kuhusu mfumo unaofaa wa ufuatiliaji wa mashirika yaliyobinafsishwa baada ya Tume kumaliza muda wake. Sasa ni kuhusu Uendelezaji wa Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Majadiliano kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Katika mwaka 2006/2007, Baraza la Taifa la Biashara *(Tanzania National Business Council, TNBC)* lilifanya mikutano mitatu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mikutano hiyo ni: Mkutano wa Nne wa Baraza (*TNBC* 4); Mkutano wa Pili wa Wawekezaji wa Ndani (*LIRT* 2) na Mkutano wa Sita wa Wawekezaji wa Kimataifa (*IIRT* 6).

Madhumuni ya mikutano hiyo ilikuwa kuendeleza mashauriano kati ya Serikali na Sekta binafsi yenye lengo la kukuza sekta binafsi, kuboresha mazingira ya kufanya biashara nchini na kukuza hali ya uwekezaji nchini. Mapendekezo yatokanayo na mazungumzo ya mikutano hiyo hufanyiwa kazi zaidi na vikundi kazi *(Working Groups)* vya kitaalamu vikiongozwa na Sekretarieti ya Baraza kwa lengo la kuyafikisha kwenye ngazi ya maamuzi Serikalini pale panapohusika. Vikundi hivyo ni Uwezeshaji, Kilimo; Fedha; Miundombinu na Teknolojia; Viwanda; Ardhi, Utalii; na Rasilimali Watu. Aidha, Baraza la Taifa la Biashara liliendeleza ushirikiano na mashauriano na Baraza la Biashara la Tanzania Zanzibar (*ZBC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Juni 30, 2007, Serikali kupitia Baraza la Biashara la Taifa imeanzisha Mabaraza ya Biashara ya Mikoa katika Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara. Madhumuni ya mabaraza ya mikoa ni kuendeleza shughuli za Baraza la Taifa la Biashara kwa kupanua wigo wa mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ili kuboresha mazingira ya biashara na kukuza uwekezaji katika ngazi ya Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya matunda yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mashauriano kati ya Serikali na Sekta Binafsi ni pamoja na: uzinduzi na kuanza kutekelezwa kwa mradi wa Kuleta Ushindani katika Sekta Binafsi *(Private Sector Competitiveness Project – PSCP);* utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania – (MKUMBITA); kuanzishwa kwa Mfuko wa Kuwasomesha wataalam wa kitanzania wenye vipaji maalum unaofadhiliwa na wenye makampuni makubwa nchini pamoja na Benki ya Dunia na Serikali *(CEO Scholarship Fund);* mabadiliko ya taratibu na sheria za ajira; kuboresha taratibu na sheria ya ardhi; kuanzisha mfumo wa usajili kwa kompyuta katika Mamlaka ya Usajili wa Biashara na Utoaji Leseni (*BRELA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Baraza la Taifa la Biashara litaendelea kuimarisha mashauriano kati ya Serikali, Sekta Binafsi na wadau wengine nchini katika ngazi ya kitaifa na ya kimataifa kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji. Vikundi kazi *(Working Groups)* katika ngazi ya taifa na mikoa vitaimarishwa ili kutoa ushauri wa utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa katika ngazi husika. Aidha, Baraza litaendelea kusimamia uendeshaji wa mabaraza ya biashara ya mikoa kwa madhumuni ya kuyawezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBITA) Katika mwaka 2006/07, Programu ya MKUMBITA kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi husika iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuboresha mazingira ya kufanyia biashara Tanzania kama ifuatavyo:

(i) Sheria mpya ya Uandikishaji wa Biashara *(Business Activities Registration Act – BARA),* ambayo mtekelezaji na msimamizi mkuu ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Januari 2007. Sheria hii inalenga kupunguza ukubwa wa sekta isiyo rasmi kupitia uandikishaji wa biashara na utoaji leseni

za biashara kwa urahisi na kwa gharama nafuu zaidi, na hivyo kuifanya sehemu ya sekta rasmi

(ii) Kuendesha mafunzo ya Upembuzi Yakinifu *(Regulatory Impact Asssessment)* kwa Wabunge, Makatibu Wakuu wa Wizara na Makatibu Tawala wa Mikoa, Kamati na Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Wakurugenzi wote wa Wizara, Idara na Taasisi zote zinazotekeleza programu ya MKUMBITA.

Mafunzo hayo yalilenga kuwatayarisha watunga sera na sheria kutambua faida zitokanazo na maboresho na marekebisho ya sera, sheria na kanuni yanayoendelea nchini.

(iii) Kuanza utekelezaji wa mradi wa utatuzi wa mlundikano wa kesi za migogoro ya ardhi jijini Dar es Salaam ambapo mtekelezaji mkuu wa mradi huu ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Uchambuzi uliofanywa na Wizara husika ulibaini kuwepo kwa mlundikano mkubwa wa kesi za muda mrefu. Jiji la Dar es Salaam lilionyesha kuwepo karibu asimilia 50% ya mlundikano wa kesi za ardhi kuanzia mwaka 2004. Ufanisi wa mradi huu utakuwa mfano wa kuigwa kwa mikoa mingine yenye matatizo kama hayo kama vile Mbeya, Arusha, Mwanza, Kagera, Kilimanjaro na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Programu ya MKUMBITA kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi zinazohusika itaendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kukamilisha utengenezaji wa kanuni za Sheria mpya ya Uandikishaji Biashara (BARA9 *Regulations*) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

(ii) Kuendesha Mafunzo ya Upembuzi Yakinifu *(Regulatory Impact Assessment)* kwa Makatibu Wakuu, Baraza la Wawakilishi na Makatibu Tawala wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Majadiliano yanaendelea ili kuingiza mafunzo ya *Regulatory Impact Assessment (RIA)* katika mitaala ya kufundisha wanafunzi wa shahada ya kwanza na ya pili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(iii) Katika kupata uzoefu na *Best Practice* ya mfumo huu wa upembuzi yakinifu, Programu ya MKUMBITA itapeleka baadhi ya maofisa kwenye mafunzo nje ya nchi ili kupata ujuzi na kuweza kufundisha watu wengi nchini.

(iv) Kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya kibiashara kwa kupeleka huduma za Kitengo cha Mahakama ya Biashara mikoani kama vile Mwanza, Mbeya na kwingine.

Pia katika juhudi za kupanua matumizi ya mtandao wa kompyuta katika kuendesha kesi za biashara, mkutano mkubwa utakaojumuisha Majaji wa Canada, India, Malaysia na Uingereza unatazamiawa kufanyika nchini ili kubadilishana uzoefu na ujuzi.

(v) Kundeleza utelekezaji wa mpango wa marekebisho ya sheria na kanuni mbalimbali za ardhi. Vile vile kupeleka mpango wa kusuluhisha na kutatua mlundikano wa migogoro ya ardhi mikoani baada ya ule wa jiji la Dar es Salaam, kwa kuanza na Arusha na Mbeya na baadaye kwenda mikoa mingine ya Manyara, Kilimanjaro, Mwanza, Kagera na Tanga.

(vi) Kuboresha Masjila za Wakala wa Biashara na Leseni (*BRELA*) kwa kutumia kompyuta katika kutunza kumbukumbu.

(vii) Kuimarisha mfumo wa Uandikishaji wa Vizazi na Vifo chini ya usimamizi wa *RITA*; na

(viii) Kutekeleza Mradi wa Kitambulisho cha Taifa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kukusanya, sasa ni kuhusu Kuchambua, Kutunza na Kusambaza Taarifa na Takwimu za Kiuchumi na Kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006, Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ambayo ni maboresho ya Sera ya mwaka 1992 ilipitishwa. Mwezi Februari 2007, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliizindua Sera hii pamoja na kuutangaza rasmi Mkutano wa Tano wa Afrika wa Idadi ya Watu utakaofanyika mwezi Desemba 2007.

Lengo kuu la Sera hii ni kuratibu na kuhuisha sera, mikakati na programu nyingine ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya watu yanapatikana, pamoja na kukuza usawa wa kijinsia na kufanikisha uwezeshaji wa wanawake. Aidha, Mkutano wa Tano wa Afrika wa Idadi ya Watu utawakutanisha watafiti na watunga sera ili kujadili masuala ya idadi ya watu na maendeleo, na changamoto zilizopo Barani Afrika ili ziweze kujumuishwa katika ajenda za maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na kukamilisha mkakati wa Utekelezaji wa Sera na kuendelea na uandaaji wa utafiti wa hali ya utumishi nchini. Aidha, Wizara pia itaendelea kuandaa na kusimamia kufanyika kwa Mkutano wa Tano wa Afrika unaohusu Idadi ya Watu na Maendeleo utakaofanyika Arusha hapo tarehe 10-14 Desemba 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/2007, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kuchapisha na kuwasilisha takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Takwimu za Pato la Taifa kwa kila nusu mwaka kwa kipindi cha Julai hadi Desemba 2006 zilitolewa.

Zoezi la ukamilishaji wa Safu Mpya ya Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2001 na kutumia mfumo mpya wa Umoja wa Mataifa *(10SNA1993)* lilifanyika na utayarishaji wa takwimu za Hali ya Uchumi kwa mwaka 2006 umekamilika.

Aidha, Wizara imehakikisha kuwa tafiti mbalimbali zimeendelea kufanyika ipasavyo kama zilivyoainishwa katika MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kukusanya na kuchambua takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii. Aidha, tafiti mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango Kabambe wa Kufuatilia Hali ya Umaskini *(MKUKUTA Monitoring Master Plan)* nchini zitafanyika ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kutenga na kuingiza maeneo ya kuhesabia watu kwenye kompyuta *(GIS)* ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika mwaka 2012;

(ii) Kukusanya na kuchambua takwimu za mazingira;

(iiii) Kutayarisha taarifa za hali ya uchumi na maendeleo ya jamii za mikoa na hali ya uwekezaji mikoani;

(iv) Utafiti wa hali ya watu wenye ulemavu;

(v) Kufufua ukusanyaji wa takwimu za uhalifu nchini kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi;

(vi) Utafiti kuhusu Hali ya Viashiria vya VVU/UKIMWI Tanzania *(HIV/AIDS Indicator Survey);*

(vii) Kukamilisha Mfumo wa Kitaifa wa Ukusanyaji wa Takwimu zilizo rasmi *(Tanzania Statistical Master Plan);*

(viii) Ufuatiliaji wa ajira mpya zitokanazo na Shilingi bilioni 21 za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; na

(ix) Kutekeleza tafiti nyingine kama zilivyoainishwa kwenye MKUKUTA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujenga uwezo wa wachumi na watakwimu, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika, kiliendesha mafunzo ya Cheti na Stashahada ili kuboresha ukusanyaji, uchambuzi, utunzaji na matumizi ya takwimu.

Chuo kilisajili jumla ya Wanachuo 67 kutoka nchi mbalimbali za Afrika kama ifuatavyo:-

Wanachuo kutoka Sudan 4, Uganda 3, Afrika Kusini 4, Namibia 1, Tanzania Bara 41 na Tanzania Zanzibar 14. Kati ya hao wanawake ni 16 na wawili kati yao wanatoka nje ya nchi, yaani Namibia na Afrika Kusini. Wanachuo 14 kutoka Tanzania Bara walifadhiliwa na Wizara yangu katika mpango wa kuboresha mfumo wa kukusanya na kuchambua takwimu za kiutawala chini ya MKUKUTA.

Mbali na kozi ndefu, Chuo pia kiliendesha mafunzo ya muda mfupi ya Mbinu za Utafiti wa Kitakwimu kwa walimu 16 wa Chuo cha Mamlaka ya Kodi Tanzania, na mafunzo ya Mbinu za Uchambuzi na Uandaaji wa Taarifa kwa washiriki 28 kutoka nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika kitaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya takwimu katika kiwango cha cheti na stashahada kwa lengo la kuboresha ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu katika mipango mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma, kiliendelea na ujenzi wa maktaba kubwa yenye uwezo wa kuhudumia watumiaji 600 kwa wakati mmoja. Chuo pia kilianza ujenzi wa jengo la kwanza la taaluma, jengo la ukumbi wa matumizi mbalimbali na uzio kuzunguka eneo la Chuo.

Kwa upande wa taaluma, jumla ya wanachuo 1,055 walihudhuria mafunzo mbalimbali yakiwemo mafunzo ya cheti, Stashahada na Stashahada ya Juu, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Aidha, mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali yalitolewa.

Chuo kimechaguliwa na Serikali kuwa miongoni mwa vyuo muhimili vitakavyosaidia kuzijengea uwezo wa Serikali za Mitaa katika nyanja za maendeleo ya miji na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008 Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma, kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi na kitaanzisha shahada ya kwanza katika maendeleo ya kifedha na mipango ya uwekezaji.

Aidha, shughuli za utafiti na uelekezi kwa mamlaka za Serikali za Mitaa zitaimarishwa. Chuo kitaelekeza juhudi zake katika kuimarisha uwezo wa kupanga, kutathimini na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya na Manispaa kwa lengo la kuboresha upangaji na utekelezaji mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo hivyo viwili vitaendelea kuimarishwa kwa kukarabati miundombinu iliyopo na kuongeza baadhi ya huduma kwa kujenga majengo mengine kwa ajili ya matumizi ya kitaaluma.

Aidha, Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika kitashiriki katika kutoa mafunzo kwa ajili ya Mpango wa Ulinganisho wa Bei Kimataifa *(International Comparison of Prices, (IPC – Africa).* Vile vile, Chuo cha Takwimu kitafanya mapitio ya mitaala yake na kuandaa mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika hitimisho, baada ya kueleza hayo, napenda kuchukua fursa hii ili kutoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali ambao wamekubali na wamendelea kuisaidia Serikali ya Tanzania kugharamia miradi mbalimbali kupitia Bajeti ya Wizara yangu. Wahisani hao ni pamoja na *WB1, UNDP, DFID2, DANIDA3, UNFPA4, USAID5, SWISS Development Cooperation*, Norway na Japan.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/08, wizara yangu itaendelea kuhimiza ukuaji shirikishi na endelevu wa uchumi kupitia usimamizi thabiti na sahihi wa uchumi na kutoa miongozo yenye lengo la kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Aidha, kama inavyoonyeshwa katika dira ya Wizara yangu, Wizara itaongeza juhudi katika kutekeleza majukumu yake na kuwa Kituo Rejea *(Centre of Excellence)* katika usimamizi wa uchumi na maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2007/2008 sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya bajeti ya shilingi 75,150,654,000 (bilioni sabini na tano, milioni mia moja na hamsini, na mia sita hamsini na nne elfu) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji pamoja na Asasi zilizo chini yake kwa mwaka 2007/2008 kwa mchanganuo ufuatao:-

Fedha zinazoombwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 53,709,000,000 (bilioni hamsini na tatu, na milioni mia saba na tisa) ambazo kati ya hizo shilingi 15,718,000,000 (bilioni kumi na tano, na milioni mia saba na kumi na nane) ni fedha za ndani ya nchi yetu na shilingi 37,991,000,000 (bilioni thelathini na saba, na milioni mia tisa tisini na moja) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie:-

Fedha zinazoombwa kwa ajili ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni shilingi 21,441,654,000 (bilioni ishirini na moja, milioni mia nne na arobaini na moja, na mia sita na hamsini na nne elfu).

Kati ya fedha hizo, shilingi 6,337,935,000 (bilioni sita, milioni mia tatu na thelathini na saba, na mia tisa thelathini na tano elfu) ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 15,109,719,000 (bilioni kumi na tano, milioni mia moja na tisa, na mia saba na kumi na tisa elfu) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA :** Ahsante sana. Hoja imetolewa na kuungwa mkono. Sasa nitamwita Msemaji wa Kamati iliyohusika na Wizara hii, yuko wapi? Msemaji wa Kamati hii, Mheshimiwa Malima, Makamu Mwenyekiti. Huwa tunapenda wale wanaozungumza wakasogea karibu inakuwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

**MHE. ADAM K.A. MALIMA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 81(1) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba sasa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kufanya hivyo naomba nami nitumie fursa hii, kutoa salamu za rambirambi kwa familia zote zilizokumbwa na misiba mbalimbali iliyotokea wakati huu wa Kikao cha Bajeti ikiwa ni pamoja na familia ya Mzee Chifupa, kwa kupotelewa na Mbunge mwenzetu, Amina Chifupa Mpakanjia na familia za Wajumbe wa Bodi ya Nyanza na Mbunge za zamani, Mheshimiwa Stephen Kazi, waliofariki katika ajali ya gari, familia ya Mbunge wa zamani, Mheshimiwa Chubi, pamoja na familia za Marehemu wa ajali za mabasi za Singida, Mbeya na Arusha. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote hao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 6/6/2007 Kamati yangu ilipata fursa ya kukutana na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji Mheshimiwa Dr. Juma H. Ngasongwa, Alhaji, pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara kutoka Idara mbalimbali za Wizara hiyo. Kamati yangu ilipitia, ilichambua na kujadili Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007 na Taarifa ya Shabaha na Malengo ya Wizara hiyo kama ilivyo kwenye Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2007/2008.

Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wasaidizi wao wote kwa kazi nzuri na za kuridhisha walizofanya kwa Kipindi chote cha mwaka jana na matayarisho ya Bajeti ya Mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunakamilisha hotuba hii tulikuwa tumedhamiria tumpelekee salamu za kumtakia kupona haraka Mwanakamati mwenzetu Mheshimiwa Naibu Waziri Gaudance Kayombo. Nimekuja na maelezo haya lakini sasa nimegundua kwamba yupo, kwa hiyo, naomba nafasi hii kumkaribisha na kumtakia kila la kheri na afya njema na awe katika ujenzi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara kwa mwaka 2006/2007. Kamati imebaini kuwa Wizara imefanikiwa kutekeleza majukumu na malengo yake katika Mwaka wa Fedha 2006/2007, kutokana na kiasi cha fedha walichotengewa mwaka jana cha jumla ya Shilingi bilioni 23 kwa Matumizi ya Kawaida, hata hivyo kiwango hicho kilipunguzwa kwa shilingi bilioni 3.4 na kuwa shilingi 19.76.

Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 17 zilitengewa kwa ajili ya mishahara, matumizi mengine, pamoja na ruzuku kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2006/2007 Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni .12 fedha za ndani na bilioni 37 fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi

Mei, 2007 Sh.12,063,993,250/= sawa na asilimia 98.7 ya fedha za ndani zilizotengwa, na Sh.11,254,436,641/= sawa na asilimia 30.12 ya fedha za nje zilizotengwa, zilitolewa. Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2006/2007 ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango Maalum wa Kuboresha Maendeleo ya Tanzania *(Tanzania Mini-Tiger Plan – 2020),* Kamati imeona kuwa kasi ya utekelezaji wa Mpango Maalum wa kuharakisha Maendeleo wa nchi yetu kwa lengo la kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje kwa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji na kujenga miundombinu itakayovutia Wawekezaji ni mdogo.

Jitahada zinazofanyika ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa mpango huu kusaidia Taifa letu katika kuibua uchumi wake, ni lazima zifanane na mwelekeo mzima wa Taifa letu na ari mpya na malengo ya Kiuchumi. Nyingi ya programu zilizowekwa chini ya Mpango huu bado hazijaonyesha dalili za kupiga hatua zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana 2006, Kamati ilipitisha Muswada wa Sheria wa kuweka utaratibu utakaosimamia uanzishwaji, uendeshwaji na usimamizi wa maeneo maalum ya uwekezaji rasilimali *(Special Economic Zones – SEZs)*. Hadi sasa ni takribani mwaka mmoja na nusu umekwisha tangu Bunge hili lilipopitisha Muswada huo.

Hivyo Kamati ilitegemea kupata taarifa ya maeneo maalum yaliyoanzishwa kwa kuboresha miundombinu kama ujenzi wa barabara, huduma za umeme, simu, maji, n.k. ukiondoa eneo ambalo limezungukwa au limetajwa la Benjamin Wiliam Mkapa *(Special Economic Zone – BWM – SEZ)* lililoko Mabibo Dar-es-Salaam. Kamati inazingatia kwamba wakati wa kupitisha Muswada huo *sales* hizi zilikuwa ziende maeneo mbalimbali ya Tanzania ikiwa ni pamoja na Kigoma, Tanga na maeneo mengine ambayo yana *potential* ya biashara za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA),Wizara imeendelea pia kutekeleza majukumu na malengo yake kwa kukamilisha mpango wa ufuatuliaji wa MKUKUTA *(MKUKUTA Monitoring Master Plan)* ambao unatumika kama nyenzo ya kupima matokeo ya utekelezaji wa MKUKUTA kwa kukusanya takwimu, kufanya uchambuzi na tafiti mbalimbali na kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na Wadau mbalimbali.

Kamati inakumbusha kauli ya Mheshimiwa Rais alipotembelea Wizara hii, ya kwamba Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ndio ubongo wa Serikali. Maana ya Kauli hiyo ni kwamba uratibu wa mikakati ya kiuchumi ya Kitaifa *(National Economic Strategic Coordination)* inatakiwa isimamiwe na Wizara hii. Kamati imeishauri Wizara kwamba ili majukumu haya yatekelezeke ni lazima kuwe na mikakati ya kuboresha viwango vya tathmini na tafiti za Kiuchumi ndani ya Wizara kwa kujenga uwezo wa kitaaluma *(Technical Capacity Building)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Programu ya Kuunga Mkono Nguvu za Wananchi katika Kupunguza Umaskini, kwa kutambua tatizo la ajira linaloikabili nchi yetu, Serikali imetekeleza Mradi wa kutoa mikopo kwa Wajasiriamali wadogo au *(Small*

*Entrepreneurs Loan Facility – SELF)* ambapo kufikia tarehe 31 Machi 2007 Mradi huo ulikuwa umekwishatoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.5 bilioni. Jumla ya Wilaya 83 zimefikiwa na huduma hii na walengwa 52,950 ambao kati yao asilimia 60.1 ni Wanawake, wamenufaika na mikopo hiyo.

Vile vile katika mwaka 2006/2007 Programu ya kuongeza kipato iliendelea kutekeleza yaani ile *income general programm* iliyotajwa, iliendelea kutekeleza miradi yake ya kuboresha kipato cha Wananchi katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara (yaani Dodoma,

Dar-es-Salaam na Pwani) pamoja na Tanzania Zanzibar kwa kusaidia kuendeleza mashamba ya chumvi na kutoa mafunzo kwa vikundi vya wazalishaji wa chumvi Pemba; hata hivyo, pamoja na malengo mazuri sana ya programu kama hizi Kamati inaamini kwamba ni lazima ziwe na manufaa ya kuonekana na endelevu, *meaningful and sustainable* na isiwe na sura ya utekelezaji wa juu juu, tathimini za kina ni lazima zifanywe ili walengwa wanufaike kwa kuona hali zao za kimaisha zinabadilika kwa ushiriki wao katika programu hizi. Kamati inaamini kuwa ni Watanzania wengi wanahitaji misaada kama hii, hivyo ni vema Programu hii pamoja na hizi zingine zisambazwe mikoa yote badala ya mikoa michache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia viashiria vya Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(MDGS)* kama ilivyoainishwa katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga uwezo wa jamii ili ziweze kutumia fursa zilizopo - kubuni, kutekeleza na kufuatilia miradi ambayo itachangia kuboresha hali ya maisha yao. Katika kipindi cha Miaka Mitano kuanzia 2005 – 2009 awamu ya pili ya *TASAF.*

Hadi Machi 2007 jumla ya miradi 1,646 ilikwishapatiwa fedha na kati ya miradi hiyo kuna miradi kwa ajili katika mazingira magumu, miradi ya huduma za jamii na miradi ya kusaidia jamii zenye upungufu wa chakula.Utekelezaji wa Mpango wa Kuwawezesha Wananchi na Kuongeza Ajira. Kamati imefuatilia kwa karibu utaratibu uliowekwa wa matumizi ya shilingi bilioni 1 kwa kila Mkoa kama njia mojawapo ya kuwawezesha wenye vipato vya chini. Hata hivyo tathmini na uzoefu wa muda mfupi umeonyesha yafuatayo:-

Masharti ya Benki - *NMB* na hususan *CRDB* ni magumu kutimizwa na walengwa wengi wanaolengwa hivyo kuashiria tatizo la upatikanaji usio sawa kwa maeneo nchini.

Uamuzi wa Serikali ulikuwa na malengo matatu – kwanza wajibu wa kisiasa, pili wajibu wa kijamii na tatu wajibu wa kiuchumi. Kwa upande mwingine utoaji wa fedha hizo kupitia mabenki yana wajibu mmoja tu – ule wa kufanya kazi kwa faida na hasara ndogo. Matokeo yake mabenki haya yataendelea kutoa mikopo bila ya kuzingatia uwiano wa ki-mikoa (maeneo) na walengwa. Hii italeta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kwa Serikali hasa katika ngazi za vijijini ambako wanachelewa kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuna umuhimu kwamba zana yenyewe ya uwezeshaji utaratibu na malengo uendelee kuelimishwa kwa Watanzania wote ni lazima iwe wazi kwamba pesa hizi siyo sadaka, zinatarajiwa zifanyiwe kazi, zizae faida na halafu zirejeshwe ili ziweze kuzunguka na kuwanufaisha Watanzania wengine ambao hawakufikiwa na mgao wa awamu ya kwanza.

Hivyo Kamati inashauri yafuatayo:- Kwanza, kazi ya kuendesha mikopo iachiwe Mabenki yaliyoteuliwa, lakini kwa kuzingatiwa kuwa kila mkoa unapata kiwango chake cha bilioni moja.

Uongozi wa mkoa ufanye utaratibu wa kuyaagiza Mabenki haya kugawa fedha hizo ki-wilaya kutegemea benki zilizoko huko. Mtandao wa *NMB* ni mkubwa. Zoezi la kulenga *(target)* Walengwa lifanyike na Serikali ya wilaya ili kuhakikisha uwakilishi mzuri, katika wale wanaonufaika na mikopo hii. Kwa kufanya hivi dhana ya uwezeshaji itasambaa nchi nzima kuliko ilivyo hivi sasa. Aidha, utaratibu wa sehemu ya Fedha hizi kutumika kwa ajili ya kuanzisha mabenki ya jamii *(Community Banks)* ili kutoa hamasa kwa nguvu za wananchi wanaochangia kuanzisha benki hizi unatakiwa uzingatiwe. Uanzishwaji wa Benki za Jamii ndio njia ya uhakika na endelevu ya kuwalenga wale wananchi wenye vipato vya chini katika muda ujao. Ni muhimu kufanya tafiti ya mafanikio ya benki hizi za jamii katika nchi za wenzetu ambazo zimeanzisha utaratibu kama huu na tuone namna itakavyoweza kutumika hapa kwetu. Ili kuepuka kujenga Taifa la Wachuuzi fedha hizi lazima zigawanywe katika miradi ya uzalishaji, uzalishaji wa kilimo na miradi mingine ya uzalishaji kama vikundi vya viwanda vidogo vidogo.

Mwisho, elimu ya ujasiriamali itolewe kabla ya kuwapatia mikopo ili kuwawezesha kuwa na matumizi ya ufanisi katika mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuratibu Mashirika yaliyobinafsishwa na kusimamia Ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia. Katika Mwaka 2006 jumla ya mashirika kumi (10) yalibinafsishwa katika ngazi ya makubaliano ya awali, mali zisizo za makampuni *(non core assets)* 22 ziliuzwa, jumla ya mashirika 12 yalibinafsishwa katika ngazi ya Mkataba wa Mauzo *(Final Sales Agreement)*, Kampuni ya Ndege ya *ATCL* ilirudishwa katika miliki ya Serikali na hadi kufikia tarehe 31 Machi 2007 jumla ya mashirika ya umma 336 na mali za mashirika hayo yalikuwa yamebinafsishwa tangu zoezi la ubinafishaji lianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haina kipingamizi na mchakato wa Serikali wa kubinafsisha Mashirika na Makampuni, lakini Kamati inatahadharisha kuwa ubinafsishaji wa Mashirika yaliyosalia ya *TRC, TANESCO* na *NIC* unahitaji uangalifu na umakini mkubwa.

Mashirika haya yanagusa maisha ya watu moja kwa moja na yanagusa uhai wa uchumi wa Taifa letu. Shirika lolote kati ya haya haliwezi kufa peke yake, likifa na sekta nyingine nazo zitakufa pamoja nalo; umeme unagusa viwanda, maji yanagusa viwanda, na kadhalika. Hivyo basi Kamati inaishauri Serikali ichukue tahadhari zote muhimu wakati wa kubinafsisha Mashirika haya.

Mfano wakati Bunge linaridhia sheria ya kuruhusu ushindani wa mashirika binafsi ya bima na sheria iliyoanzisha Shirika la Bima la Taifa haikuweka kipengele katika Sheria hizo ya kuyataka mashirika ya umma kama vile Benki Kuu, *TANESCO, PPF, ATC*, n.k kuendelea kukata bima zao katika Shirika hili la umma katika kipindi cha mpito kama ilivyofanywa na nchi nyingine wakati wa utekelezaji wa zoezi kama hili. Hali hiyo ilichangia kudhoofisha uwezo wa Shirika hili la Umma na wakati huo kusaidia kuimarisha kibiashara mashirika ya binafsi yaliyokuwa yanashindana na *NIC.*

Pamoja na ukweli kwamba hali ya *NIC* katika miaka hiyo ilikuwa ni mbaya sana lakini Kamati imeridhika kwamba shirika hili sasa limekwenda linafanya marekebisho lina hali nzuri kidogo zaidi ya kifedha. Serikali inao uwezo sasa wa kukaa na Mashirika haya ambayo yanatumia fedha za umma yenyewe yakiwa ni mashirika ya umma, kufanya biashara na mashirika binafsi badala ya kukata bima zao au sehemu ya bima zao katika mashirika ya *NIC* pamoja na masuala ya *fair trading, economic labourization* na kadhalika na kuna umuhimu wa kuiongezea biashara *NIC* kwa kufanya hivyo tutaiongezea thamani yake na kuiwezesha kubinafsishwa au kurekebishwa katika mazingira mapya yenye maslahi zaidi kwa Mtanzania.

Katika hilo Kamati imeshauri kwamba Serikali igawe Shirika la *NIC* katika mashirika mawili moja yenye kushughulikia masuala ya Bima ya Maisha katika kufanya hivyo itumie mfano wa *NMB* ambapo asilimia 51 ya hisa ziliuzwa kwa sekta binafsi na asilimia 49 ilibaki katika mikono ya Serikali kwa niaba ya wananchi na hatimaye baadaye hisa hizo kuuzwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Bajeti ya mwaka 2007/2008. Kamati imepokea taarifa kwamba katika kuandaa Bajeti ya Mwaka 2007/2008, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imezingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, kwa kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na Mpango Mkakati wa Wizara 2007/2008 - 2009/2010. Aidha, matayarisho ya Bajeti yamezingatia pia maelezo ya Mwongozo wa utayarishaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2007/2008 – 2009/2010. Kamati imepokea maelezo ya utekelezaji wa Idara za Wizara hii na Ofisi zilizo chini yake kama mfano Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma, Chuo cha Takwimu cha Mashariki ya Afrika, Kituo cha Uwekezaji *TIC.* Tume ya kurekebisha Mashirika ya Umma *PSRC,* Baraza la Taifa la Biashara na Baraza la Taifa la Uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Kamati imeridhika kuwa katika kipindi cha 2007/2008, Wizara:-

Itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuishauri Serikali katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla. Juhudi zitaelekezwa zaidi katika kutekeleza malengo yaliyowekwa katika dira ya taifa ya maendeleo 2025, kupitia mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Mpango wa kuharakisha maendeleo 2020 *Tanzania Min Tiger Plan* na Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005.

Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano kitaendelea kuelimisha wananchi juu ya majukumu na Sera zilizoratibiwa na Wizara.

Kitengo cha Ugavi na Huduma kitaendelea kuboresha mfumo wa manunuzi na utunzaji wa vifaa na huduma nyingine za Wizara.

Kitengo cha Uhasibu kitaendelea kuboresha mfumo wa uwekaji hesabu za Wizara, kuongeza ujuzi wa wafanyakazi, kujibu hoja za ukaguzi na kuziwasilisha kwa wakati, kusimamia malipo kufuatana na sheria na Kanuni za fedha za umma pamoja na kuandaa hesabu za Mwaka wa Fedha 2006/2007 na kuhakikisha zinawasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati.

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kitaendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa Sheria na Kanuni za Fedha na manunuzi ya umma zinafuatwa.

Idara na Sera ya Mipango itafanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Wizara na kuratibu utayarishaji wa Bajeti ya Wizara na Asasi zake, kuratibu maandalizi ya Hotuba ya Waziri wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kuhusu Mpango wa Bajeti katika Fungu 66 pamoja na kuratibu na kuandaa Kongamano la Mwaka la Maafisa Mipango *(Planners Conference).*

Idara ya Uchumi jumla itaendelea kuchambua mwenendo wa vigezo na viashiria vya uchumi jumla, kuratibu maandalizi ya Hali ya Uchumi na Maendeleo ya Kijamii na kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Sera za jumla na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuchambua mwenendo wa viashiria na vigezo katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Idara ya Sekta ya Nje itatathimini na kubaini fursa za kuendeleza biashara ya nje pamoja na kufuatilia maazimio ya taasisi na programu za kimataifa kama *WTO, AGOA, EPA, EBA, Canada's PACT, Japan's TPS, Korea's TPS, China's TPS & FOCAL na TICAD.*

Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu itaendelea na majukumu ya kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu, kuandaa wigo wa kuainisha masuala ya idadi ya watu katika mipango ya maendeleo na kuhusisha mipango ya jinsia katika mipango ya maendeleo ya Taifa.

Idara ya Kuondoa Umaskini itaendelea kuratibu mpango wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa MKUKUTA.

Idara ya Uwezeshaji itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Tija ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

Idara ya Uwekezaji mitaji ya Umma itaratibu uandishi wa Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Bajeti kwa Kipindi cha Mwaka 2008/2009 – 2010 – 2011.

Idara ya Mikakati ya Kukuza Uchumi itaendelea kufanya tathmini na mapitio na mashirika yaliyobinafsishwa na kuratibu maendeleo na uwekezaji wa sekta binafsi.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea na kukusanya na kuchambua takwimu rasmi za kiuchumi na kijamii na kufanya tafiti zilizoainishwa katika mpango kabambe wa kufuatilia hali ya umaskini nchini.

Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi na kuandaa Mitaala ya Shahada za Uzamili katika maendeleo ya Uchumi na Mipango ya mazingiara. Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika kitaendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya takwimu katika kiwango cha Cheti na Diploma kwa lengo la kuboresha ukusanyaji, Uchambuzi na matumizi ya takwimu nchini.

Kituo cha Uwekezaji kitaendelea na kazi ya kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje katika sekta ambazo zitalipatia Taifa nguvu ya ushindani na ambazo zitasaidia katika kuondoa umasikini na kukuza uchumi kwa haraka zaidi.

Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma intarajia kukamilisha kazi iliyobaki ya ubinafsishaji katika muda wake wa miaka minne (4) ya nyongeza ya uhai wake unaoishia tarehe 31 Desemba 2007.

Baraza la Taifa la Biashara litaendelea kupanua na kuimarisha mashauriano kati ya Serikali, Sekta binafsi na wadau wengine nchini katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa, na

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi litaendelea kuwaelimisha na kuwahamisisha wananchi kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji, na kutoa mafunzo kwa Wajasiliamali 200 kwa kila mkoa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Kamati imeridhika kuwa katika Kipindi cha Mwaka 2007/2008 Wizara itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kuishauri Serikali katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla.

Juhudi zitaelekezwa zaidi katika kutekeleza malengo yaliyowekwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Mpango wa Kuharakisha Maendeleo 2020 *(Tanzania Mini-Tiger Plan 2020)* na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo, hapo awali nilikumbushia kauli ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alipotembelea Wizara hii na kuwaambia kwamba wao ndio ubongo wa Serikali.

Ukiuchukulia mfano wa kiwili wili cha mwanadamu kauli hii inatoa umuhimu wa kipekee na dhamana kubwa kwa Wizara hii. Ni lazima wao ndio wawe mstari wa mbele wa kubuni na kutoa mwongozo kwa Idara zingine za Serikali kuhusu mikakati ya kujikwamua kiuchumi kwa makadirio ya muda mfupi na ya muda mrefu. Ni lazima kuwe na mikakati ya ndani ya kuboresha uwezo wa kitaaluma na kiutendaji wa kuiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake kwa namna inayoendana na ari, kasi na malengo ya Awamu ya Nne.

Hatua hizi ni lazima zitujumuishe kuongeza uwezo wa kitaaluma, *capacity building* lakini pia kuongeza tija katika kazi zao, hawana nafasi Wizara hii ya kufanya kazi zao kwa mfumo wa *business as usual* katika awamu hii.

Taarifa zao na miongozo yao ni lazima iwe na ushahidi wa kufanyiwa utafiti wa kina, tathmini za uhakika ambazo ni kioo, *reflaction* ya mahitaji na mazingira ya kiuchumi, kijamii na kisiasa ya Tanzania ya leo. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuwa Mpango wa Kupunguza Umaskini upewe umuhimu mkubwa; hususani katika yale maeneo ambayo yanatoa fursa hizo.

Baadhi ya programu HUSIKA ambazo zinazoelekezwa kwenye Halmashauri *(TASAF, PADEP, ADSP)* n.k. isimamiwe vizuri. Ni maoni Kamati ya kwamba nadharia mzima na tafsiri ya kiuchumi ya *decentralization by devolution D by D* ambayo ndiyo msingi wa mkakati wa kuhamisha majukumu ya Serikali Kuu kwenda kwenye Serikali za Wilaya, lazima ielimishwe bila kuchoka kwa Watendaji wahusika ili kuboresha uwajibikaji na utendaji. Hili ni jukumu kubwa muhimu la Wizara hii. *(Makofi)*

Kamati imebaini kuwa kasi ya utekelezaji wa Programu ya MKURABITA imechelewa kutoa matokeo yaliyokusudiwa. Aidha, utaratibu wa utekelezaji wa majaribio *(Pilot Project)* ya Programu hii katika mikoa ya Dar-es-Salaam na Mbeya hautaweza kutoa picha halisi katika mikoa mingine.

Hivyo Kamati inapendekeza wigo huu upanuliwe katika mikoa mingine ili matokeo yake yaweze kutekelezeka kwa Watanzania walio wengi zaidi. Kamati inaamini kuwa urasimishaji wa mali za Watanzania wa kipato cha chini ni njia mojawapo ya kuwezesha Watanzania hao kukopesheka katika Taasisi za Fedha.

Ubinafsishaji wa *NIC* na *TRC* ufanywe kwa makini hasa ikizingatiwa kuwa vyombo hivi vinahudumia wadau wengi, pamoja na wafanyakazi, na vina umuhimu wa kipekee kwa uchumi na maendeleo ya wananchi wa Tanzania. Dhama ya kuendeleza na kukarabati miundombinu ya Reli ni ya kipaumbele na ni lazima isimamiwe japokuwa kuna ushirikiano kati ya Serikali na Mwekezaji.

Kwa upande wa *NIC,* ubinafsishaji wa huduma utofautishwe na majengo. Aidha, hatua za haraka zichukuliwe kukamilisha mchakato wa ubinafsishaji wa *NIC,* la sivyo, wateja watapoteza imani *(confidence)* juu ya uwezo wa *NIC* na hivyo kupoteza biashara na kupungua thamani.

Kamati hii ambayo pia inaisimamia *PSRC* imeridhika na taarifa kwamba utekelezaji wa mikakati ya maendeleo na uwekezaji katika mikakati hii ya ubinafsishaji wa *TRC* na *NIC* inaendelea vizuri lakini tunahimiza kwamba lazima pawe na makubaliano ya kuondoka katika mikataba hii kama tunaona kwamba utekelezaji wake hauna maslahi kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Katika eneo la Uwezeshaji wa Wananchi wenye vipato vya chini, kupata mitaji kupitia mabenki, *SACCOS* na taratibu nyingine ni vyema sasa taasisi hizi zipunguze gharama za uendeshaji/utawala, ili walengwa wazingatie kupunguza uwezekano wa hasara inayotokana na matumizi mabaya ya mikopo na hatimaye kushindwa kuilipa mikopo hiyo. Aidha, elimu ya ujasiriamali itolewe sanjari na kuhamasisha wananchi hususani wa vijijini, kuchukua mikopo na kuilipa.

Kamati inashauri Serikali kufanya tathimini ya mara kwa mara ili kubaini uwezo wa rasilimali zetu katika kuchangia na kukuza pato la Taifa. Katika rasilimali hizo ni pamoja na mkaa wa mawe *(Mchuchuma)*; Chuma cha Liganga, Gesi na uimarishaji wa bandari za Tanga, Mtwara na pia bandari ya ndani ya Kigoma kama kituo cha biashara cha kimataifa na nchi za jirani. Aidha Kamati inahimiza uzalishaji wa bidhaa zisizo za asilia, kama vile asali na viungo Mashamba ya Mpira ya Mheza, Zanzibar na Kilombero yafufuliwe sanjari na Kilimo cha michikichi Kigoma yanaweza kuleta mapato makubwa kwa wananchi.

Kamati imebaini kuwa upo ufinyu wa fedha zinazopelekwa kuendesha vyuo vilivyo chini ya Wizara hususani Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma. Kamati ilifanya ziara katika Chuo hiki na kubaini kuwa Chuo hiki hakina hosteli kwa ajili ya wanafunzi wake. Aidha, Mkuu wa Chuo tumebaini amekuwa akikaimu kwa muda mrefu sasa. Tunaomba tutambue nafasi ya chuo hiki kwa utekelezaji wa mikakati ya kiuchumi na ya kijamii kwamba ni mkubwa mno na muhimu pia uwezekano uangaliwe wa kulifanya chuo hiki kuwa ni sehemu ya Kitivo cha Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kamati inaishauri Wizara kuwa na utaratibu wa kuboresha tafiti na tathmini za kiuchumi za sekta zote (Kilimo, Maji, Afya, Miundombinu, na kadhalika na mchango wake jumla wa Taifakwa namna ambayo Wizara kama kiungo cha kuratibu masuala yote ya Uchumi kina uwezo wa kutambua mabadiliko yasiyotegemewa *an expected shocks* ya Uchumi (km *inflation,* matatizo ya *exports and imports)* bei za mafuta na kadhalika na kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na hali hiyo ili athari zake zisiwe za kina na pana kwa uchumi na wananchi *(Economy Trends Tracking Unit (ETTU)* Kamati inaishauri Wizara kuwa na Kitengo kwa ajili ya kazi hii kama ilivyo Wizara kama hii katika nchi zingine ambazo inaweza ikajulikana kama *economy trends tracking unit.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, ili kufanikisha utekelezaji wa kazi za Wizara na Asasi zilizo chini yake, Mheshimiwa Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji analiomba Bunge lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 78,33,654,000/= kwa mchanganuo ufuatao:- Matumizi ya Kawaida - Sh. 21,441,654/=;

Miradi ya Maendeleo - Sh. 53,709,000,000/=; Jumla ya mahitaji yote – Sh.75,150,654,000/=. Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichukue fursa hii niwapongeze kwa dhati kabisa wajumbe wote wa Kamati yetu kwa michango, maoni na kwa kufanya kazi nzuri sana kutekeleza kazi zote za Kamati bila kuchoka.

Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina mbele ya Bunge lako Tukufu kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Dk. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmoukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mheshimiwa Elisa D. Mollel, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuiberi,

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda nikushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kutupatia miongozo mbalimbali ndani ya Bunge letu. Aidha, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Makatibu wa Kamati yetu, Ndugu Anselm L. Mrema na Hellen S. Mbeba kwa kuipa Kamati uwezo na nyenzo zote muhimu katika kufanikisha kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii ya kuwa hapa kwa unyenyekevu na heshima kubwa niwashukuru wananchi wote wa Mkuranga, DC wangu, Bwana Henry Clemence, Halmashauri yangu pamoja na madiwani wa wilaya yetu, kwa mapenzi yao na utekelezaji wao wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Naomba niishukuru familia yangu, mke wangu Aziza na watoto wetu Ali, Abdallh, Amina, Ayubu, Mariam, Amin, naam! kwa mapenzi yao kwangu. Naomba niwashukuru wazazi wangu, mama yangu mzazi, Mungu ampe umri na naomba nitumie fursa hii kumwombea makazi mema peponi. Marehemu baba yangu, Prof. Kigoma Ali Malima, chochote mnachoona hapa nikijitanunua basi sina ujanja isipokuwa kudra ya Mwenyezi Mungu na malezi na uangalizi wa karibu sana wa marehemu baba yangu, wakati wote wa uhai wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lisingekuwa na heshima hii kubwa kama isingekuwa mchango wa viongozi waandamizi humu ndani. Wengi wao ni wazazi wangu wa karibu wa hiari wa miaka mingi, wamenipokea wanilea wameniongoza na kunipatia ushauri nasaa. Mzee KingungeNgombale-Mwiru, Mzee Athumani Janguo, Mzee Mshangama, Mzee William Shellukindo, Mama yangu Mama Anna Abdallah, Mama Zakia Megji, Mama Tatu, Mama Fatuma, Mzee Cheyo unayenyoosha mkono na wewe

Mzee wangu Gideon Cheyo, Mzee Ndesamburo pia na wazee wenzangu wengine, Mzee Mwapachu. Bunge hili ni tajiri kwa sababu ya hazina ya uzoefu mnaokuja nao nyinyi humu ndani ambao ndiyo ngome yetu sisi Wabunge wageni vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kumshukuru mno kaka yangu Waziri Mkuu Edward Lowassa, sina la kusema, namshukuru kwa kila hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru Wabunge wenzangu wote, napenda kutamka kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (Makofi)

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, leo umetoa kali lakini ulikuwa unafanana na baba yako kabisa.

**MHESHIMIWA KABWE ZUBERI ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka salama na kwa mara nyingine tena kuniwezesha kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 45(3)(b)(c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kutoa salamu za pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa Hayati Chifu Abdallah Fundikira aliyetutoka hivi karibuni. Tanzania itamkumbuka kama mmoja wa magwiji wa siasa za Taifa hili. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi – Amin!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee kabisa naendelea kuwashukuru wananchi wa jimbo la Kigoma Kaskazini kwa kunikubali kuwa mtumishi na mwakilishi wao. Naahidi kuendelea kutekeleza majukumu yao waliyonipa kwa umahiri, uadilifu, na umakini mkubwa, na kwa wale wananchi Jimbo la Kigoma Kaskazini hasa hasa kutoka kwenye Kata za Mkigo na Mwandiga ambao juzi juzi hapa walikuwa na wasiwasi na suala la biashara ya udongo wa Pemba. Napenda kuwaarifu kwamba biashara hiyo haijapigwa marufuku, isipokuwa tu Waziri alishauri wananchi wasitumie udongo huo. Kwa hiyo, waendelee na biashara hiyo kwa sababu ni sehemu ya msingi sana ya kipato chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Ania Chaurembo, kwa ushirikiano mzuri anaonipa katika kutetea maslahi ya Watanzania ndani na nje ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kwa Bunge hili la bajeti, ofisi ya Kambi ya Upinzani imekuwa ikifanya kazi na vijana kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaopata uzoefu kabla ya kazi rasmi (*Practical Training and Internship Programme*). Kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kuwapongeza na kuwashukuru vijana hawa kwa

kazi nzuri waliyowafanyia Watanzania hadi sasa kupitia ofisi yetu chini ya uratibu mzuri wa bwana Oliver Mwikila. Vijana hawa ni ndugu, Khamis S. Ali, Jackline Mkotani, Tumaini Shalli, Afua Shabani, Demani Yusuph na Ndugu Edward E. Kinabo. Nasema ahsanteni sana, nawahakikishia kuwa mchango mlioutoa hautapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mipango na Uchumi, Uwezeshaji, inashughulikia pamoja na mambo mengine maswala ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma, uwekezaji na uratibu wa sera za uchumi. Wizara hii hufanya kazi zake mbalimbali zilizo chini ya idara,vitengo na taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubinafsishaji, tunatambua ya kuwa lengo kubwa la kubinafsisha mashirika ya umma katika programu inayoendeshwa na *The Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC)* iliyoanzishwa chini ya the *Public Corporations Act,* ya mwaka1992 iliyorekebishwa mwaka 1993 na 1999, ilikuwa ni kuleta ufanisi zaidi katika uzalishaji wa makampuni hayo yaliyobinafsishwa. Hata hivyo, ubinafsishwaji wa Shirika lolote la umma unapaswa kufanywa pale panapokuwa na sababu za msingi za kufanya hivyo. Moja ya mashirika ambayo yamebakia kubinafsishwa chini ya *PSRC* ni Shirika la Bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tarehe 8 Agosti, 2007 katika kikao cha Kamati ya Fedha na Uchumi, Bunge lako Tukufu liliweka historia. Historia ambayo nimeona ni vyema niiweke katika hotuba yangu ili iwe ni kumbukumbu nzuri ya utendaji wa Bunge lako Tukufu.
Historia hii inahusiana na suala la ubinafsishaji wa Shirika la Bima la Taifa. Suala hili lilichukua muda mrefu sana na hivyo kuondoa "*Confidence*" ya biashara ya Bima. Historia hii ni ya kuonesha jinsi ambavyo Bunge kupitia kamati zake zinaweza kulifanyia kazi jambo mahususi lenye maslahi kwa Taifa na kufikia mwafaka.

Mheshimwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, *PSRC*, Menejimenti ya *NIC* na wafanyakazi jana wamefikia muafaka kuhusu ubinafsishaji wa Shirika la Bima na kuamua kuahirisha mchakato unaoendelea wa kubinafsisha *NIC* na kuchukua hatua za kurekebisha Shirika hili. Mwafaka huu bado unafanyiwa kazi upande wa Serikali. Pamoja na mambo mengine Shirika la Bima litarekebishwa kwa njia ya kuwaachisha wafanyakazi wote na kuwalipa haki zao, kubadilisha Bodi na Uongozi wa *NIC* na kufanya taratibu za ajira upya ili kuweza kuendesha biashara hii ya Bima. Vilevile shirika kama jinsi ambavyo Kamati ya Fedha imependekeza litaongezewa mtaji wa uendeshaji kwa njia za kuuza baadhi ya mali zake au kwa njia nyingine yoyote itakayofaa ili kuliwezesha kulipa madeni na kujiendesha kiufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inakubaliana na mapendekezo yaliyopo ya kulibinafsisha Shirika hili kwa utaratibu uliotumika kuibinafsisha benki ya *NMB* na kurekebisha Shirika la Umeme yaani *TANESCO*. Uamuzi huu ni wa maslahi ya Taifa na umeonyesha uimara wa Bunge lako Tukufu. Nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Mheshimiwa Abdallah Kigoda na wajumbe wote wa Kamati kwa kazi

nzuri sana yenye mafanikio makubwa. Kazi hii imeonyesha kuwa Bunge hili lina meno, na tukiamua tunaweza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira Kutokana na Ubinafsishaji, moja ya sababu kubwa iliyokuwa inatolewa na Serikali kuhusu kubinafsisha mashirika ya umma ilikuwa ni kuongeza ajira na kuongeza pato la nchi. Kambi ya Upinzani tunaitaka serikali itoe takwimu za sasa za idadi ya mashirika yaliyobinafsishwa na idadi ya ajira zilizotengenezwa kutokana na ubinafsishwaji huo. Tunahitaji takwimu hizi ili kupima mafanikio ya utekelezwaji wa sera ya ubinafsishaji katika kuongeza ajira maana tuna mashaka kuwa idadi ya mashirika yaliyobinafsishwa ni kubwa kulinganisha na ajira zinazotokana na ubinafsishaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa mashaka yetu pengine unaweza kuthibitishwa kwa mlinganisho wa takwimu haba tulizonazo kama ifuatavyo: Kwa mujibu wa takwimu za Kituo cha Taifa cha Uwekezaji *(TIC*) za mwaka 2002, mashirika 265 yalikuwa yamebinafsishwa, mpaka mwaka 2002 kati ya hayo 135 yalinunuliwa na wazawa kwa asilimia 100. Mashirika 15 yalinunuliwa na wawekezaji wa nje kwa asilimia 100, na mashirika 115 yalinunuliwa kwa njia ya ubia. Na katika hotuba iliyotolewa mwaka jana na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, jedwali namba 2, linaonyesha kuwa hadi kufikia mwaka 2005 ajira kutoka katika sekta hii zilikuwa ni 88,713 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo tutatafuta wastani wa jumla ya ajira 88,713 kwa kutumia idadi ya mashirika 265 yaliyokuwa yamebinafsishwa hadi mwaka 2002, tutabaini kuwa kwa wastani shirika moja lililobinafsishwa limetengeneza ajira za watu 335. Wastani huu hata hivyo hauna usahihi wa kutosha kwani jumla ya ajira 88,713 sio za mashirika yaliyobinafsishwa tu bali pia inahusisha mashirika ambayo hayakuwa yamebinafsishwa. Vilevile ni wazi kuwa mashirika yaliyobinafsishwa si yale 265 ya mwaka 2002 bali ni zaidi ya hapo. Kwa mantiki hiyo basi wastani wa ajira kwa shirika moja lililobinafsishwa utakuwa ni chini zaidi ya ajira 335 kwa shirika. Ni kwa minajili hii basi tunahitaji takwimu halisi za sasa za mlinganisho wa idadi ya mashirika yaliyobinafsishwa na ajira zilizotengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji uweze kuwa wenye mafanikio na kutengeneza ajira za kutosha, Kambi ya Upinzani, tunaishauri Serikali kuzingatia yafuatayo: Ubinafsishaji wa mashirika ya umma yaliyobakia utoe kipaumbele kwa wazawa ambao wako tayari na wenye uwezo wa kuendesha mashirika haya.

Pale ambapo tatizo ni udhaifu wa menejimenti kiutendaji ama kiubadhirifu, ufumbuzi uwe ni kuwawajibisha wabadhirifu na kuajiri watendaji wapya wa ndani badala ya kuchukua menejimenti za kigeni kutuendeshea mashirika yetu. Penye ubia na wageni ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa Watanzania wanafaidika na ubia huo kwa kiasi cha kutosha. Kwa hili tunasisitiza haja ya Serikali kuendelea kupitia mikataba kati yake na kampuni mbalimbali za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine kubwa tunalolipata katika ubinafsishaji ni suala zima la kulinda wawekezaji na viwanda vya ndani. Moja ya eneo tulilofanya ubinafsishaji mkubwa ni katika sekta ya Mkonge na mazao yake. Tumebinafsisha viwanda vyetu viwili vya kuzalisha magunia yanayotokana na kamba za katani, kiwanda cha Morogoro na kile cha Moshi. Mpaka sasa ni kiwanda cha Morogoro tu ndio kinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inao uwezo wa kuzalisha tani 16 milioni za magunia ya katani kutoka katika viwanda hivi viwili kama vikifanya kazi kwa kiwango chake. Hata hivyo, biashara hii ya magunia imevamiwa na magunia yanayoagizwa kutoka nje na yanayotumia Jute. Huko nyuma Mheshimiwa Mbunge Estherina Julio Kilasi (Mbarali) alijenga hoja ya kupandisha kodi ya forodha ya magunia yanayotokana na *Jute* ili kulinda sekta ya Mkonge. Ni kweli kuwa Serikali imeweka "*suspended duty*" ya 50%. Hata hivyo, hii haitoshi. Ni vema tuchukue maamuzi mahususi ili si kulinda wawekezaji katika eneo hili bali pia kulinda zao la Mkonge. Magunia ya Mkonge ni imara zaidi, yanaweza kutumika zaidi ya mara moja na yanazuia unyevunyevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi siku ya Jumatatu 6 Agosti, 2007 Bunge la India limefanya marekebisho makubwa katika sheria yake inayoitwa *Jute Packing Materials (Compulsory Use in Packing Commodities) Act* 1987 ili kuipa nguvu zaidi na kulinda zao la Jute. Huko India ni marufuku kutumia magunia ya aina nyingine yoyote tofauti na *Jute* kwa bidhaa muhimu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, umefikia wakati sasa, na tayari nimetoa wazo hili kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na kukubaliana na msingi wa hoja (*principle*) kufanya marekebisho ya sheria zetu ili kulazimisha matumizi ya magunia ya katani kwa kuhifadhi bidhaa kama Kahawa, Korosho, Mahindi na kadhalika. Ninaamini kabisa kuwa Serikali itaweza kuliangalia suala hili kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie katika eneo hili la ubinafsishaji kwa kujadili suala la muda wa *PSRC*. Kama sote tunavyofahamu Tume ya Rais ya kurekebisha mashirika ya umma inamaliza muda wake mwaka huu mwezi wa Disemba kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, bado kuna masuala kadhaa yanayohusu maslahi ya nchi, yanatakiwa kuangaliwa ili kujua kama ni vema kumalizia muda huu wa PSRC au kuwa na chombo maalumu kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa majukumu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu kuwa *PSRC* imekuwa na matatizo makubwa sana na wananchi wengi wamekuwa wakiilaumu kwa kubinafisha mashirika yetu kiholela. Mali nyingi za nchi zimepotea kwa ubinafsishaji usio na utaratibu na hata kupelekea taifa kupata hasara kwa mfano katika mashirika kama *ATCL* na *TTCL*. Vilevile viwanda vingi vilivyobinafsishwa vimekuwa ni maghala tu na uzalishaji umesimama.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kufuatia mkopo kutoka Benki ya Dunia, kuna jumla Sh. 45 bilioni *(IDA* 3304-*TA*) ambazo zinasubiri uhakika wa *PSRC*. Fedha hizi kwa mujibu wa barua kutoka serikalini kwenda kwa Mkurugenzi mkazi wa Benki ya Dunia ya

tarehe 20/4/2007, zitatumika kuwezesha mashirika kama *TCRA*, *TCAA, SUMATRA* na mashirika mengine ya usimamizi (*regulatory institutions*).

Kesho tunajadili mabadiliko ya sheria ya *EWURA* ili kuipa meno kudhibiti biashara ya mafuta. *EWURA* itashindwa kufanya kazi sawa sawa iwapo tutakosa fedha hizi kutoka Benki ya Dunia. Katika hili napenda Serikali itueleze ni masharti yepi ambayo Benki ya Dunia imetupa kutokana na Mkopo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa haraka ni lazima uchukuliwe ili Taifa lisipoteze fedha hizi na kuua maana halisi ya kuwa na hizi Regulatory Authorities. Kosa tulilolifanya katika LART na kujikuta tumepoteza mali za takribani 18 Bilioni tusilifanye tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala kadhaa yamebakia katika zoezi la ubinafsishaji. Masuala haya yanahitaji chombo kwa ajili ya kuratibu. Miongoni mwa masuala hayo ni pamoja na: Kumalizia kazi zilizobaki za ubinafsishaji wa mashirika 33 yaliyobakia; Kusimamia utekelezaji wa mikataba ya mauzo ya mashirika yaliyobinafsishwa; Kushughulikia utetezi wa kesi zaidi ya 150 dhidi ya Serikali kuhusiana na mashirika yaliyobinafsishwa; kufuatilia hati za umiliki wa viwanja na majengo zaidi ya 70 ya mashirika yaliyobinafsishwa na yanayobinafsishwa; kufuatilia/kushughulikia madai ya kibiashara dhidi ya mashirika ya umma; kujenga misingi imara ya kufuatilia (*manuals and procedures)* na kutathmini utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa; kuandaa muundo na sheria za *Public Partnership* kwa ajili ya miradi mipya na ya zamani ambayo sekta binafsi na serikali zinaweza kushirikiana

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani mwaka jana katika Bunge hili tulishauri Kituo cha Uwekezaji cha Taifa (*TIC*) kiweke mazingira bora ya uwekezaji katika mikoa iliyo pembezoni (*marginalised regions*) ili nayo pia ifaidike na Juhudi za *TIC*. Kadhalika, tulitaka kasi ya kufungua vituo vya uwekezaji vya Kanda iongezeke ili kutoa huduma bora za uwekezaji nchini.

Kwa taarifa tulizonazo sasa ni kuwa Kituo hiki kipo katika hatua za mwisho za kufungua ofisi kanda ya kusini mkoani Mbeya. Ofisi hiyo itakuwa ni ya tatu kufunguliwa kikanda baada ya Mwanza na Kilimanjaro na itatoa huduma mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, na Ruvuma. Tunapongeza juhudi zinazofanywa na Kituo hiki katika kusogeza huduma za Kituo karibu na wananchi. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kila kanda nchini inakuwa na ofisi ya Kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kuvutia wawekezaji ni kazi kubwa na nyeti mno. Sisi kama Taifa bado hatujaweka mikakati mahususi ya kuvutia uwekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani. Katika nchi yetu uwekezaji umekuwa ukifanyika zaidi katika sekta ya migodi ya madini na kiasi kwenye mashirika. Bado katika sekta nyingine za uchumi mathalani kilimo na ufugaji uwekezaji haujafanywa kikamilifu licha ya sekta hizi kuwa ndio mhimili mkuu wa uchumi wetu, bado hatujakuwa na mikakati bora ya kuvutia wawekezaji. Kwa mfano, bado Balozi zetu katika mataifa mbalimbali hazijapelekewa

wafanyakazi wataalamu wa masuala ya uwekezaji. Umefika wakati sasa kuanza kutekeleza sera ya Diplomasia ya kiuchumi kwa umakini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa liko mbioni kumpata tena mrembo mpya yaani "*Miss Tanzania*" atakayewakilisha nchi hii kwenye mashindano ya urembo ya Dunia. Kama ambavyo imekuwa ikisemwa na wadau wa mashindano haya, moja ya faida kubwa zitokanazo na mashindano haya ni mrembo wa nchi husika kuwa na fursa ya kuitangaza nchi yake kwa mataifa mengine kiuchumi, kidiplomasia na kiutamaduni. Kwa Tanzania, licha ya kutoa warembo kadhaa, bado fursa haijatumika ipasavyo. Kwa kuwa moja ya jukumu la Kituo cha Uwekezaji ni kuitangaza nchi kiuchumi ili kuvutia wawekezaji wa kutosha basi Kambi ya Upinzani inashauri Kituo hiki kuingia makubaliano na Kamati ya *Miss* Tanzania ili kutumia kikamilifu warembo wetu katika kuvutia wawekezaji. Utaratibu tunaoupendekeza ni kwa Kituo hiki kutoa hadidu rejea (*Terms of reference)* kwa warembo ili ziwaongoze vyema katika kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini badala ya kuachwa tu wajisemee kwa utashi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, ili kuboresha uwekezaji nchini, Kambi ya Upinzani inaendelea kusisitiza ushauri wake ilioutoa mwaka jana kama ifuatavyo: Kuweka maafisa wa masuala ya biashara na uwekezaji katika Balozi zetu zote zenye fursa ya wawekezaji wa kutosha. Maafisa wapate mafunzo maalumu ya utangazaji wa fursa za uwekezaji zilizopo nchini na vilevile kutoa taarifa nchini juu ya fursa za biashara zilizoko huko.

Kwa nchi kubwa kama Marekani, Uingereza, China, India na Ujerumani, Serikali iangalie uwezekano wa kufungua vituo vya biashara na uwekezaji katika mikoa muhimu ya nchi hizo na baadae pia vituo hivyo kufanya kazi kama *consulates* zetu. Mfano dhahiri ni umuhimu wa kufungua Kituo cha Biashara na Uwekezaji katika Jimbo la *California* nchini Marekani na *Munich* nchini Ujerumani ili kuweza kuitangaza nchi kwa wepesi zaidi.Tufungue vituo vya Biashara katika nchi ambazo ni wawekezaji wazuri kwetu kama Uholanzi, haraka iwezekanavyo ili kuweza kushindana vizuri katika kutafuta wawekezaji. Bajeti ya *TIC* iongezwe ili imudu majukumu yake mbalimbali hususan utekelezwaji wa mikakati ya kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007/2008, Kituo Cha Uwekezaji kinakusudia kutathimini mafanikio ya juhudi za kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje nchini kwa kubaini matokeo halisi ya uandikishaji na utekelezaji halisi kwa lengo la kubaini matatizo na vikwazo vinavyowakabili wawekezaji kwa nia ya kuwapatia ufumbuzi. Hili ni jambo jema lakini mkazo zaidi pia uwekwe katika kubaini matatizo wanayopata Watanzania ambao ni waajiriwa katika sekta ya uwekezaji. Tunasisitiza hili kwa sababu kumekuwepo malalamiko mengi ya wananchi kuhusu unyanyasaji unaofanywa na baadhi ya wawekezaji kwa wananchi walioajiriwa katika maeneo mbalimbali. Aidha, tathmini hiyo ilenge kubaini faida na hasara ambazo taifa limepata hadi sasa kutokana na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria ya Kituo cha Uwekezaji vitega uchumi (*The Tanzania Investment Act, 1997, Act No*. 26), sehemu ya 7, Waziri muhusika na masuala ya ubinafsishaji amepewa mamlaka ya kuteua wajumbe wa Bodi ya *TIC*. Hata

hivyo, sheria imetoa masharti mahususi kwa wateuliwa wa bodi wakiwemo watu wenye ujuzi na uzoefu wa kutosha katika shughuli za Uma na sekta Binafsi na masuala ya uongozi. Vilevile sheria inataka wajumbe wa Bodi ya *TIC* wawe nusu kwa nusu kati ya wajumbe wanaotokana na sekta ya Uma na wale wanaotokana na sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uteuzi wa hivi karibuni wa wajumbe wa Bodi ya *TIC*, Waziri amefanya uteuzi unaotia mashaka kinyume na umuhimu wa majukumu ya *TIC*. Kwa mfano, kwa nini Waziri amemtoa katika Bodi ya *TIC* Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi ilihali tukijua kabisa kuwa suala la Ardhi ni suala nyeti sana katika masuala ya Uwekezaji vitega uchumi. Vilevile, Waziri ametumia vigezo gani, kwa mfano, kumteua aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Morogoro katika Bodi ya *TIC* ilhali akijua kabisa kuwa uwezo wa mtu huyu katika masuala ya Uwekezaji unatia mashaka? Pia Waziri anasemaje kuhusu uamuzi wake wa kumteua aliyekuwa mfanyakazi wa *TIC* (wakati huo *IPC*) na kufukuzwa kazi, kuwa mjumbe wa Bodi ya *TIC*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuwa Mawaziri wana mamlaka ya kisheria ya kufanya uteuzi katika Bodi mbalimbali. Hata hivyo, mamlaka haya yasipoangaliwa kwa makini tutajikuta tunafanya teuzi ambazo hazina maslahi ya Taifa bali maslahi binafsi, kiitikadi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ina idara nyeti sana inayoitwa Idara ya Sekta ya Nje. Idara hii inaombewa kibali cha kutumia jumla ya shilingi milioni 830 tu. Moja ya kazi ya Idara hii pamoja na mengine, ni kushughulikia tathmini na kubaini fusra za kuendeleza biashara ya nje kwa nchi yetu. Fedha zinazoelekezwa kwa idara hii ni kidogo mno kulingana na majukumu yake muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara tumekuwa tukielezea tatizo kubwa la nchi yetu kutofanya vizuri katika mauzo ya nje. Mauzo yetu ya nje yamekuwa yakitegemea sana madini na hasa dhahabu kama tulivyoonesha katika hotuba yetu ya Hali ya Uchumi nchini. Idara hii inapaswa kuongezewa nguvu zaidi ili kuimarisha mikakati yetu ya kisera katika sekta ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara hii pia ndio yenye jukumu la kushughulikia suala zima la uratibu wa ushiriki wetu katika mijadala mbalimbali ya kimataifa. Hivi karibuni kumetokea mjadala mkali sana ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusiana na majadiliano yanayoendelea kuhusu Makubaliano ya Ubia wa Kiuchumi kati ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya. Kwa faida ya Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla, ni vema suala hili lijadiliwe zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa faida ya Bunge lako Tukufu na kwa manufaa ya Watanzania tunaowatumikia, leo tunarejesha tena mjadala juu ya suala la *Economic Partnership Agreement (EPA)* linaloonekana kutoeleweka vyema. Economic Partnership Agreement *(EPA)* ama kwa Kiswahili "Makubaliano ya Ubia wa Kiuchumi (MUK)" ni mshikamano kati ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki kwa upande mmoja na nchi za Jumuiya ya Ulaya kwa upande mwingine, uliosainiwa jijini *Cotonou* nchini *Benin* mwezi Juni, 2000 na unaotoa fursa kwa nchi tajwa kuwa na taratibu zinazowiana kibiashara,

kuondoa mipaka ya kibiashara kati yao na kuchochea ushirikiano katika maeneo yote yanayohusika na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya faida kubwa zinazotarajiwa kutokana na *EPA* kwa nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki ni pamoja na kuimarika kwa utengamano wa kikanda (*regional integration*), maboresho katika sera na fursa za kibiashara na kuongezeka kwa mwingiliano wa vitegauchumi ndani ya nchi hizi na nchi za Umoja wa Ulaya. Hata hivyo, mpango huu wa biashara huria na nchi za ulaya utasababisha pia changamoto za kisera, kiutawala na kitaasisi kwa nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki ikiwa ni pamoja na: kupoteza mapato ya kodi kutokana na kuondoa ushuru; kuepuka athari za mabadiliko makubwa katika mwelekeo wa biashara na changamoto ya udhibiti mzuri wa sekta ya huduma huria pamoja na kuweka biashara huria ndani ya nchi za Afrika, Karibeani na Pasifiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tutakuwa tunapeleka bidhaa zetu Ulaya bila kulipa kodi nao wataingiza za kwao bila kulipa kodi kuanzia Januari, 2008, ni lazima jambo hili tuliangalie kwa umakini kwa sababu tafiti zote zinaonyesha kwamba tutapoteza asilimia 30 ya mapato yanayotokana na Ushuru wa Forodha kutokana na kuingia kwenye *EPA*. Hata hivyo, wataalamu wanasema kuwa athari hii ni ya muda mfupi, baadaye nchi inaweza kufaidika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hatua zilizofikiwa kuhusiana na *EPA* ni muhimu kwa nchi yetu kuingia *EPA*. Suala ni jinsi gani nchi inaingia katika umoja huo, maana tukiingia kichwa kichwa hatutanufaika kama tunavyotarajia bali tutakuwa ngazi ya mafanikio ya nchi nyingine. Zipo njia kuu mbili za nchi kujiunga na *EPA*, moja ni nchi kupitia kwenye kikundi hususan tengamano za kikanda *(regional integrations)* kama *COMESA, SADC, EAC* na kadhalika. Njia nyingine ni nchi husika kuingia yenyewe *EPA* kama uchumi wake ni imara zaidi kama ilivyofanya *Mauritius*. Tanzania imechagua kuingia *EPA* kupitia Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi nchi za *SADC* zinazojadili *EPA* ni saba, kati ya hizo nne ni wanachama wa Umoja wa Forodha wa Kusini mwa Afrika *(SAC*U) ambayo imetawaliwa zaidi na Afrika Kusini. Afrika Kusini ina mkataba wa biashara huria na Jumuiya ya Ulaya, kwa mantiki hiyo tunapoingia katika kundi hili, tunaenda kutekeleza mkataba wa soko huria uitwao "*Trade and Development Cooperation Agreement"* ambao ni kati ya Afrika ya Kusini na Jumuiya ya Ulaya. Tukifanya hivyo tunakwenda kuwa soko la Afrika Kusini; tunakwenda kujiuza kirahisi kwa Afrika Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua juhudi za serikali katika kuhamasisha wanachama wenzetu wa *EAC* ili kuunda *EAC-EU-EPA*. Tunatambua juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano katika kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi yanalindwa katika kufikia makubaliano juu kundi tutakalosaini nalo *EPA*. Tunatambua kuwa maslahi ya wenzetu wa Kenya yapo *ESA*. Lakini tunaamini kabisa kwa kutumia Ofisi ya Rais wetu,

na kwa kutumia hekima ya kidiplomasia iliyotukuka ya nchi yetu, tunaweza kuhamasisha wenzetu Uganda, Rwanda na Burundi wakakubaliana nasi katika kuunda *EAC-EPA*. Vilevile, kufuatia umuhimu wa uchumi wa kijiografia, tunapendekeza kutumia Diplomasia ya hali ya juu kumwomba Rais wa *DRC* akubali kusaini nasi katika *EAC-EPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inakusudia kuendelea kukusanya na kuchambua takwimu rasmi za kiuchumi na jamii na kuendelea kufanya tafiti mbalimbali zilizoainishwa katika Mpango Kabambe wa Kufuatilia Hali ya Umaskini nchini. Kazi hii ni ya gharama lakini yenye umuhimu mkubwa kwa Taifa. Taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa nazo pia zimekuwa zikifanya tafiti za masuala mbalimbali nchini tena baadhi zikitumia takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Kambi ya Upinzani inaishauri serikali kuanza utaratibu wa kuuza takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa Taasisi ama watafiti wengine pale zinapohitajika. Kwa kufanya hivyo Ofisi hii itaweza kuingiza mapato yatakayochangia gharama za tafiti zake na hata kuwa na nyongeza ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kigoma Special Economic Zone, mwaka 2006 tulipitisha sheria kuhusu Kanda Maalumu za Uchumi (*Special Economic Zone)*. Baadhi ya mikoa tayari imeleta mapendekezo yao Serikalini kuhusu uanzishwaji wa *SEZ*. Mkoa wa Kigoma pia umefanya hivyo. Napenda kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mheshimiwa Kanali Joseph Simbakalia na Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma kwa kuandika *"concept*" nzuri sana inayoitwa "*Concept Paper and Terms of Reference for Scoping of the Project to Establish a Special Economic Zone in Kigoma."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kigoma *Special Economic Zone* unakusudia kufanya maendeleo makubwa katika Manispaa ya Kigoma-Ujiji na wilaya za jirani ili kufanya eneo hili kuwa kituo kikuu cha kiuchumi na kiunganishi cha biashara kati ya Tanzania na nchi jirani kama *DRC,* Zambia, Burundi na Rwanda. Kimsingi malengo ya mradi ni: kuboresha na kurasimisha biashara ya bidhaa za viwanda, mazao ya misitu, chakula, na madini kati ya Tanzania na nchi tajwa kupitia Ziwa Tanganyika kama njia ya kuu biashara ya ndani na kiunganishi cha Tanzania na masoko ya kimataifa; kuboresha na kupanua ukubwa na majukumu ya bandari ya Kigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Kigoma *SEZ* utapelekea kuwa na mambo makubwa manne (*four interactive and mutually supporting components*). Mambo haya ni kama ifuatavyo:- Ukanda wa Biashara Huru (*Free Trade Zone*); *Trade Logistics Hub*; Ukanda wa Uzalishaji nje (*Export Processing Zone*); na Bandari Huru *(Free Trade Zone).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa mradi huu, jumla ya shilingi bilioni 3 zinahitajika. Kiasi hiki ni kidogo sana kulinganisha na umuhimu wa mradi huu si tu kwa uchumi wa watu wa Kigoma lakini pia kwa Taifa zima. Kwa kufanikiwa mradi huu, uchumi wa mikoa ya magharibi utaongezeka. Ni matarajio yetu kuwa Serikali haitatoa kiasi pungufu ya kilichoombwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema ikaeleweka kuwa Serikali makini ni Serikali inayokubali kushaurika na viongozi mahiri ni wale wanaobuni na kutekeleza sera makini na zinazotekelezeka. Vinapokosekana vyote hivi basi tegemeo pekee ni Kambi ya Upinzani inayojali. Ushauri wetu wa kiufundi tuliotoa tangu kuanza kwa Bunge hili la bajeti ni ujumbe tosha kwa Watanzania kuwa Wapinzani tunaweza kuongoza dola kama tukipewa ridhaa.

Ni matumaini yetu kuwa serikali hii itazingatia ushauri tuliotoa bila kujali itikadi za kisiasa. Nafasi ya kufanya hivyo bado ipo. Muda ni muafaka kwa mabadiliko. Kutofanya lolote hakuvumiliki, kufanya kitu fulani hakutoshelezi, kufanya kila kitu si tu ni lazima bali ni wajibu wetu ulio dhahiri. Tufanye kila kitu tukizingatia vipaumbele. Sasa ni wakati wa kuwajibika ili Tanzania isonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Sasa utachukua Serikali baada ya uchaguzi siyo kabla ya uchaguzi, anataka wenzake wampishe sasa hivi. Nadhani itabidi tuzingatie utaratibu wa demokrasia. *(Kicheko)*

Waheshimiwa tuna wachangiaji wengi na kwa idadi yetu mpaka tuweze, hatuwezi kuzidi nane, maana yake kwa sasa hivi tutakuwa na wachangiaji sita na mchana watakuwa wawili. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Sameer Lotto na Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi watafuatia.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Wizara ya Uchumi, Mipango na Uwezeshaji. Na mimi pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wataalamu wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wameendelea kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitachangia kwa kiwango kidogo tu kwa sababu michango mingi ambayo imetolewa katika Wizara mbalimbali kimsingi inaratibiwa na Wizara hii. Nitapenda kuchangia katika maeneo yafuatayo: kwanza kabisa nitatoa pongezi kwa kazi nzuri ambazo zimefanyika katika Wizara hii lakini pia nitatoa mchango katika Idara ya Uwezeshaji wa Wananchi, nitazungumzia tofauti zilizopo kati ya walionacho na wasio nacho. Nitatoa mchango katika hali nzima ya uchumi na taasisi za fedha, na juu ya umaskini na wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, natoa pongezi kwa Wizara katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali. Wizara yetu imejitahidi katika kutekeleza mambo mbalimbali ambayo yaliainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Tumeona wenyewe jinsi ambavyo Wizara imekuwa ikitoa mchango mkubwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Wizara yetu imetekeleza mambo mengi yanayohusu mikopo ya wananchi na imejitahidi kuhusu mfuko wa uwezeshaji wa wananchi.

Vilevile imeweza kufungua mabaraza mbalimbali ya biashara, karibu katika mikoa yote Tanzania *TIC* imefanya kazi nzuri sana, halikadhalika *TASAF* wamefanya kazi nzuri kwa kutekeleza miradi mingi ya afya, na elimu. Pia watu wa takwimu na Chuo cha Mipango ambacho kinatusaidia sana katika kuleta wahitimu wengi ambao wanasaidia kuleta katika mipango ya wananchi vijijini, nao wamejitahidi. Vilevile watu wa MKURABITA wamefanya kazi nzuri ya kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo yetu na ninaomba niwataje watu wa Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki na wengine wengi katika idara hii wamejitahidi kufanya kazi mbalimbali vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba nitoe changamoto kwa wataalamu wetu wa Idara mbalimbali katika Wizara ya Uchumi, Mipango na Uwezeshaji. Changamoto kubwa inayowakabili ni juu ya taarifa mbalimbali kuwafikiwa wananchi na miongozo ya uchumi bado haijaweza kuwafikiwa wananchi wengi wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba mjitahidi mtoe taarifa mbalimbali ili wananchi wanufaike na mwenendo mzima wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe kwa Wizara iwe na kampeni maalumu za kupunguza umaskini Tanzania kwa sababu bado tunatekeleza mikakati mbalimbali ya kuondoa umaskini lakini bado ukiangalia katika kampeni zinazofanyika, kampeni za UKIMWI zinaonekana wazi, kampeni za mazingira zinaonekana wazi lakini kampeni za kuondoa umaskini Tanzania bado hazijawa na hamasa kubwa. Nawaomba wataalamu mjitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala zima la uwezeshaji wa wananchi Tanzania. Naipongeza Serikali kwa kuwawezesha wananchi kwa kutoa pesa kiasi cha mfuko wa uwezeshaji shilingi bilioni moja kila mkoa lakini bado tunahitaji uwezeshaji uendelee kukua. Tunaamini kwamba huo ni mwanzo tu lakini bado wananchi wengi hawajanufaika na hizo pesa. Kwa hiyo, Serikali ifikirie namna ya kuongeza fungu hilo lakini vilevile katika kufikiria namna bora ya kuwafikia wananchi wengi ni lazima suala la *Community Bank* lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wakipenda kuangalia mafanikio ya *Community Bank* tunawakaribisha waje Mbinga waone *Community Bank* ya Mbinga inavyofanya kazi nzuri na kuwapatia wananchi wa Mbinga kipato kizuri na Mkoa mzima wa Ruvuma. Kwa hiyo, naomba suala la uwezeshaji wa wananchi lipewe kipaumbele na hususan katika Mkoa wa Ruvuma Serikali iangalie iweke mfumo mzima wa *SEZ* kwa sababu uchumi wa Mkoa wa Ruvuma umetengwa na mikoa mingine. Mkoa wa Ruvuma uko mbali sana, ukitoa Dar es Saalam, ukitoka maeneo ambayo yana biashara kubwa. Kama Serikali haitaweka mfumo wa *SEZ* pale kwa maana ya *Special Economic Zone* bado wananchi wa Ruvuma watahangaika katika uwanda wa biashara. Naomba Serikali ilifikirie hilo na ombi hili nalitoa kwa mara ya tatu au ya nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naomba nizungumzie juu ya tofauti ya wananchi walio na kipato na wananchi ambao hawana kipato. Tofauti hii inazidi kuwa kubwa na wananchi wengi hawaonyeshi furaha na matumaini juu ya maisha yao kwa kulingana na kwamba hali zao wengi zimekuwa ni duni na naomba tofauti hizi

zishughulikiwe, kama zisiposhughulikiwa maana yake kutakuwa na tofauti kubwa na italeta migogoro katika nchi yetu.

Naomba kitengo cha kuondoa umaskini kiangalie ni namna gani kinaweza kikaweka takwimu za watu ambao hawana kipato kama vile maskini, walemavu na watu wengine wengi ambao hawana kipato ili waweze kutengeneza programu na mkakati maalumu wa kipekee kuwashughulikia watu wa makundi maalumu. Naamini Serikali imeanza mchakato wa *social protection*. Naomba mchakato huo uendelee na vilevile kitengo hiki ikibidi kiongezewe *resource* kwa maana ya wafanyakazi na pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie juu ya uchumi na taasisi za fedha. Watu wote tunafahamu kwamba Watanzania hatuwezi kupata maendeleo endelevu au uchumi endelevu bila kuwa na mitaji na katika ripoti ambayo imetolewa na *FINSCORP* ambao wamefanya utafiti wa vyombo na huduma za fedha nchini imeonyesha kwamba asilimi 54 ya Watanzania wametengwa na taasisi za fedha. Sasa hawa Watanzania wataendeleaje bila kuwa na mitaji?

Ninaomba taasisi za fedha ziangalie namna gani zitaweza kuwafikia wananchi wote wa vijijini na nalisema hili katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa makusudi kwa sababu Wizara hii ndio ina jukumu kubwa la kupanga namna gani hizi taasisi zitawafikia wananchi. Kwa hiyo, naomba sana wananchi wawezeshwe kwa kupitia taasisi za fedha waweze kupata mikopo. Naipongeza Serikali kwa kuongeza pesa kidogo kwa *TIP* ili iweze kuwawezesha wananchi wanaotaka kufanya miradi wakope wafanye miradi mikubwa na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie juu ya suala zima la umaskini na wanawake wa Tanzania. Hakuna asiyefahamu kwamba wanawake wa Tanzania wamepitia mchakato mzito sana mpaka kufikia hapo walipofikia, wamekandamizwa na mila na desturi, wamekandamizwa na mfumo dume lakini bado mfumo wa uchumi unawatenga. Ninaomba Wizara ya Uchumi, Mipango na Uwezeshwaji itengeneze program maalumu ya kuwawezesha wanawake hawa ili waweze kushiriki katika uchumi na katika programu hizo, iandae programu ambazo zitakuwa na maana katika uchumi mkuu na uchumi mdogo mdogo. Program nyingi zinaonyesha tu wanawake wanashiriki katika uchumi mdogo mdogo, wanawake wa Tanzania sasa wanataka kushiriki katika uchumi mkuu. Naomba Wizara itusaidie sana na itupatie nafasi ya kuona wanawake gani wamefanikiwa katika uchumi Tanzania ili wanawake wengine waweze kupata *role mode* na waweze kufuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala zima la sekta binafsi. Katika maelezo mengi tumeambiwa kwamba sekta binafsi itakuwa ndio injini ya maendeleo ya Tanzania; injini ya uchumi wa Tanzania. Lakini bado sijaona ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi huu na ninaposema hivi nina maana kwamba Watanzania hawa wanatakiwa waonyeshe uwezo wao katika uchumi kama Watanzania wazalendo wenyewe.

Tunakubali katika sekta binafsi Watanzania wamepiga hatua lakini tunataka kuona hatua zilizopigwa ni za Watanzania wenyewe wazawa. Kama uchumi mkuu

utashikiliwa zaidi na watu wengine itakuwa tabu sana kwetu kuendelea. Katika hotuba yake ya tarehe 30 Desemba, 2005, ukurasa wa 36 Mheshimiwa Rais, alisema, na ninaomba nimnukuu: "...tutaanza kuwawezesha Watanzania kimakundi, kundi la kwanza ni kundi la Watanzania wasomi...." Naomba Wizara inieleze ni wasomi wangapi Watanzania wamewezeshwa, wamefungua makampuni yao na kama Serikali imewawezesha ili tuweze kufanya tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Rais alizungumzia ataanza kuwawezesha Watanzania wenye biashara ndogo ndogo na biashara za kati, je, ni Watanzania wangapi wamewezeshwa? Lakini la tatu alisema atawawezesha wakulima wadogo sana, wavuvi na wafugaji wadogo wadogo je, ni wangapi wamewezeshwa ili tutathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuokoa muda nawashukuru sana viongozi wote lakini pia naishukuru Wizara hii na naomba kuunga mkono hoja yetu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Kwa kweli nakushukuru kwa kuniokolea muda maana yake unamtosha mtu mwingine.

**MHE. PAUL P. KIMITI**: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyotuletea hasa baada ya kutoa hoja yake na yale yote ambayo yamezunguzwa kwa ujumla, mimi kwa yote hayo naunga mkono hoja yake moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii kutoa rambirambi zangu kwa mzee wetu Chief Abdallah Said Fundikira ambaye sote tunamfahamu amekuwa kiongozi wetu kwa muda mrefu lakini pia ni kati ya viongozi wa kwanza kabisa kuanzisha mfumo wa vyama vingi. Yeye alikuwa na chama chake kinaitwa *UMD*, na mwanzoni sisi hatukumwelewa alikuwa na maana gani, lakini alikuwa na nia nzuri ya kuanzisha utaratibu wa kuwa na vyama vingi. Sisi tunadhani alileta changamoto kubwa sana katika nchi hii. Lakini yeye baada ya kukaa na kuona sera za Chama cha Mapinduzi zinakuwa nzuri zaidi akaamua kurudi ndani ya CCM na jana wote ni mashahidi amezikwa kwa heshima zote za chama na Serikali na tumwombee Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya Mzee wetu Abdallah Said Fundikira. *Amin!*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nataka nizungumzie mambo makubwa manne. Kwanza, ni suala zima la Wizara ya Mipango na Uwezeshaji. Wizara hii kazi yake kubwa ni kupanga. Sisi tunaelewa zamani tulikuwa na migogoro; zamani Wizara ilikuwa ya Fedha ilichanganywa na Wizara ya Mipango na ikawa kuna matatizo kwa sababu wanapoweka fedha na mipango pamoja kuna tabia ya kutegeana kwamba kwa sababu unatakiwa kutafuta fedha, hivyo unaweka mipango midogo ambayo italingana na fedha zenyewe.

Siku hizi imetenganishwa na mimi nashukuru jinsi wanavyoshirikiana Wizara hii pamoja na Wizara ya Fedha kuhakikisha mipango wanayoipanga inaenda vizuri,

nawapongeza sana Mawaziri wote wawili. Sasa tatizo nililokuwa nalo, ni kuwa huwezi kuendesha nchi bila kuwa na mipango na mipango inaanzia kwenye vijiji. Inaanzia kwenye vijiji vyetu huko lakini hakuna wataalamu wa mipango. Nataka nizungumzie hilo kwa sababu tusije tukadhani mipango itaendelea kwa kutegemea wataalamu walioko juu, mipango lazima ianzie kwenye vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishukuru Serikali na Waziri kwa kuwa amekisaidia sana Chuo cha Mipango lakini bado kazi ambayo inatarajiwa kufanyika haijatekelezwa. Chuo cha Mipango tungetegemea Mheshimiwa Waziri akipe kila aina ya msaada ili kijibu matarajio yake ya kuhakikisha mipango hasa ianzie vijijini, iingie kwenye kata, iingie kwenye tarafa, iingie kwenye Wilaya zetu.

Kwa sasa hatuna wataalamu wa mipango katika ngazi zote hizo, sijui Waziri ana mipango gani. Lakini pia ili kufanikiwa lazima tuwe na uhakika kwamba mipango hiyo inaandaliwa vizuri kwa kutumia Chuo chetu cha Mipango hapa ili kwanza kiwe na nafasi za kutosha za kutoa wataalamu hao lakini pia kiwezeshwe kuwa na hosteli za kutosha ili vijana wengi wajifunze namna ya kupanga mipango yetu ili angalau sasa matarajio ya kufuta umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la uwezeshaji, ukiangalia na ukifuatilia mpaka sasa mwananchi amewezeshwa kiasi gani ni vigumu kujua. Mheshimiwa Waziri atajaribu kutuambia. Katika Ilani yetu ya Uchaguzi tumeona kwamba yako mengi sana ambayo tulitegemea yangekuwa yameanza kutekelezwa, lakini mpaka sasa kuna matatizo makubwa matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza tuliomba katika kikao hiki kwamba Serikali iandae utaratibu wa kuwa na mpango wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Lakini pia tukaomba kama inawezekana tuwe na mkakati pia wa maagizo na ahadi zote za Rais ziwe katika mtiririko wa mpango ili tujue ahadi hizi zinatekelezwa kwa utaratibu upi. Na la mwisho tukasema pia tuwe na *time frame* kwa sababu Ilani ya Uchaguzi ni ya miaka mitano tuone tutakwenda katika utaratibu upi mwaka hadi mwaka.

Huu ni mwaka wa pili tungedhani ingetusaidia ili kuwaambia wale ambao watakuwa wanazembea katika kusimamia Ilani ya Uchaguzi wakachukua hatua ambazo zitatusaidia kusukuma suala zima la kuleta maendeleo haraka. Programu yetu ya *empowerment* ya uwezeshaji, juzi niliona Serikali ikiwabana baadhi ya wawekezaji hasa watu wa madini. Watu wa madini wameanza kurekebisha baadhi ya mikataba yao na mimi nashukuru kwa sababu mikataba ya madini ilianza kuwa ni kero katika nchi lakini siyo watu wa madini tu kwa nini tusiendelee moja kwa moja kuangalia taasisi nyingine ambazo pia tunaona sheria zake hazitusaidii ili kutoa uhakika kwamba wananchi wanashirikishwa kuwa na hisa katika makampuni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano. Ukichukua kampuni ambazo zinashughulika na mambo ya *shipping*, *shipping companies*, sheria inatamka wazi kwamba asilimia 25 ya *shares* zitakuwa za wananchi wazalendo lakini ukiangalia mpaka sasa ni wangapi wana hisa katika makampuni hayo utashindwa kujua. Na si ajabu

wanachopewa ni fedha kidogo za ahsante, wanaweza kuwa wameandikwa majina yao lakini fedha zenyewe hakuna. Ni vizuri tukaliangalia hilo. Lakini pia tuangalie suala la *EWURA* ambalo tunalizungumzia.

EWURA ni shirika na taasisi ambayo tunategemea lingetusaidia kupunguza baadhi ya matatizo tuliyonayo. Mheshimiwa Rais katika kikao chake cha juzi aliiagiza Serikali ikae na kujadiliana tuone namna ya kurekebisha kasoro kama zipo katika sheria ili *EWURA* isimamie vizuri suala zima la mafuta kwani limeanza kuwa kero. Limekuwa ni kero kwa sababu wengine wanatumia vigezo kwamba kuna sheria ambayo kwa kweli zinawafanya *EWURA* isifanye kazi yake vizuri na kwa nini liendelee, tusipolitumia shirika hilo vizuri au taasisi hiyo tutapata matatizo katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nishukuru mambo mawili: kwanza ni suala zima ambalo Mheshimiwa Ole Naiko ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa *TIC* amelifanya kule Sumbawanga. Mwezi wa sita tulikuwa na kongamano ambalo tulipata wawekezaji kutoka nchi mbalimbali na mwenzetu wa *TIC* alitusaidia kuratibu shughuli zote katika Mkoa wetu wa Rukwa. Kwa mara ya kwanza katika Mkoa wa Rukwa tulishangaa kuona kuna wawekezaji ambao kwa kweli hawakufahamu......!

**NAIBU SPIKA**: Unamaanisha *TIC*?

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndio *TIC, Tanzania Investment Center,* walishangaa kuona kwamba Mkoa wa Rukwa una vivutio vya hali ya juu kushinda mikao mingi. Na kwa sasa tunamwomba Mheshimiwa Ole Naiko, hatua ya pili ni kutusaidia kuendelea kuwahimiza wawekezaji waliofika waje Mkoa wa Rukwa waone kitu gani kinaweza kufanyika na wao wenyewe watusaidie ili angalau tuufungue mkoa wetu uweze kufanikiwa katika mambo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hii tuliyonayo nataka niiombe tena Serikali kwamba iimarishe miundombinu ya barabara kwa sababu huwezi kufungua Mkoa wa Rukwa bila kuwa na uhakika wa barabara, hilo la kwanza. Hakuna mwekezaji yeyote atakayekuja Rukwa bila kuwa na uhakika wa barabara. Mimi naishukuru Serikali imetenga karibuni shilingi bilioni 13 katika bajeti hii kwamba tunarajia sasa katika kipindi hiki barabara hii itaanza kutengenezwa.

Nataka tu nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia kwako kwamba sasa watupe *time frame* kwa sababu ni mwezi wa tatu tangu itangazwe wamekuwa kimya, hakuna taarifa yoyote kwamba imefikia hatua gani kuanza kujenga barabara hiyo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mkoa wetu, tusipofanikiwa katika hilo tutapata matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyokuwa unasema, mimi nina mfano mmoja kwamba uwezeshaji wa vijana wetu tunaweza kuufanya, tusingoje Wizara, lazima tuwe watundu na tunaweza kutoa mifano mbalimbali. Nitachukua mfano, nilipokuwa Wizara ya Kazi na tulikuwa na Mheshimiwa William Lukuvi, tulianzisha mpango Dar es Salaam na ninamwomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuendeleza mpango huo. Tuliwaomba vijana ambao kwa hiari yao wenyewe wangependa wapate maeneo ya

kulima bila kuomba msaada wa Serikali. Tulifanya makusudi mazima. Mwaka 1998 tulipata vijana Dar es Salaam wapatao 3000 walijitolea na tukatafuta maeneo sehemu za Kisarawe sehemu moja inaitwa Kidunda na nyingine inaitwa Nyani.

Maeneo hayo yalipangwa kwa kuwa na eka tatu tatu kila moja na bahati nzuri vijana zaidi ya 1000 walijitokeza na hawakuomba senti moja. Tulichofanya ni kuwasaidia usafiri wa kutoka Dar es Salaam mpaka kwenye maeneo hayo. Tulikuwa tunafanya kila Ijumaa watu wa *TAZARA* walikuwa wanasafirisha bure hao vijana mpaka sehemu hizo. Wanashinda huko na Jumamosi wanarudishwa.

Tukaendelea kwa kipindi karibu miezi sita. Mafanikio yalianza kuonekana mazuri lakini baada ya sisi kuondoka, ule mpango haukuendelea. Sasa tatizo, hivi mipango inaendelea kwa sababu fulani yupo akiondoka ndio anaondoka nayo. Tunadhani ni vizuri nalo likaangaliwa ili tuwaendeleze vijana ambao wana hamu ya kutafuta maeneo wakajiendesha wenyewe katika mipango ya kuendelea katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na muda wenyewe ndio huo, naunga mkono hoja hii ili wenzetu nao wapate nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Spika, Naibu Spika na Ofisi ya Bunge yote kwa ujumla kwa kunishughulikia vema na haraka sana na kutafuta ndege ambayo ilikuja kunichukua na kunikimbiza mara moja kwenda Muhimbili kwa matibabu.

Vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye naye alifanya juhudi ya kutafuta ndege kwenye Wizara yake na ndege ile ninaambiwa ilifika hapa lakini kwa sababu kulikuwa na ndege nyingine tayari ya Serikali basi ile ikabidi irudi tupu mpaka Dar es Salaam, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwashukuru sana Naibu Waziri wa Afya Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Wabunge watatu au wanne pamoja na Ofisi ya Bunge waliokuja kunisaidia nilipokuwa nimechoka sana pale nje kuhakikisha kwamba ninafikishwa Hospitali ya Mkoa mara moja, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kuwashukuru wananchi wa Wilaya yangu ya Ludewa waliokuja Muhimbili kutoka Ludewa lakini na wale wanaoishi Dar es Salaam waliokuja kuniona pamoja na viongozi wa Halmashauri waliotoka Ludewa kuja kuniona pale Muhimbili. Wote nawashukuru sana kwani walinisaidia sana kujisikia nipo kati ya ndugu zangu na hapa vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa Muhimbili akaungana na wananchi wa Ludewa kuniliwaza na kuwapongeza wananchi kuweza kuja kwa wingi kuja kuniona mwana-Ludewa mwenzao niliyekuwa naugua pale Muhimbili, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie fursa hii vilevile kusema kwamba kuna watu mtu ukiugua anafikiria kwamba huyu pengine ataondoka, kwa hiyo kuna watu inawezekana waliojipitisha pitisha Ludewa kule wakidhania Mheshimiwa huyu pengine

hatarudi tena lakini nataka kuwahakikishia kwamba niko imara kabisa, nitaendelea kuwahudumia wana-Ludewa waache mchezo huo tupambane 2010. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye naye alikuja Mhimbili kuniona pamoja na ndugu yangu Gaudence Kayombo, tulikuwa tumelazwa pamoja Naibu Waziri wa Mipango na kwa kweli nadhani alikuwa anakuja kuangalia jinsi Serikali inavyotuhudumia kuhakikisha kwamba tunatendewa kama wananchi wa Tanzania, ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kasoro moja, nimshukuru mke wangu na ndugu zangu wa karibu kwa jinsi walivyojitahidi kunihudumia wakati nilipokuwa naugua, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Iringa pamoja na Wabunge wote kwa ujumla, wale walioguswa na kuugua kwangu na wakanitumia *message* na wengine walikuja kuniona na kunitakia kheri, wote kwa ujumla nawashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niliomba nichangie kwenye maeneo madogo tu matatu. Kwanza kabisa ningependa kuzungumzia kuhusu uhamasishaji ambao umetajwa katika kifungu cha 34 ukurasa wa 24 ambapo tunaambiwa kwamba kituo hiki kilihamasisha uwekezaji katika Mkoa wa Ruvuma, Mara na Rukwa kwa nia ya kuhamasisha wananchi waweze kuwekeza katika fursa zitakazojitokeza au zilizopo ndani ya mkoa wao. Mimi nadhani ni kitu kizuri sana kilichofanywa na Wizara na kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile katika mkoa wa Iringa na hususan katika Wilaya ya Ludewa kuna mipango kabambe ya kuanza kuendeleza ile migodi ya Mchuchuma na Liganga na kujenga viwanda kule Liganga vya kuyeyusha chuma, nilidhani ni fursa nzuri sana kwa kituo hiki kikaanza kutusaidia.

Mimi kama Mbunge nimeanza kuwahamasisha wananchi kujiandaa kwa ujio wa viwanda pamoja na shughuli za uchimbaji lakini pengine kituo hiki kingetusaidia vizuri zaidi kama kingehamia sasa Mkoa wa Iringa na hususan Wilaya ya Ludewa kutusaidia wananchi wa kule ni vipi tunaweza tukajipanga ili kupokea miradi itakayokuja na tujiweke sawa ili tuweze kupata faida kutokana na migodi ile. Hiyo ilikuwa ya kwanza na ni ombi Mheshimiwa Waziri aangalie ni vipi anaweza kutusaidia kuja Ludewa ili watusaidie kuhamasisha wananchi wajiweke sawa.

La pili, kwenye kifungu cha 27 ukurasa wa 19 pale zimetolewa changamoto za utekelezaji wa mpango wa kiuchumi na kuongeza ajira kwa wananchi kupitia mikopo ile ya Mikoa. Sasa ninataka nizungumzie kuhusu changamoto ambazo hazikutolewa hapa. Changamoto alizoziorodhesha hapa ni za kweli lakini mimi kwa uzoefu kwenye Wilaya yangu kwanza niligundua kwamba maeneo yote yaliyokuwa pembezoni ukiacha mijini maafisa wa mikopo kwenye benki hizi walianzia kazi mijini na sehemu ambazo zinafikika kirahisi. Lakini maeneo kama ya Ludewa wamekuja mwishoni wakati huduma

za kutoa mikopo zimeshasimamishwa, na hata afisa mikopo aliyeletwa alikuwa ndiyo ametoka shule, hana uzoefu wowote mpaka apate maelezo kutoka ama Makao Makuu kwamba hapa fanya hivi na pale fanya vile.

Mimi nilitegemea kwamba ili kutenda haki wale maafisa mikopo wazoefu wangesambazwa haraka sana, kwanza, maeneo ya pembezoni kuliko kuanza na sehemu za mijini ambako kuna fursa nyingine nyingi tu.

Sasa mategemeo yangu ni kwamba katika awamu hii ya pili inayokuja Wizara itahakikisha kwamba benki hizi zinapeleka maafisa mikopo kwenye maeneo ya pembezoni zaidi ili waweze kutumia fursa iliyotolewa kinyume na utaratibu ulivyokuwa kwenye awamu ya kwanza. Lakini nakubaliana na Kamati ya Bunge ilivyozungumzia kuhusu mgao wa mkopo huo kwamba Mkoa wa Iringa una mgao wake lakini Viongozi wa mkoa kule wanaohusika na mikopo hiyo wahakikishe kwamba inagawanywa kwenye Wilaya kwa haki kutegemea na utaratibu utakaotumika ili sisi ambao hatukupata kwenye awamu ya kwanza haki yetu tuipate na Wilaya ya Ludewa ipate haki yake hata kama tumechelewa lakini tutaitumia kwa nafasi zetu.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri hili litekelezwe, tusaidie namna ya kulifanya ili Wilaya za pembezoni au Mikoa ya pembezoni isiathirike kwa sababu ambayo siyo kosa lao. Sisi kuwa pembezoni au mbali na kutokuwa na miundombinu siyo kosa letu, kwa hiyo, tusiadhibiwe kwa sababu ya makosa ambayo Serikali haikuweka miundombinu katika maeneo hayo.

La tatu, ni *Environment Impact Assessment (EIA)*, katika kifungu cha 88 Ukurasa wa 13 umezungumzia kuhusu kuanzisha *pilot project* za upandaji miti na mkasema hasa ile ambayo hainyonyi sana maji kwa niaba ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapanda miti kwa ajili ya kutengeneza karatasi na *wood chips*.

Sasa nimeshukuru kwamba mmeainisha karibu vijiji 6 kwenye wilaya zilizotajwa na upandaji umeanza. Mimi ninashauri kwamba tumeweka Sheria katika nchi hii kwamba hakuna *Project* yoyote itakayotekelezwa mpaka *Environment Impact Assessment* imefanywa na tunaomba Serikali yenyewe ianze kuonyesha mfano kwa kufanya hivyo.

Mimi nitalifuatilia hili suala tuhakikishe kwamba hivyo vijiji vilivyoainishwa kabla hawajaanza kupanda hiyo miti wafanye *Environment Impact Assessment* kwa sababu *impact* siyo kunyonya maji tu kuna *impact* nyingi sana ambazo hatuwezi tukazijua leo kabla ya mradi haujaanza lakini baada ya mradi kuanza tukagundua kwamba kumbe tulikosea, tusingeanza kupanda miti hii hapa. Kwa hiyo, uchaguzi wa miti ambayo mnasema hainyonyi maji lakini kuna athari nyingine ambazo licha ya kunyonya maji sana, nyingi tu ambazo zinatakiwa ziainishwe ili tuone hizo tutapambana nazo vipi endapo zitajitokeza hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba watusaidie na tuhakikishe kwamba hii *project* nzuri ifanyiwe tathmini ya athari za mazingira kinagaubaga vizuri

kwa kutumia wataalamu wanaoelewa, na mimi nitalifuatilia huko mbele kuhakikisha kwamba limetekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana kwa kunipa fursa na naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana ninyi ni watu wazuri sana kila mtu ameacha dakika kadhaa, nashukuru. Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, halafu nitamwita Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kama yupo.

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kwa sababu Wizara hii ni Wizara mtambuka, nataka kuongelea taarifa hizi ambazo zitakwenda kupitia Wizara hii kwenye Wizara nyingine ambazo nitaziongelea hapa.

Kwanza kabisa, nataka nifikishe salamu hizi kwenye Wizara ya Mazingira. Mimi nilipoongea katika Wizara ya Mazingira napenda nisisiteze kwamba sina nia ya kukataza watu kushuka milimani, lengo na madhumuni ni kwamba watu watakaoshuka waandaliwe fidia ipasavyo. Pamoja na hayo wanapopelekwa kuwe na miundombinu kamili mfano maji, barabara, shule na Zahanati angalau vipatikane hivyo huko wanakokwenda na mimi nishirikishwe kikamilifu katika maandalizi hayo yote. Huo ni ujumbe katika mazingira kwa Kaka yangu Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya.

Nataka kuongelea Barabara, nashukuru tumetengenezewa Barabara Ngerengere kutoka Ubena na daraja linakarabatiwa pale. Barabara hii ndiyo iliyomwangusha ndugu ya Semindu Pawa, mimi nashukuru kwama barabara hii imetengenezwa kwa ahadi ya Rais na mimi kwa kufuatilia kwa ndugu yangu Mheshimiwa Andrew John Chenge tumeweza kupata Barabara hii.

Barabara nyingine tuliyotengenezewa ni Barabara ya Mdaula – Kidugalo ambayo imekwenda moja kwa moja Jeshini, ingekwenda kilomita kama 5 au 10, upande mmoja ingeweza kufika kwenye kijiji cha Kidugalo lakini imelenga Jeshini. Nitaomba baadaye kama tunaweza Waziri akanisaidia kwamba kama tunaweza tukaichepua na ikaweza kufika kwenye kijiji ambacho hakiko mbali na Barabara hii kwenye njia panda ilipoishia hapo.

Katika ahadi ya Rais katika Barabara hizi alizungumzia Barabara kutoka Ngerengere – Tununguo ikakutana na Barabara Kuu iendayo Kisaki. Sasa napenda kujua kwamba je, katika utekelezaji wa ahadi au mipango ijayo Barabara hii ya Tununguo imeangaliwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi sasa nitazungumzia Barabara ya Morogoro– Dodoma, Barabara ya Morogoro – Dodoma nasikitika kusema ni mbovu kupindukia, ina mamia ya viraka. Naomba nirekebishe kauli hapa maana naona *Chief Whip* anaweza akasema nithibitishe mamia ya viraka. Barabara ya Morogoro – Dodoma ina viraka vingi au labda Katika Mkoa wa Morogoro nimevihesabu ina viraka 224. Mkoa wa Dodoma nimevihesabu ina viraka kwenye kipande kisichozidi kilomita moja kina viraka 29. Eneo

la Chalinze Dodoma, ina kiraka kilichoko juu ya kiraka na kilichoko juu ya kiraka. Sasa nani wa kulaumiwa Barabara hii?

**NAIBU SPIKA**: Ulipata kazi kubwa sana Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto.

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya kazi hiyo. Barabara hii nimlaumu Mheshimiwa Andrew John Chenge, hapana! Nimlaumu Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, hapana! Labda Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, hapana! Barabara hii ni lazima mtu atupiwe lawama, kuna kiongozi jasiri, mkakamavu nasikia mlokole, mkali, mtetezi wa wanyonge na mwadilifu lakini sifa zote hizo zimeingia doa kwenye Barabara hii na yeye lawana zote ziende kwake, sitaweza kumtaja, ujumbe umefika! *(Kicheko)*

Nataka kuzungumzia Jeshi. Wanajeshi wanashukuru hizi Barabara mbili nilizozizungumzia zimelenga moja kwa moja kwao. Wanajeshi wanashukuru vilevile kwamba tuna ahadi ya kuwapatia maji kutoka Ruvu kupitia Chalinze. Nimezungukwa na Kambi sita za Jeshi kwa hiyo bado wana matatizo madogo madogo kama nyumba za kuishi, nyumba zao zina sifa ya kuitwa *full suit* yaani bati juu na bati chini. Kwa kweli wanaishi katika mazingira ambayo si mazuri.

Hawa hawa ndiyo wanajeshi ambao miundombinu inapokwama kwa mfano, Barabara ya Chalinze kwenda Segera ilipomeguka na ilipokatika hawa ndiyo walikwenda kutengeneza Barabara ile. Kwa siku mbili wakatengeneza daraja ambalo Wizara ya Miundombinu ilisema itachukua zaidi ya wiki mbili, hawa Wanajeshi, *Brig.* Regard na wengineo ndiyo wanaishi katika mazingira magumu. Naomba ndugu yangu Mheshimiwa Prof. Juma Athuman Kapuya wafikirieni hawa na muwasaidie hawa Wanajeshi.Lakini wana tatizo lingine maduka ya *duty free* ambayo yamewazunguka, maduka yale hayauzi bidhaa zile muhimu ambazo wanazihitaji kama saruji….!

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto hii Wizara ni Wizara ya Mipango, sasa Wanajeshi wanaingia wapi humu tena? *(Makofi)*

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mipango ya kusaidia Wizara ya Ulinzi ndiyo ninayoizungumzia hapa. Kwa hiyo, naomba mipango ya Wizara ya Ulinzi iangalie kuwasaidia Wanajeshi.*(Kicheko)*

Mheshimiwa Naubu Spika, *duty free shops* zilizowazunguka Wanajeshi haziwanufaishi, hakuna udongo ulaya, hakuna mabati lakini kinachopatikana kule ni majokofu na luninga ambazo wengi hawana uwezo wa kuzinunua. Kwa hiyo, naomba ama kuangaliwe mipango ya kuweza kuweka maduka mawili au matatu katika Wizara ya Mipango hiyo ili Wanajeshi wakawa na maamuzi ya kuchagua.

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, sipendi sana kuwaingilia Wabunge wanapozungumza. Yaani hayo ungezungumza wakati ule tulipokuwa tunazungumza mambo ya jumla lakini hivi leo tunazungumzia Wizara hii na watumishi wake na Waziri

hawawezi kufanya *duty free* wala hawawezi kuingia kwenye mipango, hawawezi! Leo tunazungumzia Wizara yake, kwa hiyo leo ni *specific* sasa ukianza kuogelea dunia nzima leo pale tumeshapita ile *stage.* Tafadhali rudi kwenye mchango wa Wizara.

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa sababu kama nilivyosema niliamini kwamba hii ni Wizara mtambuka na masuala yote haya yanatokana na mipango ya Wizara hii. Lakini kama nimekosea kama nilivyowahi kuomba kwamba tunajifunza kwa makosa, sikuwahi kupewa semina kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda hapa sasa sijui kama nitakuwa nimepotea tena. Ninataka kuzungumzia Wizara ya Mipango iliyoandaliwa kwenye Wizara ya Maji. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA**: Hapana hiyo haipo tena.

**MHE. SAMEER ISMAIL LOTTO:** Hiyo haipo! Basi. Sasa kwa kuwa nilikuwa nataka niseme kuhusu TAMISEMI na hapa sijui haitoniruhusu na hata Mambo ya Ndani lakini kama huko kote hairuhusiwi, haya mengine ujumbe utakuwa nimeweza kuufikisha.

Nitakachosema ni kwamba ahsanteni kwa kunisikiliza na naunga mkono hoja, Mungu Ibariki Morogoro Vijijini, Mungu Ibariki Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana, na sasa nitamwita Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kama hayupo ninamwita Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi.

**MHE. GODFREY WESTON ZAMBI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Sikujua kama nitachangia sasa hivi lakini nashukuru sana kwa kuipata nafasi hii kwa sababu niliitafuta sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nianze kwa kuwashukuru Viongozi wa Wizara kwa maana ya Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kurudi tena Bungeni baada ya kutokuwepo kwa kipindi sasa kwa sababu ya kuugua. Karibu sana ndugu yangu Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitazungumzia masuala kadhaa lakini suala la kwanza linahusu ubinafsishaji wa shamba 208 lililopo kule Mbozi. Shamba hili lina ukubwa wa ekari 12,051 sawa na hekta 4,879.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwa masikitiko kidogo, kwamba shamba hili kwa taarifa za Wizara lilianza kutafutiwa mwekezaji tangu mwaka 1996 na tangu lilipoacha shughuli zake kama Shamba la Serikali mwaka 1994 wananchi wamekuwa wakililima kwa kulipia kiasi fulani cha fedha kisha wanaruhusiwa kulima. Lakini kwa sababu tuliona kuna shida ya ardhi ya wananchi wetu kule Mbozi, Mbunge aliyetangulia mzee wangu Edson Halinga na Serikali ya Wilaya ya Mbozi na mimi nilipoingia Bungeni hapa mwaka juzi tumekuwa tunaomba sana sana kwamba Serikali isitishe azma yake ya kuliuza shamba hili kwa wawekezaji kutoka nje ya Wilaya na ikiwezekana wauziwe wananchi ambao wanalizunguka shamba lile kwa sababu wana uhaba mkubwa sana wa ardhi.

Lakini kauli za Serikali zimekuwa kwamba Mbozi hakuna shida ya ardhi na ninakumbuka kuna swali liliwahi kujibiwa hapa Serikali ilisema *land pressure* kwa Mbozi ni kati ya 68% na 70%. Sikuridhika sana na majibu hayo na nikasema kwamba inawezekana takwimu zilizotumika na Wizara ya Kilimo, pengine zilikuwa za miaka 10 iliyopita kwa sasa hazina ukweli hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana niliandika barua kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mnamo tarehe 04/07/2006 nikiomba Serikali iwape wananchi shamba hilo. Waziri Mkuu aliwaandikia Waziri wa Kilimo na Waziri wa Mipango mnamo tarehe 24/07/2006 akiomba wampe *status* ya shamba hilo ili pengine Serikali iweze kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo sijapewa jibu lolote, kwa sababu niliandika barua nilitegemea ningeandikiwa barua, mpaka leo sijaweza kuandikiwa barua yoyote. Badala yake majibu pengine yalitolewa kupitia *Hansard*, sasa sijui kama nabeba *Hansard* kwenda kwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi kuwaambia kwamba haya ndiyo majibu ya Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wale wanaozunguka shamba lile, naomba nivitaje vijiji vyake: kuna kijiji cha Iwalanje, Magamba, Iporoto, Msanyila na Lwati. Waliniomba rasmi kwamba niiombe Serikali, ndiyo hilo ombi ambalo nililipeleka Serikalini lakini bado sikupata majibu. Sasa mimi najiuliza hivi kubinafsisha ni lazima kuwe ni kubinafsisha kutoka nje? Au hata ndani unaweza ukabinafsisha kwa maana ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi ambao kwa kweli wako tayari. Wakati fulani Serikali imesema kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilikuwa inadaiwa lakini tulikubali lile deni kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ianze kulipa deni kwa mashamba mengine ambayo yaliwahi kubinafsishwa huko nyuma. Sasa mimi nataka Serikali inieleze nini hatima ya mashamba yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hata kama tungekuwa tunabinafsisha kuanzia mwaka 1996 mpaka leo na shamba hili wanasema limeshatangazwa mara kadhaa lakini bado limeshindwa kupata wawekezaji. Sasa inachukua muda gani kuwapata wawekezaji kwa sababu wananchi wanapewa matamanio kwamba pengine watapewa lakini hawapewi na mwekezaji haonekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa napenda kwa kweli nisikitike sana, mwaka jana wananchi hawa ambao walikuwa wamezoea kulima lile shamba kwa kukodishwa

walizuiwa wasilime kwa maana ya kwamba mwekezaji atapewa. Mwezi wa pili waliandikiwa barua na msimamizi wa eneo lile kwamba wasilime mazao ya muda mrefu, kwa mfano mahindi kwa sababu mwekezaji angepewa shamba mwezi wa 8 au wa 9 labda angepewa lakini hajapewa mwekezaji huyo. Mwaka huu pia wananchi hao wamezuiwa kulima kwa sababu hizohizo kwamba mwekezaji atapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba sasa Serikali iwaeleze wananchi wa maeneo hayo niliyoyataja mwekezaji huyo kama yupo atapatikana lini? Atapewa lini? Ili basi wananchi wakate tamaa kwamba hawatapewa tena mashamba hayo kuliko kuendelea kuyahodhi na wakati mwekezaji huyo hajulikani mpaka leo na eneo liko vilevile kwa zaidi ya miaka 10 sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine Serikali inachukua hatua baada ya mambo kuanza kwenda mrama. Nakumbuka Mheshimiwa Estherina J. Kilasi hapa Bungeni mwaka jana alipiga kelele sana kwa sababu ya mashamba yake yale ya mpunga, aliiomba sana Serikali iwape wananchi wale mashamba kwa maana ya kuwauzia lakini Serikali ilikataa na kuendelea na mpango wake wa kuyauza.

Lakini wakati wananchi wale wamekata tamaa na kuanza kuonekana kama vile kuyadai kwa sasa ndipo Serikali iliposhtuka na kuanza kupanga mipango ya kwenda kuzungumza na wananchi wa maeneo yale. Sasa huu siyo siyo utawala bora hata kidogo na mimi naomba kama Wizara hii imedhamiria kuendelea na ubinafsishaji wa mashamba yale basi Waziri aende Mbozi akaonane na wananchi wa maeneo yale awaeleze kwamba Serikali haitawapa mashamba haya kuliko kuendelea kunyamaza tu mpaka leo. Nategemea nisikie majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Waziri ili nisije nikaenda kwenye vifungu jioni ya leo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba nizungumzie kwa kifupi suala la mikopo kwa wajasiriamali. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mikopo itaendelea kutolewa lakini taarifa ambayo tulipewa na Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na kwa takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba mkopo ambao ulikusudiwa kwa wananchi wa Mkoa wa Mbeya ule wa shilingi bilioni moja tayari ulishatumika na tayari pesa zimekwisha. Sasa nataka niiombe Serikali pamoja na kwamba wanasema mikopo itakuwa inarudishwa kwa maana ya *revolving fund* lakini wakati huu wananchi wa mkoa wa Mbeya na wale wa Wilaya ya Mbozi watumaini nini? Kwamba watasimama mpaka hizi pesa zitakaporejeshwa au Serikali itatafuta utaratibu mwingine tena wa kupata pesa ili wananchi wale ambao wana ari kubwa sana ya kuweza kukopa na kujiletea maendeleo basi waweze kupata mikopo hiyo. Nategemea Waziri pia atueleze ili wananchi hawa waweze kusikia na pengine kupunguza maswali ambayo tunaweza tukaulizwa sana tunaporudi kule majimboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda nilizungumze ni suala la ubinafsihwaji wa TAZARA. Naomba niseme kwamba mimi nimefanya kazi TAZARA kwa takriban miaka 11. Suala la ubinafsishwaji wa TAZARA limeanza kuzungumzwa

takriban miaka 10 sasa na kila tunapokutana kwenye vikao tunaelezwa kwamba mipango ya kubinafsisha Shirika hili la TAZARA ipo na inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naelewa kuna taasisi ambazo zimetangazwa baadaye sana kwamba zitabinafsishwa na tayari zimeshabinafsishwa lakini TAZARA ambayo imeanza kuzungumzwa takriban miaka 10 iliyopita mpaka leo sijaona hatua yoyote ya maana kwamba kuna mpango wa kuinusuru. Mimi naomba niseme kwamba naielewa vizuri TAZARA, kwa sasa iko kwenye hali mbaya sana kama ni mgonjwa ungeweza kusema yuko kwenye koma,ungeweza kusema yuko kwenye *intensive care*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Serikali iweke mipango na itupe ratiba nzuri inayoeleweka ya kubinafsisha Shirika la TAZARA. Leo wafanyakazi wanapata tabu hawawezi kupata mafao yao hasa wale wanaostaafu, hawawezi kupata mafao yao kwa wakati unaostahili kwa sababu hali ya shirika lile ni mbaya kuliko kawaida. Kwa hiyo, mimi naomba tuwe na mipango inayoeleweka tuwaeleze ili wafanyakazi wa shirika lile na wenyewe waanze pengine kujiweka sawa wakielewa kwamba Serikali imekuja na mpango mzuri wa kuibinafsisha taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niiombe sana Serikali, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto alipokuwa anawasilisha taarifa yake mwisho kwenye hotuba yake kama nilimsikia, naomba nikariri maneno yale kidogo, anasema: "tufanye kila kitu tukizingatia vipaumbele sasa ni wakati wa kuwajibika Tanzania isonge mbele."

Mimi nazungumzia vipaumbele pengine tofauti na yeye kidogo. Mimi ninavyofikiri ni kwamba vipaumbele vyetu vimekuwa ni vingi mno pengine ukilinganisha na *resources* tulizonazo. Kwa hiyo, naiomba Serikali na kupitia Wizara hii tuwe na vipaumbele ambavyo vinaweza vikatekelezeka kwa urahisi na tunaweza tukafanya *monitoring* kwa urahisi kuliko kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Kuna usemi unaosema kwamba, "Ukitaka kufanya kila kitu mwisho wa siku unaweza ukakuta hujafanya kitu". Kwa hiyo, mimi naomba Serikali iwe na mipango mizuri ili tuweze kufanya mambo machache lakini tukafanya kwa uhakika zaidi na nina hakika tunaweza tukasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. sasa nitamwita Mheshimiwa Kilontsi Muhama Mporogomyi na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura naye ajiandae.

**MHE. KILONTSI MUHAMA MPOROGOMYI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, leo hii nilitarajia nizungumze mambo kama matatu hivi. Moja ilikuwa juu ya *The African Peer Review Mechanism* lakini sitaizungumza. Lakini ya pili nataka kuzungumzia mipango ya Nishati katika nchi yetu, lakini nayo pia sitaizungumzia kwa sababu nimepata *note* maalumu ili nitoe ufafanuzi hapa mbele yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba katika hotuba ya Upinzani iliyotolewa na ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto amezungumzia juu ya *EPA Process* ukurasa wa 15 – 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikuarifu kwamba mimi nimeshiriki mikutano mingi sana ya *EPA* yaani *Economic Partinership Agreements* na katika mikutano yote hii sikushiriki tu lakini nilikuwa nawakilisha nchi za *Africa, Carribean* na *Pacific* kama Mwenyekiti. Yapo mambo ambayo mimi mwenyewe nimeelekeza kwa maandishi na hata mambo mengine anayoyazungumza katika hii karatasi yake mimi ni *author* wa karatasi moja inayoitwa *Negotiations Watch*. Mimi nimeandika kitu kinachoitwa *EPA Related Adjustment Costs* katika nchi hizi. Kwa hiyo, ninatambua suala hili kwa upana zaidi na vizuri zaidi kwa sababu kwa muda wa kipindi cha karibu miaka 6 mimi nimekuwa Mwenyekiti wa *Negotiations* zote za *Economic Partnerships at the level of the ACP.* Sasa naomba tushirikiane na Serikali kujaribu kueleza yale ambayo yana-*reflect* nguvu ambayo Serikali yetu inafanya na nguvu ambayo Serikali inaelekeza. *(Makofi)*

Sasa niseme hivi, ule ukurasa wa 15 anasema: "Baada ya faida zinazotarajiwa kutokana na *EPA* kwa nchi za Afrika, *Carriben* na *Pacific* ni pamoja na kuimarika kwa utengano wa kikanda (*Regional Integration).*" Angekuwa anajua mabishano ambayo tumekuwa nayo *at the level of the ACPEU Joint Parliamentary Assembly then* asingesema hivi. Kwa sababu, kama kuna kitu kimeingiliwa na *EU* ni kujaribu kutubabaisha na kutoonyesha ushirikiano mkubwa kwenye *level* ya *economic integration* katika Afrika. *(Makofi)*

Kwa hiyo katika *review* ambazo zilikuwa zikifanywa na nchi za Afrika tumejikita sana katika kujaribu kusema hivi nani anasema ingia hapa, ni wewe *EU* au ni mimi ninayechagua. *Obviously* ni nchi yenyewe inayotaka kuingia katika ushirikiano wa aina fulani kwa kuzingatia mahitaji yake makubwa sana ambayo nchi ile inayatambua.

Lakini pia ukurasa wa 16 anasema kwa kuwa tutakuwa tunapeleka bidhaa zetu Ulaya bila ya kulipa kodi nao wataingiza za kwao bila kulipa kodi kuanza. Nilizungumza juzi nikasema tutakachofanya kwenye *level* ya mazungumzo haya ni mazungumzo yatakayojadili *substantially all trade* ya huku na huku. *Substantially all trade* ina-*imply* kwamba inawezekana kuna kiwango fulani cha bidhaa ambazo sisi tutahitji kupeleka kule. Lakini lazima pia tuangalie tunacho maana kama tungekuwa tunacho kwa kiwango kikubwa *then* tusingehangaika na kusema tu-*negotiate* kwenye *study* ya *Commonwealth* ambayo ilifanywa kama miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, wameeleza juu ya matatizo yanayotarajiwa katika *negotiations* hizi na wameeleza juu ya viwango vya mashirikiano ya kibiashara haya jinsi yatakavyokuwa, lakini pia wanaonyesha gharama ambazo nchi hizi zitaingia. Suala hapa ni kweli kutakuwa na *adjustment costs* katika *levels* tatu. *Level* ya kwanza ni ile ambayo nilizungumza kwamba kutakuwa na *adjustment costs* katika kuangalia bidhaa zetu tunazozalisha na namna gani tunavyozizalisha, tunaziuza wapi na tuna *skills* za namna

gani katika viwanda vyetu. Kwa hiyo, mambo manne hapa yanazungumziwa na niliyazungumza juzi. Moja ni *fiscal adjustments* ya pili ni *trade facilitation* and *export diversification.* Ya tatu ni *production and employment adjustment* na ya nne ni *skills development and productivity enhancement*. Haya yote yapo na yamechukuliwa na kujadiliwa katika vikao hivi vya juu sana.

Lakini si hii tu, kwenye *Council of Ministers* haya mazungumzo yote yamekuwa yanakwenda. Ni kweli zipo gharama na hizi gharama tutaenda nazo lakini nchi yenyewe ndiyo itakayochukua uamuzi gani ifanye kwenye *level* hiyo. Uamuzi nchi zitakazofanya katika mazungumzo ya hivi sasa kuna *development literature* ambayo inaitwa *alternatives to EPAs.* Kwenye *alternatives to EPA* yapo mambo ambayo yamezungumzwa na mwezi wa Februari mwaka jana kuna *centre* moja inaitwa the *European Centre for Development Management* iliweka wazi *a wide range of potential alternatives scenarious to EPAs* na kule wanasema nchi inaona kwamba haiwezi kusaini mkataba huu. Nchi iamue yenyewe sio lazima tusaini, nchi inaamua yenyewe kusaini au kutosaini. Lakini inaamua kutosaini kwa kuzungumzia na kuangalia *consequences* zingine zitakazotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, linalofuata ni lile ambalo liko kwenye Namba 39 ya kwake. Anasema *Mauritius* sasa iko tayari ku-*negotiate* peke yake. Mimi hili silifahamu wala sijalisikia mahali popote, lakini ninachosema ni kwamba Mauritius ilikuwa ina-*negotiate* chini ya utaratibu wa *ESA (Eastern and Southern Africa).* Lakini Mauritius ilichokuwa ina-*negotiate* peke yake ni ile inayohusu *International Sugar Protocol* ndiyo iliyokuwa inajadili peke yao. Lakini kwenye upande wa *EPA* wako *ESA* pamoja na *Seychelles* na hawako peke yao.

Sasa hii mimi ndivyo ninavyojua *unless* kama hili limezuka katika kipindi hiki ambacho mimi nilikuwa sipo, lakini nimeendelea kupata *information* maana hata hizi za *East African* nilikuwa nazipata. Hata Mheshimiwa Rais wetu alipokwenda *EU* mimi nilipigiwa simu. Nilipigiwa simu na wataalamu ambao tumezoeana kule *EU* kwa *Directorate General* wa *Trade Development Policy* ambapo masuala haya yanafanyika. Nilipigiwa simu, alisema, "wameshukuru sana Rais wetu alikuja kuzungumzia masuala ya *EPA*. *EU* walifurahi sana kuonana naye na wamezungumza kwa kiwango kikubwa na akasema anafikiri wameelewana vizuri." Kwa hiyo, kama *level* ya juu ya Rais imekwenda mpaka *EU* kufanya hii kazi haiwezekani isiwe inafanya kazi ambayo inaeleweka kwa kiwango hicho halafu tukasema hawafanyi kitu chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalofuata ni hili la Kenya. Mimi nafikiri la Kenya tulichukue tulifanyie kazi kama nchi. Tunalifanyia kazi kama nchi, tusiseme hawa si wetu maana tumeshaingia mkataba nao huu wa forodha. Kama Kenya wameona kwamba pengine muda uliobaki kuanza ku-*negotiate EPA* nyingine Januari, 2008 itafika kesho kutwa na wakasema bora tukae hapa tulipokuwa maana tumeshafikia kiwango kikubwa cha majadiliano, inawezekana ni mojawapo ya sababu maana hatujapata maelezo ya kutosha.

Sasa hili linaloelezwa hapa kwamba sisi tutakuwa tunatangatanga, si kweli kwamba tunatangatanga, mimi nafikiri ni katika kutafuta muafaka na nchi ambazo tuna ushirikiano mkubwa nazo. Hizi nchi hatuwezi kuziacha lazima tuendelee nazo, tuendelee kushirikiana nazo na kadri tunavyoshirikiana ndivyo tutafikia muafaka na muafaka huu utatufikisha mahali ambapo tutaweza tukasaini mkataba mzuri na huo mkataba ukaweza kutusaidia na sisi tukaendelea. Tuelewe kwamba *EPA* si kitu rahisi sana unachoweza kukizungumzia ama mitaani au barabarani, kwa kweli ni *complicated*. *EPA* ni kitu *complicated* si kitu tu unaweza kuzungumzia hivyo. Ukisoma makaratasi ya *EU*, *papers* za *EU* wanavutia kwao, na sisi watu wetu wanavyosema wanaandika msimamo wetu. Msimamo wetu unasema ninyi mlisema tukishaungana pamoja kazi yenu kubwa itakuwa ku-*support economic integration*. Sasa yako wapi yale mliyosema na yako wapi haya mnayotueleza, ndivyo wanasema. Lakini ukienda kichwa kichwa utakuta wanakuambia maneno mengi na *very correct* wanasema sasa bwana wewe huku unakokwenda sio kwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome tu kitu kimoja au ninukuu juu ya ile ambayo nimesema wameandika wataalamu wa *Development Management* na watu wa *Development Studies Sussex University,* wameandika pia *paper* ambayo inahusiana na hii *alternative EPA*. Naomba ninukuu wanasema, "*In the area of "alternatives" EPAs is an area where considerable work has recently been initiated and this includes works undertaken by Dr. Chris Stevens of the Institute for Development Studies at Sussex University and a review of work in this area undertaken by European Centre for Development Policy Management. The detailed work undertaken in both these contexts could usefully inform ACP Parliamentarians as they grapple with the implications of EPAs; alternative EPAs and the "alternatives" to EPAs, for people they represent"*

Kwa hiyo, tuna wajibu wa kuendelea kusoma haya na kuangalia ni wapi tunahitaji kwenda ili tuweze kusaini mkataba huu tukiwa tunajua tunachokifanya. Haya maneno mawili tuyatenganishe. *Alternative EPA and the Alternatives to EPA*, ni mambo mawili tofauti sio kitu kimoja. Kwa hiyo, ndugu yangu Zitto sio kwamba tumepotea, tunakwenda na kule tunakokwenda, tunakuona sio kwamba hatukuoni na sio kwamba hatuoni kile tunachokifanya.

Mimi nina imani Serikali inajua inachokifanya na nina imani na wale tunao-*negotiate* tunajua tunachokifanya. Na maneno haya sio maneno ya kuokotwa tu mahali popote ni maneno ya kujadiliana, ni maneno yanayokwenda kwa utaratibu. Sasa utaratibu huu tunaozungumza sisi hauwezi kuwa utaratibu wa nguvu, ni utaratibu wa majadiliano na mimi nina imani majadiliano haya lazima yawe majadiliano yanahusisha Serikali kwa Serikali, nchi kwa nchi. Hata hayo mengine yanapotokea tunapokaa mimi nina imani tutakuwa tunaelewana. Mimi nina imani siku moja tutafika mahali tuseme sasa tuna-*negotiate* chini ya *East African Community* kama *EPA configuration.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa ufafanuzi huo na mimi naomba niunge mkono hoja iliyotolewa na nimpongeze sana Waziri wa Mipango kwa hotuba yake nzuri, na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mporogomyi anatuwakilisha sisi katika *ACP* kwa miaka mingi. Sasa kanuni zetu zinatoa fursa kwa mtu ambaye ametumwa au anahusika na jambo fulani kuweza kulisemea Bunge, kwa hiyo ndiyo sababu amepewa nafasi hiyo.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa wasaa huu wa kuweza kuchangia hoja ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kabla sijasema lolote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumponya ndugu yetu, kaka yetu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Kayombo ambaye leo tuko naye hapa Bungeni. Nitashukuru sana wakati wa majumuisho Waziri wa Wizara hii akitueleza wigo wa masuala ya uwezeshaji. Kwa sababu inavyoonekana wengi wanaelewa uwezeshaji labda ni kutoa kiasi cha pesa kupeleka kwenye Mabenki au kuandaa mazingira ya ubinafsishaji. Lakini ninaamini uwezeshaji ni pamoja na kutoa elimu kwa wananchi wa Tanzania kuweza kujua fursa zilizopo katika maeneo yao na waweze kuzitumia fursa zile katika kuondoa umaskini walionao. Sasa kama tafsiri hii ni sahihi basi nitashukuru sana Waziri akiithibitisha. Hali kadhalika kutokana na tafsiri hii ya uwezeshaji napata kigugumizi kutokana na hali iliyojitokeza baadhi ya Wilaya katika nchi yetu kufuatia kutoweza kupata zile fedha za uwezeshaji ambazo wengi tunaziita mamilioni ya JK.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Tunduru ni miongoni mwa Wilaya ambazo safari hii wananchi wake hawakuweza kupata pesa hata mwananchi mmoja. Hili nimeweza kulithibitisha juzi baada ya kuongea na *Branch Manager* wa *NMB* Tunduru. Ingawa Waziri wakati anafanya majumuisho ya hotuba yake ya Mipango aliwahi kutamka kwamba Wilaya ya Tunduru haina benki na ndiyo maana hazikupelekwa zile pesa.

Tunduru Benki ipo *NMB* na iko pale toka mimi nikiwa Sekondari na ni miaka 27 toka nimalize sekondari benki ile ipo pale. Ila kikubwa ninachoamini bado wananchi wa Tunduru walikuwa hawajapata elimu ya kutosha juu ya masuala ya ujasiriamali na hii ni changamoto kubwa kwa Wizara. Tatizo hili naamini kabisa si la Tunduru peke yake ni tatizo la wananchi walio wengi wa nchi yetu, elimu ya ujasiriamali haijaenea, hivyo ni jukumu la Wizara hii kuhakikisha kwamba wanapatikana wataalamu wa kutosha wa kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wananchi wa Tanzania, bila elimu bado Watanzania tutakuwa katika matatizo makubwa. Fursa tulizonazo katika maeneo tunayoishi ni nyingi lakini kwa kuwa elimu ya ujasiriamali hatuna, wengi tunashindwa kuzitumia fursa zile zilizopo ili kuweza kuondoa umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitamwomba Waziri atueleze kama kuna mipango yoyote ya kuwawezesha wananchi wa Tanzania hasa wale wa makundi maalumu. Ninaamini kabisa wengi wetu tunafahamu kwamba tuna tatizo kubwa la ajira kwa vijana. Je, Wizara yetu ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji imejiandaa vipi kuhakikisha kwamba hawa vijana wetu wa Kitanzania wanawezeshwa ili waweze kutumia fursa zilizopo katika mazingira waliyopo kuweza kuondoa umaskini walionao. Vilevile kundi lingine ni la akina mama, ambao ndio walezi wa familia zetu za

Kitanzania. Je, Wizara ina mikakati gani juu ya kuwasaidia akina mama waweze kuzitumia fursa walizonazo kuweza kuondoa umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi lingine ambalo mara zote limekuwa likisahauliwa ingawa sisi wote tunaelekea huko ni kundi la wazee. Hakuna mahali ambapo nimeona hawa wazee wakitajwa juu ya kusaidiwa ingawa michango yao ndiyo iliyotufikisha hapa tulipo. Kwa bahati mbaya au nzuri sisi wote tunaelekea huko uzeeni. Ninaiomba sana Wizara hii ijaribu kuliangalia suala hili la wazee, tuwawezeshe, tuwajengee mazingira ili umri wao uendelee kuwa mkubwa zaidi, kinyume cha hivyo tukishafikia miaka 60 basi matarajio ya kuondoka katika dunia hii yatakuwa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nazungumza na *Branch Manager* wa *NMB* Tunduru aliniambia kwamba benki ile ina ripoti Mkoa wa Mtwara ingawa kiutawala Tunduru iko Mkoa wa Ruvuma. Nilivyotaka atoe ufafanuzi akasema hii ni mikoa ya Kibenki. Sasa je, mwananchi wa Tunduru atakapotaka kuchukua hii mikopo ya ujasiriamali ni fungu lipi ambalo litakaloelekezwa kwa mwananchi wa Tunduru; je, ni fungu la Mkoa wa Ruvuma ambako anaripoti kwa utawala au Mkoa wa Mtwara ambako kibenki Tunduru inaripoti Mkoa wa Mtwara? Hili nitaomba sana ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho yake ili kuondoa utata ambao unapatikana katika Wilaya yangu ya Tunduru kiasi imepelekea wananchi wale wakashindwa kupata mikopo. Hii na kitu cha kusikitisha zaidi hakuna hata mtu mmoja ambaye amepata fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naiomba Wizara pamoja na kwamba hili limezungumzwa na wachangiaji wenzangu waliotangulia, tumeambiwa kwamba kutakuwa na awamu nyingine ya mikopo ya uwezeshaji. Hili suala la kwamba pesa zinapelekwa kwa Mkoa ni zuri lakini sasa katika hii mikoa kuna Wilaya nyingine ambazo zinaonekana wajanja ni wengi au mazingira ya miundombinu imekuwa mizuri zaidi kuliko Wilaya zingine. Matokeo yake zile Wilaya ambazo hazina mazingira ya miundombinu, zinakosa mikopo ile kwa sababu tu hazina miundombinu ya kutosha. Mimi nashauri awamu inayokuja pamoja na kwamba mgao utakuwa wa kimkoa lakini vilevile zitakapofika katika Mkoa kuwepo na mgao katika Wilaya. Kiasi fulani kiende Mbinga, kingine Namtumbo na sisi wa Tunduru basi kiasi chetu kiwepo pale. Safari hii Tunduru tumekosa kwa sababu fedha zote zimechukuliwa na wenzetu wa Mbinga, Namtumbo na Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu wake, watendaji wa Wizara pamoja na Taasisi zao kwa kutayarisha bajeti nzuri. Pili, nimpe pole ndugu yangu, rafiki yangu Bwana Kayombo kwa matatizo ya afya yaliyomkabili na namwombea Mwenyezi Mungu azidi kumjalia nafuu ya haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kama ifuatavyo: Wizara hii kama ambavyo wenzetu wa Kamati ya Uchumi na Mipango walivyotukumbusha kwamba Rais alisema alipokuwa anazungumza nao kwamba ndio ubongo wa Serikali, kwa maana nyingine lugha ya kigeni tunasema ni *think tank*. Kwa hiyo, kama *think tank* inawajibika sana katika kutayarisha mipango kabambe ambayo ndiyo itakuwa ni dira ya maendeleo ya nchi hii na Wizara nyingine zote zikafuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulifanya hili, huko nyuma nilipata kushauri kwamba labda ingekuwa ni vizuri na napenda nisisitize tena Wizara itafute utaratibu wa kuwa na jopo la wataalamu ambao wanaweza kutumia lugha yoyote ile wawaiteje lakini wawe ni wataalamu ambao watakuwa na sura pana zaidi ya uchumi wetu kisha wawashauri namna gani uchumi huu kwa ujumla wake unahitaji kupangwa na ni sekta zipi zipewe kipaumbele. Hapa ni suala la kuangalia uchumi kwa upana na ni sekta zipi zipewe kipaumbele. Hizo sekta kwa ujumla ni zile ambazo zinapaswa kutoa mchango wa haraka katika maendeleo ya uchumi wetu pamoja na vilevile kuongeza kasi ya uchumi huu kukua. Sasa hivi katika takwimu tulizonazo ni kwamba uchumi wetu baina ya sasa mpaka 2009 utakuwa kati ya asilimia 7.3 mpaka asilimia 7.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi hazitupi matumaini makubwa sana na hasa tukilinganisha na ukweli kwamba *population* yetu inakua kwa wastani wa asilimia 2.9 takriban asilimia 3. Kwa maana hiyo *real growth* ya uchumi wetu ni hiyo *GDP growth* toa ile *population growth,* kinachobaki ndio ukuaji wa uchumi yaani *real terms.* Kwa maana hiyo uchumi wetu unakua kwa asilimia kati ya 3.234 hivi asilimia ambazo hazitusaidii sana katika kuleta mapinduzi ya haraka ya kupambana na tatizo hili la umaskini na kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, hili ndilo ambalo nilikuwa nataka wenzetu wangejaribu kutafakari kwa kutumia wataalamu wao na ikiwezekana waongeze kwa kutumia jopo la wataalamu kutoka nje ya Wizara kama vile ambavyo *Business Council* inavyofanya ambayo inaweza ikashauri katika masuala ya biashara. Tuna *CTI* inashauri katika masuala ya viwanda na kadhalika, kwa nini tusiwe na jopo la wataalamu ambalo litashauri katika masuala ya kiuchumi kuisaidia Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, nataka nitie mkazo kwenye sekta ya kilimo. Kama tunavyofahamu sekta hii inaajiri takriban asilimia 80 ya Watanzania, ina- *contribute* karibu asilimia 45 ya *GDP* ya nchi yetu. Ina-*contribute* karibu asilimia 60 ya *foreign exchange* ya nchi hii. Kwa maana hiyo hii ni sekta muhimu sana. Tunapozungumzia kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa Tanzania kwa kweli mahali ambapo tunapaswa kuelekeza nguvu zetu zote ni katika sekta ya kilimo, tunafanya nini katika sekta ya kilimo?

Katika sekta ya kilimo hatuwezi tukaiendeleza sekta hii na jembe la mkono na kwa kutegemea mvua za mwaka hadi mwaka. Ni kweli kuna mipango ya *irrigation*, ni kweli kuna mipango ya kuhimiza matumizi ya pembejeo kutumia plau pamoja na matrekta. Lakini matumizi ya pembejeo, plau na matrekta yanahitaji fedha. Ni lazima Wizara hii ingekuja mbele kabisa ikaieleza Serikali kwamba ili tuweze kupindua kilimo kiwe ni kilimo kwa maana ya *(green revolution*) mapinduzi ya kijani ni lazima kuwe na *credit system* ya muda mrefu, wa kati, ili kuwawezesha wakulima waweze kupata hizi

pembejeo, matrekta na kadhalika vinginevyo tutakuwa tunazungumza tu kama ambavyo bado tunazungumza. Tunahitaji *real action* ambayo itaendana na dhana na makusudio yetu ya kuleta mapinduzi ya kijani katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa hapa nitoe pongezi kwa Wizara na kwa maana hiyo kwa *UNDP* kwa kuchagua kituo au kijiji cha Mbola katika Wilaya ya Uyui kule Tabora kuwa ni kijiji cha mfano wa namna ambavyo unaweza ukawaendeleza wanakijiji katika kuanzisha taratibu mpya za kilimo. Kijiji kile sasa kinaanza kutoa matunda mazuri na baadaye ni utaratibu wa Serikali kupitia Wizara hii pamoja na Kilimo nadhani ku-*multiply* yale matokeo ya Mbola ki-nchi.

Naipongeza sana Serikali kwa kuwa mfano wa kijiji hiki, kinafanya vizuri lakini vilevile ningependa nitumie fursa hii kuiomba Wizara itumie uwezo wake kuiomba *UNDP* kwamba maadamu wameanza na kijiji ndani ya Mkoa wa Tabora na kwa sababu Mji wa Tabora uko nyuma, Mji wa Tabora ni mji wa kihistoria, una kila sababu ya kuendelezwa, kwa sababu ambazo hatuzijui unakwamakwama maendeleo yake. Naiomba Wizara ijaribu kutafuta uwezekano wa kuuingiza mji wa Tabora kama mradi wa *UNDP* unaofanana na kijiji cha Mbola sasa tutoke kwenye kijiji twende kwenye mji na mji wa kufanyia hivyo uwe ni mji wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la miundombinu tumelizungumza sana lakini ni kazi ya Wizara hii sasa kuangalia miundombinu kwa ujumla wake ndio msingi wa maendeleo ya nchi. Mambo mengine yote tutazungumza, tuendeleze kilimo sawa, lakini ukilima bila kusafirisha mazao yako kutoka pale ulipoyalima kuyapeleka sokoni hujafanya kitu. Kwa maana hiyo miundombinu ni muhimu na hasa barabara pamoja na reli. Sasa hivi kuna habari ya Reli ya Kati kubinafsishwa mambo hayo yanaendelea, sawa.

Lakini ningependa Wizara hii itupe uhakika wa hasa hasa katika kuanzisha Kampuni ya Tanzania *Railways Limited.* Kampuni hii hisa zake ni ngapi na wanahisa ambao wamegawana asilimia 51 kwa 49 wamejitayarishaje kuchangia hisa hizo. Kwa dakika hii hapa ninavyoongea je, hao wabia wawili wamekwishaingiza hisa zao katika Kampuni hiyo, kwa sababu ni jambo muhimu sana Reli ya Kati ifanye kazi. Reli ya Kati ikifanya kazi hiyo peke yake itaiongezea nchi pato hili kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka bandari ya Dar es Salaam kwenda Kigoma na baadaye Kongo kuna mzigo wa takriban tani 4,000,000, hazina usafiri wa uhakika. Usafiri wa uhakika ni Reli ya Kati. Kwa maana hiyo Reli ya Kati ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii. Tukiwekeza pesa kwenye reli hii kama ambavyo sasa tunaelekea kufanya tutapata mafanikio makubwa kwa muda mfupi sana. Hadithi hiyo inaendelea hata kwa barabara ya kati kutoka hapa Dodoma kupitia Tabora kwenda Kigoma, ni barabara muhimu sana ningeiomba Wizara hii kama msimamizi izingatie ushauri huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante sana.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Nakushukuru kwa sababu umetusaidia kutumia muda huu ingawa wewe katika hali ya kawaida usingefikiwa hata kidogo. Sasa mchana tukirudi tutakuwa na wachangiaji wawili. Mheshimiwa Anne Malecela ambaye amechangia mara mbili na Mheshimiwa Ndugai amechangia mara mbili, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoahirisha nilikuwa nimetoa nafasi kwa Mheshimiwa Anne K Malecela na Mheshimiwa Job Y. Ndugai. Sasa namwita Mheshimiwa Anne K.Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii muhimu ya Bajeti ya Makadirio ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ambayo ndiyo itakayotupa picha kamili. Pamoja na hayo, naomba nishukuru kwa kupata nafasi hii, kwa sababu nategemea katika vikao vilivyobaki, sitapata nafasi tena ya kuchangia katika Wizara nyingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika kuchangia Wizara hii, nitakwenda zaidi katika majukumu ya Wizara hii kubwa. Jukumu la kwanza ni kuchambua na kubuni sera za uchumi jumla, kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi. Jukumu lingine ambalo nitapenda kuligusia ni jukumu la kubuni, kufanya utafiti na uchambuzi ya masuala muhimu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jukumu la tatu ni kuratibu, kuhimiza na kufuatilia masuala ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa historia fupi kidogo ya uchumi wa dunia, uchumi endelevu. Katika Karne ya Kumi ya Nne mpaka ya Kumi na Saba, Mataifa ya Ulaya ndiyo yaliyoanza kuleta mageuzi kiuchumi. Ilifikia mahali Mataifa ya Ulaya yakaona kwamba, uchumi ulikuwa hauendi vizuri si kwa wao tu lakini kwa dunia nzima. Kipindi hicho kwa Ulaya walikuwa wameendelea sana kielimu, kisiasa na kwa kweli walikuwa wamefikia mahali hata uwezo wa kifedha ulikuwa ni mkubwa. Karne ya Kumi na Nne mpaka ya Kumi na Saba kukatokea mageuzi ya kiuchumi kutoka kwenye uchumi ambao ulikuwa ni wa kawaida wakaenda kwenye uchumi wa viwanda na hapo kukatokea mageuzi ambayo yalionesha ni endelevu kuanzia Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Marekani nayo ilipofika mwaka 1776, baada ya kupata uhuru tu nao waliingia kwenye mageuzi ya kiuchumi. Kuanzia kipindi hicho mpaka sasa ,uliwengu umekuwa unaendelea kuwa katika mageuzi ya kiuchumi mpaka sasa hivi tumfikia kwenye sura ya ubepari. Hatuwezi kusema ujamaa ni ubepari, *globalization* ina sura ya ubepari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mada yangu kubwa ambayo ninaomba niinogelee kwa msisitizo lakini kwa unyenyekevu, Serikali ya CCM, Serikali yetu wenyewe tufike mahali na nchi kwa ujumla na sisi sasa tunapaswa kuleta mageuzi kiuchumi. Kwa nini nazungumza hivyo? Kwa sababu tumeona umuhimu wake, bila ya sisi kufika na kuamua

kwamba sasa tunaanza kugeuza uchumi wetu uwe uchumi endelevu *seriously* kimatendo. Katika mfumo huu wa *globalization* wakati tupo kwenye ushindani wa mataifa makubwa na mataifa maskini na hatuwezi kujiweka kando ni lazima na sisi tukubali kuleta mageuzi katika uchumi wetu. Lakini tuletee mageuzi kivitendo, sio mageuzi haya ambayo tunazungumza kila siku. Tusipokubali kuleta mageuzi, tukubali kufa kiuchumi. Huku duniani kuna mataifa makubwa ya aina mbili; Mataifa ya kwanza ni ya ulimwengu wa kwanza, *the giants*, ni mataifa makubwa na matajiri. Sisi tupo kati ya yale mataifa maskini eti maana yake natumia neno eti kwa sababu mimi siamini sana. Lakini sisi tupo katika kundi la mataifa maskini.

Ukiangalia kwa sura, utaona mataifa ya ulimwengu wa kwanza hawa wanaojiita matajiri wanacho wanachoringia. Wanaringia teknolojia ya kisasa zaidi. Wanaitumia teknolojioa ya kisasa katika *production*, katika uuzaji lakini sisi hatujawa kwenye kundi hilo. Sisi tupo kwenye kundi la umaskini, lakini na sisi ukiangalia kiundani tunavyo vya kulingia, ambavyo Mataifa ya Kwanza hayana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna rasilimali na utajiri wa Tanzania utatoka kwenye rasilimali zake tu basi kama zitatumika vizuri. Naomba nirudie, kama zitatumika vizuri. Naomba nijinukuu mwenyewe nilipokuwa nachangia Hotuba ya Wizara ya Fedha nilisema hivi: "Sisi Watanzania si maskini, umaskini tunausababisha sisi viongozi na wenzetu ambao wapo kwenye nafasi za utekelezaji (watendaji)." Kuna watu wakaguna wakasema ameanza huyu. Lakini naomba nimsifu Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe, anastahili na naomba nimsifu Waziri wa Maliasili na Utalii na Naibu Waziri, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, mimi ni mwalimu wangu amenifundisha ualimu, wameanza kutuletea mageuzi ya kiuchumi tena kivitendo. Iwapo tutatoka kwenye Sekta ya Wanyamapori kama tutatoka kwenye Bajeti ya 2006/2007, shilingi bilioni 11, lakini 2007/2008 shilingi milioni 33.3. Hivi hayo si mageuzi kiuchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba niseme hivi, tunazo rasilimali nzito za aina tatu. Tuna maliasili na utalii, tuna madini, tuna bandari na vingine vingi, lakini niishie katika hivi vitatu. Mimi ndipo ninapotaka kumwomba Waziri wa Mipango, anisikilize kwa hayo. Tuna maliasili na utalii, tuna madini na tuna bandari. Mimi naomba kabisa Tanzania turingie maliasili hizi, hawa wenzetu mataifa makubwa wanapokuja na *modern technology* yao watukute na sisi tuna rasilimali yetu tukutane katikati. Jambo walilofanya wenzetu wa Maliasili na Utalii kipindi hiki ni maringo, wameringia rasilimali yetu ya utalii. Wameringia magogo yetu, wameringia simba wetu, ndovu wetu ambao tulikuwa tunawauza kwa bei ya kutupa ndiyo wamegundua, kwa hiyo, mtu unaringia ulichonacho. Akitaka kuja kuwinda tembo kwa kiasi hiki aje, hataki aache. Lakini iwapo sisi Watanzania, rasilimali yetu tutakuwa tunai-*surrender* tu, tutaendelea kuwa maskini na wala hata hiyo mipango itakuwa haiendi na wala Wizara ya Fedha kila siku tutakuwa tunaambiwa kasungura kadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Tanzania turinge, madini tunayo mengi, tuna dhahabu, almasi, *nikel*, tuna rubi, tuna *green garnet*, tuna *soda ash*. Lakini *on top of that* sisi tuna *Tanzanite.* Hapa nataka nisimame kidogo, tuna *Tanzanite* sisi peke yetu duniani na ndiyo maana jina la *Tanzanite* linafanana na Tanzania lakini je, *are we the only*

*producer and supplier of Tanzanite?* Tunapata faida kubwa kutoka kwenye *Tanzanite?* Ukizungumza hapo utapewa kiswahili kingi, lakini mimi jamani nataka nizungumze kidogo tena kwa unyenyekevu, Serikali tunaomba turingie haya madini. Haya madini tuweke *enough restrictions,* tuweze ku-*monopolise market* ya *Tanzanite* jamani, tusipofanya hivyo tutaendelea kuwa omba omba wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tunalipuuza, mimi mara ya kumi nazungumza kwamba inawezekana, mtu mara moja anasema haiwezekani. Kasema nani jamani? *Have you attempted?* Kabla hata hatujajaribu, tayari tunaanza kusema sisi hatuwezi. Kuna uwezekano mkubwa sana Watanzania kukopa, tunaweza kuwa na *processing plant* hapa nchini, madini haya tuka-*monopolise* wenyewe. Hakuna mahali pengine tutakapo nyanyukia zaidi ya kwenye maliasili zetu. Mwenyezi Mungu, aliamka akatugawia hivi vyote bure kabisa, akaipa hii nchi amani kwamba, mnaweza mkafanya kazi saa 24. Lakini Watanzania sisi tuna *resources* zetu hizi ambazo ndiyo za kutunyanyua tunawaachia wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi hapa kwenye *Tanzanite* ninaomba pasimamiwe vizuri, naomba kidogo ninukuu Biblia. Kwa wale wanaosoma Biblia mkasome Zaburi ya 126:5-6, Muhubiri 11:4, 2 Samwel 5:

**NAIBU SPIKA:** Uombe ruhusa kama unataka kunukuu.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ruhusa kunukuu Biblia. Zaburi126:5-6, Muhubiri 11:4 na 2 Semwel 5 na Yoshua 1:9. Mwenyezi Mungu, kupitia Biblia analiambia Taifa: "Hata kama Mungu anakupenda kivipi au umebarikiwa kivipi, lakini kama hutakuwa hodari, hutajitahidi, hutakuwa shujaa, lengo la Mungu ni vigumu kutimia na unapotaka kwenda mbele ukiangalia upepo, hufiki popote maana utashindwa kabla ya kuanza safari."

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba na kuisihi Serikali sasa kama ambavyo Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe amethubutu, maana huku ni kuthubutu, ameleta mageuzi makubwa kweli kweli. T unaomba mageuzi haya yaende kwenye madini, mageuzi haya yaende kwenye bandari, tena Mheshimiwa Waziri wa Madini ukiunda hiyo Tume yako ya kuzunguka, niweke mimi pia, muweke Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo huko, tutakusaidia kazi. Tulete utaratibu mpya kwenye madini yetu, hatuna njia nyingine ya kututoa tulipo zaidi ya kwenda kukamata rasilimali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona hakuna kingine cha kuringia, turingie nini sasa ni kuringia rasilimali zetu tu. Lakini katika kuhangaika huku, Ulaya walipokuwa wanaleta mageuzi ya kiuchumi, Wachina, Wamarekani walipokuwa wanaleta mageuzi ya kiuchumi, watu wengi kweli walikufa. Ukisoma historia ya uchumi, watu wengi walipoteza maisha yao na sisi tukubali watu wengi wapoteze maisha yao tunapoleta mageuzi ya kiuchumi. Juzi alivyoleta mageuzi ya kiuchumi, Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe kuna *risk* pale mmeisikia, ndiyo kufa kule. Tunaomba kweli wale waliokuwa wanatuhujumu wachukuliwe hatua na tusikie tukifika kwenye madini tunataka tuingie kwa undani, uchumi usogee.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye bandari, watakaokufa wakati tunafanya marekebisho, jamani tutawaacha wafe sisi tusonge mbele. Mimi la kwangu kubwa ninaomba nizungumzie hilo la kwamba, bila ya kuleta mageuzi kiuchumi, Tanzania tutakuwa tegemezi mpaka mwisho wa maisha yetu na sisi viongozi na watendaji wote nchini, mtu hustahili kuitwa kiongozi kama huna sifa pamoja na nyingine tatu; Uzalendo, Upendo na Huruma kwa wananchi maskini wa nchi hii. Lakini viongozi sisi hatuna huruma, upendo wala uzalendo. Ndiyo maana yametokea haya yaliyotokea Wizara ya Maliasili na Utalii. Tulikuwa tunapata hasara lakini ni watu kujilimbikizia. Kwa hiyo, mimi ninaomba tukubali wale watakaokufa wafe, tusonge mbele lakini tulete mageuzi kiuchumi kama ambavyo ameleta Mheshimiwa Profesa Jumanne A. Maghembe sasa kwenye madini, twende na kwenye bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi ya kuzungumza, nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati anapoleta majumuisho, hebu basi atuelekeze katika mipango tutaona sura tofauti, tutaona mageuzi kidogo mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ndiyo ubongo wa Serikali, ndiyo *think tank.* Wizara hii ndiyo inashughulikia mambo mengi yanayohusiana na mipango na majadiliano kati ya nchi yetu na kwingineko duniani, kuhusu mambo ya biashara na uchumi kwa ujumla, kabla ya nchi yetu kuingia mikataba mbalimbali. Nawaomba sana nikiendeleza alipomalizia Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, tuwe makini sana, tuhakikishe maslahi ya nchi yetu yanazingatiwa zaidi.

Mmarekani mweusi, Marehemu Martin Luther King, aliwahi kuandika kitabu katika uhai wake akakiita "*The Foolishness of God*," sitatafsiri maana yake ninaweza nikakosea. Alikuwa akizungumzia habari ya mipango ya ajabu ajabu ya Mwenyezi Mungu. Akajiuliza ni kwa nini boga au tikiti likawa na tunda kubwa kuliko embe ambalo shina lake ni zito, kubwa na la uhakika, lakini hili tikitiki shina lake ni dogo sana, ni mipango ya Mwenyezi Mungu. Hii inaonesha umuhimu wa mipango. Kwa nini Mwenyezi Mungu, aliumba masikio mawili kwa mwanadamu lakini akampa mdomo mmoja ni mipongo ya Mwenyezi Mungu na mifano iko mingi kuonesha kwamba, mipango ni muhimu sana. Hapa tuko kwenye kipindi cha bajeti, huwezi kuwa na bajeti kabla ya kupanga lazima uwe na mipango kwanza baadae unatengeneza bajeti, unatenga fedha, unaonesha jinsi unavyozipata na unavyozitumia katika kupitia mipango yako ili itekelezeke.

Lakini vilevile hapa Afrika wakati wa uhuru, Rais wa zamani wa Ghana, ambaye watu wote tunampenda Marehemu Nkrumah, aliwahi kusema kwamba, tafuteni uhuru wa kisiasa ninyi Waafrika, mengine yote yataongezwa kwenu na bahati nzuri Afrika yote sasa imekuwa huru. Uhuru umekuja lakini bado Afrika kama Afrika ni Bara maskini tena ni maskini kuliko yote duniani. Lazima tujiulize ni kwa nini kumekuwa na umaskini huu kwa Afrika? Mimi nadhani moja ya majibu ya kwa nini tumekuwa kwenye hali

ngumu Afrika nzima ya weusi ni kwa sababu ya mipango, uchumi na uwezeshaji. Kwa hiyo, ili tuendelee tunahitaji *road map* ya maendeleo, *focus, vision* na hayo yote yatatokana na mipango mizuri, taratibu nzuri za uchumi wetu na uwezeshaji kuwawezesha wananchi na mipango ya makusudi ya kuwawezesha Watanzania. Tutakubaliana katika nchi mbalimbali za Afrika kuvutia wawekezaji, kuvutia *direct foreign investment,* tumekuwa tukitoa masharti ya kushindana kwa urahisi ili wawekezaji waje kwetu zaidi. Kila nchi inashindania kwa kutoa masharti rahisi rahisi na ndiyo malalamiko yetu kwenye madini. Malalamiko makubwa sana ni kutokana na hiyo, ni tatizo la Afrika nzima. *(Makofi)*

Katika kufanya hivyo, wawekezaji hawa hawatuchangii inavyopasa katika mapambano yetu ya kutusaidia kuondokana na huu umaskini. Hili ni tatizo ambalo ni lazima tulitazame na Serikali yetu hapo mwanzo ilishaahidi kwamba, italiangalia ili rasilimali alizotupatia Mwenyezi Mungu, ziweze kutusaidia. Nisitoe mfano wa hapa nyumbani, Nigeria ni nchi ya sita au ya saba kwa kuuza mafuta machafu duniani. Wakishauza mafuta wao nao kwa sehemu kubwa ya mafuta wanayotumia yanakuwa *refined* Ulaya halafu wanayanunua tena kwa mara kumi ya bei kwa kiwango kile kile cha pipa walichowauzia na mafuta yaligunduliwa Nigera mwaka 1948, mpaka leo tatizo lipo pale pale. Nigeria hiajatoa wanasayansi wa kuweza kutengeneza viwanda vya ku-*refine* wakapata *refined petroleum products*. Mpaka leo Nigeria hawajaweza na nchi nyingine za Afrika zilizo nyingi mpaka sasa hatujaweza kwa mfano, sisi tuna dhahabu hatujaweza kuwa na Wahandisi wetu wanaoweza kugundua kwamba, hapa kuna dhahabu na kupima kwamba dhahabu yenyewe iko nyingi kiasi fulani na utaratibu wake wa kuchimba uko hivi, bado hatuna hiyo *capacity*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili tuendelee tuondokane na umaskini huu, lazima tuelekee huko. Tukitegemea Wazungu waje wagundue, wewe umekaa wakugundulie kwamba, hapa kuna mali na mali yenyewe ipo kiasi gani na yeye akuchimbie halafu umpe masharti eti ;nusu kwa nusu tugawane itawezekana? Atakupangia anavyotaka, kwa hiyo, tunaanza kwenye unyonge wetu wa kuhakikisha kwamba, tunaimarisha sayansi na teknolojia. Masomo ya hesabu, sayansi na teknolojia, yapewe umuhimu wa kipekee. Wahandisi na wanasayansi wetu wapewe umuhimu wa kipekee. Nalirudia tena hili, kwenye viwanda vingi unakuta Ofisi ya *Engineer* ipo vichochoroni, Maafisa Utawala na nini ndiyo wapo kwenye makapeti. Hatuwezi kusogea ng'o kwa utaratibu huo. Lazima tuwathamini hawa watu, ndiyo walioweza kuendeleza huko kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika*, science and technology* walipwe vizuri, tuwape motisha vijana wetu. Watanzania wangapi wamesoma Ulaya? Wengi na wengine mpo humu. Mmesoma darasa moja na Wazungu tena mlikuwa mkifanya vizuri kuliko wao, kwa nini sisi hatufanikiwi kama wao? Lazima tujiulize, tuwape motisha vijana wetu, tuwawezeshe na tuwathamini. Lakini vilevile panahitajika mabadiliko na hapa nitatoa mfano sio wa hapa nyumbani ili nisigongane kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Ndege la Kenya, lilipokuwa linayumbayumba, Serikali kule iliteua Bodi mpya ikampa Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya ku-*hire and fire*. Mwenyekiti wa Bodi cha kwanza alichoanza nacho, alipiga panga

*Chief Executive*. Halafu akamwambia yule mpya aliyechaguliwa sasa tukae tuchague Wakurugenzi. Baadhi wakabaki na baadhi wakapigwa panga. Baada ya hapo wakakaa sasa *Chief Executive* na Bodi ya Wakurugenzi, wakateremka chini mpaka mfagizi. Sasa hivi wote wanaongea lugha moja, kuanzia mfagizi mpaka *Chief Executive,* wanaelewa wanachokifanya, *Kenyan Airways* sasa hivi inafanya vizuri sana.

Sasa huku kuhurumiana kwetu lazima kupungue katika baadhi ya maeneo ambayo tunayo nia ya kweli ya kusonga mbele. Nawapa moyo viongozi wetu katika maeneo muhimu kama hivi tunataka ku-*revive Air Tanzania* huwezi hivi hivi kwa mazoea na wale watu wamekuwepo siku zote, ndiyo wameangusha hilo Shirika, ninaposema hilo Shirika moja natolea mifano na mengine yaliyo mengi. Lazima kuwe na mabadiliko na mabadiliko ni machungu kidogo, lazima twende huko lakini hatuwezi kufika huko bila mipango na uwezeshaji, tunarudi kule kule kwa Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulaya ilianza kupata maendeleo baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, kwa sababu ya kitu kilichokuwa kinaitwa *Marshal Plan*. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunakuomba *plan* ya kuindoa Tanzania hapa ilipo na utupe *time frame* kwamba, ikifika mwaka Fulani, Tanzania itakuwa ni moja ya nchi zilizoendelea. Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ameisifia sana Wizara ya Maliasili na Utalii, kwa kuweka bei halisi kwa wanyama wetu na mimi ni mtaalam wa wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafuata *presidency* kwa sababu wenzangu wengine wamewahi kusema wao ni *consultants*, sasa na mimi najieleza. Natania kidogo, lakini ni kweli kwamba, mimi na Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, tulishiriki katika Kamati Ndogo iliyopitia kwa undani kabisa na kutoa mapendekezo ya mabadiliko makubwa kwenye Sekta ya Wanyamapori.

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa na masikio mawili kusikia na amethubutu kubadilisha, kumbe inawezekana. Sasa wale jamaa wawindaji wale, wanatengeneza kitu kama njama ili uwindaji wa kitalii mwakani usiwe mzuri sana, waoneshe kwamba bei zilizopanda si halali. Ninachomwambia Waziri, hata kama hakuwindwa simba hata mmoja au tembo hata mmoja, kwanza ndiyo watazidi kuzaliana na hakuna nchi hata moja duniani yenye rasilimali ya wanyamapori inayoizidi Tanzania, haipo. Tushikilie pale pale tena ikibidi tuongeze juu kidogo, tumalize huu umaskini wetu kwa rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaja nilitembelea vijijini kule Kongwa, kila nilipoenda wananchi walilalamika sana kuhusiana na masuala ya uchumi. Wanalalamika kwamba, wanachokizalisha wao mahindi, mtama, alizeti, karanga na mazao mengine ya kilimo na hata mifugo yao, bei ni ndogo sana ikilinganishwa na bei hasa za vifaa vya ujenzi; bati, saruji, nondo, misumari na kadhalika. Ni tatizo ambalo linalalamikiwa sana, sasa kwa sababu ninyi ndiyo wachumi wenyewe, hebu litazameni, kwa nini bei zetu za mazao ya kilimo ni ndogo kiasi hicho? Kwa nini wananchi wetu wanakuwa hawamudu kufaidika na ongezeko la ukuaji wa uchumi na wao wanakuwa hawamudu maisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Mipango anaiita Sekta ya Mifugo kuwa Sekta Ndogo? Labda ndiyo maana hatusogei hata sisi wafugaji! Tunaomba sana mwakani iitwe Sekta Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, masharti magumu ya uwezeshaji, kuwawezesha wananchi. Ili mwananchi aweze kukopa zinahitajika *Title Deeds* za nyumba na mashamba, wananchi wetu hawana hizo. Tujitahidi turahisishe upatikanaji wa *Title Deeds* ili Watanzania wawezeshwe. Mikopo na Mifuko mbalimbali kwa mfano, Mifuko ya Pembejeo, Wilaya kama ya Kongwa hakuna mkulima hata mmoja aliyepata chochote kwenye Mfuko wa Pembejeo na Wilaya ya Kongwa, sijui, lakini naamini ndiyo Wilaya yenye matrekta mengi kuliko Wilaya nyingine yoyote Tanzania. Mwulizeni Mheshimiwa Charles N. Keenja, nimewahi kumpeleka wakati ule akiwa Waziri wa Kilimo na juzi Mwenge ulipopita Kongwa, tumewapitisha kijiji kimoja ambacho wananchi pale walio wengi, wanatoka kule kwa Mheshimiwa Naibu Spika, wamehamia huku kwangu, wali-*parade* trekta mpya kwenye kijiji kimoja peke yake juu kidogo ya 20, kati ya 20 na 25, trekta mpya na ni za vijana wadogo wadogo kabisa, lakini ni kwa kuhangaika wao wenyewe. Wizara ya Kilimo imewezesha matrekta mangapi katika Mkoa wa Dodoma? Vijana wenyewe sasa wanakwenda mpaka India wanaleta wanauziana. Sasa Mipango na Uwezeshaji, wezesheni hayo, mimi naamini umaskini huu tunaweza kabisa tukapambana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na narudia tena kusema, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuchangia hoja hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na yenye maelezo ya kina kuhusu mipango ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwenye hotuba ya Waziri kuhusu majukumu makuu yanayoikabili Wizara hii. Kwa ruhusa yako naomba nisome mawili tu: La kwanza, kuchambua na kubuni sera za uchumi jumla, kuratibu na kushughulikia shughuli za kiuchumi pamoja na kuandaa miongozo ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji na kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza taarifa na takwimu za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona majukumu ya Wizara hii kuwa ni magumu sana. Ni magumu kwa sababu Wizara inapanga mipango ya nchi kwa vigezo vya shilingi yetu, inayoyumba kila kukicha na utekelezaji wa mipango hii unafanyika kwenye mazingira yanayotawaliwa na Dola ya Marekani. Sasa hiyo ni kazi kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugumu huu mimi naulinganisha na kazi ya kumfundisha na kumtahini kwa Lugha ya Kiingereza, mtoto wa Kiswahili aliyelelewa katika mazingira ya Kiswahili na anayefikiri kwa Kiswahili, yaani kama sisi. Unamfundisha kwa Kiingereza na unamtahini kwa Kiingereza, naona ndio hiyo kazi. Unapanga kwa shilingi, utekelezaji wake umetawaliwa na Dola! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu nchi yetu sasa hivi kwa mara ya kwanza katika historia ya miaka 46 ya uhuru wetu, inashuhudia kitu kinachoitwa *Dollarization* ya uchumi wetu, yaani utaratibu wa kuitumia Dola ya Marekani kama fedha ya kawaida tu. Pengine nielezee jambo moja ambalo Wabunge wote wanaelewa. Tuna makampuni hapa nchini sasa hivi yana-*quote* bei ya bidhaa zake kwa Dola. Usipokuwa na Dola, unapewa adhabu ya kubadilisha hela yako ya Kitanzania kwa viwango vya juu mno. Maana yake ni kwamba, bwana na wewe unatakiwa uwe na Dola, lakini si makampuni tu, hata Idara za Serikali ikiwemo *TRA*. Pengine wengine hamjazoea hapa, lakini sisi wengine Watanzania tunaotoka Visiwani tumezoea hiyo adha. Tukiingia na magari yasiyotakiwa kuendeshwa hapa Bara yenye ZNZ, tunatozwa ada ya Dola 20 kila mwezi na hili ni tatizo. Tumeliongelea sana hili la ZNZ. Lakini linaonekana ni tatizo kubwa kweli kweli, haliishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani pengine ili liishe haraka, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar nayo ianze kututoza Dola 20, 20 kwa mwezi, tunaoendesha magari yenye T kule Zanzibar. Maana ni vitu vidogo sana hivi vinaendelea, halafu leo tunaongelea Shrikisho la Afrika Mashariki! Hapana, *let us put our house in order first*. Pengine nimeenda pembeni kidogo, tunaongelea Dola hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukumbatiaji huu wa Dola unaofanywa na makampuni na vilevile Idara za Serikali, unafanyika huku kukiwa na kampeni kubwa kweli Duniani hasa kwa Wachumi na Wataalam wa fedha wa nchi za Magharibi. Wanasema nchi maskini kama Tanzania, Mheshimiwa Anne K. Malecela ameongelea hapa kwamba, huu umaskini tunaoitwa kwa kweli huu ni wa kujitakia, lakini wanazichukulia nchi kama zetu kuwa maskini kwamba, tunatakiwa kwa kweli tuachane na sarafu zetu, ila tukumbatie Dola. Tukikumbatia Dola tutaondoa kuyumba kwa fedha yetu *(Monetary and Exchange Rate Instability)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli zimetokea nchi nyingi ambazo zilianza kama Tanzania hivi hivi kukumbatia Dola, kimya kimya. Panama na Equador sasa hivi zimekumbatia Dola, ndio *Legal Tender* nchini mle. Wanaofagilia hiyo hali hawatuelezi madhara ya kutumia Dola katika uchumi. Mimi nafikiri kwa Tanzania, madhara yako wazi ni kule kupoteza utaifa ambao tunauona, tunau-*feel* katika pesa yetu na vilevile uhuru wa maamuzi, kwa sababu sasa maamuzi ya mwisho kwa fedha kama hiyo, yatakuwa siyo ya Wizara ya Fedha, itakuwa ni *Federal Reserve* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, anijibu maswali yangu mawili, tafadhali sana, wakati wa kujumuisha. Moja, wachumi na wataalam wa fedha wanasema, *"Informal Dollarization"* kama inayotokea Tanzania, inatokea pale ambapo mfumko wa bei ni mkubwa, pale ambapo fedha ya nyumbani imepoteza nguvu ya manunuzi *(Purchasing Power)."* Sasa mimi niulize tu, hii *Dollarization* inakuja vipi Tanzania wakati Mheshimiwa Waziri, viwango anavyotueleza vya mfumko wa bei viko chini sana, kati ya 6 na 7. Tatizo ni hizo takwimu unazotupa ama tatizo ni hao wataalam wa fedha na uchumi? Nataka atufundishe kwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, lengo la Serikali yetu ni Dola hatimaye iwe fedha ya nchi kuweza kununulia nyanya, chumvi kwa kutumia Dola kama Panama na Equador.

Kama si hivyo, mbona hatuifanyii marekebisho Sheria ya Fedha ya Kigeni ya Mwaka 1992 *(The Foreign Exchange Act)*. Sheria hiyo imefungua milango wazi kwa mtu kutumia fedha za kigeni hapa *freely*. Mwenye ushahidi tofauti atanieleza, pengine Mheshimiwa Waziri mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kitu kimoja, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, ameongelea sana uwezeshaji wananchi na vyombo kama *SACCOS*. Lakini ninataka tu nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba, Mfumo Maalum wa Ushirika kwa Wajasiriamali wadogo wadogo sana huko chini kwenye *grassroots* kwa jina *Village Community Banks (VICOBA)*, ulianzishwa mwaka 2003 na Kitengo cha Kuondoa Umaskini wakati huo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikatuma wataalam wake Ruvuma na ilitumia zaidi ya shilingi milioni 20 kwenye zoezi hili kuanzisha *VICOBA.* Waziri aliyekuwepo wakati huo, mwenye dhamana hiyo, Mheshimiwa Edger D. Maokola-Majogo, Katibu Mkuu wakati huo, Mheshimiwa Mollel na Mkuu wa Kitengo hicho cha kuondoa umaskini, wakatembelea Vikundi vilivyoanzishwa na wakaridhishwa kwamba ni vikundi imara na muhimu. Lakini toka walipotembelea mwaka 2003, hivyo vikundi vikasahaulika, wala havionekani kwenye hotuba za Waziri. Hili ndilo tatizo kubwa tulilonalo kwenye Serikali yetu, tunaanzisha vitu vizuri, hakuna *follow-up*. Lakini nataka nimpe taarifa leo Mheshimiwa Waziri, vikundi hivyo viliendelezwa kwa ubunifu mkubwa na ushupavu wa binti mmoja mdogo sana kwa jina Devota Mkuwa Likokola, ambaye sasa hivi ni Mbunge wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine tumeenda kuiga Ruvuma, vikundi vimeshamiri. Sisi watu wa kutoka Kyela kwa nini tulikwenda Ruvuma? Tulikwenda Ruvuma kwa sababu *SACCOS* tumeanzisha, lakini tunaona ongezeko la *SACCOS* ni dogo mno. Ukiwahoji wananchi, wanakwambia hapana uwezo wetu ni wa chini mno. Nikagundua *variant* ya *SACCOS* kwa hali ya chini kabisa inaitwa *VICOBA*. Nikaenda Ruvuma.

Tumekwenda Ruvuma tumerudi, katika kipindi cha miezi sita tu, wananchi wa Kyela wananisikia, tunavyo vikundi hivyo vya Ushirika mdogo mdogo zaidi ya 120, ambavyo vina fedha bila msaada wa mtu yeyote wa nje zaidi ya shilingi milioni 300 *NMB*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijafaidika peke yangu, kuna Wabunge wenzangu hapa wamefaidika kimya kimya tu hapa. Mheshimiwa Dr. Shukuru J. Kawambwa, Mbunge wa Bagamoyo, najua watu wote wa Bagamoyo sasa hivi wanatingisha vichwa kwa sababu amefaidika kule na *VICOBA* hivi hivi. Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mbunge wa Vunjo naye amefaidika sana na *VICOBA* hivyo hivyo. Nataka kumwambia Waziri ni vitu vya kuvifuatilia, ndio vitu *positive* ambavyo Serikali yetu imevifanya, lakini hatufanyi *followup*. Mheshimiwa Monica Mbega, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mbunge wa Iringa Mjini naye ana *VICOBA,* Mheshimiwa Joyce M. Masunga, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, wote hao wana Vikundi hivyo vya Ushirika ambavyo vimefanikiwa sana. Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr.

Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, naye hivyo hivyo amefanikiwa sana na Vikundi hivyo vya *VICOBA* ambavyo Mheshimiwa Waziri havitaji kabisa. Lakini *they are even more effective, I can dare say* sasa hivi kwa Wilaya ya Kyela, viko *more effective* hata kupita *SACCOS*, kwangu mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *last but not least*, *the Right Honourable* Edward N. Lowassa, *The Prime Minister,* Monduli kule tumeanza vikundi hivi ili kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada zake za pekee za kuwanyanyua watu wa chini kimaisha na kwa kipato. Kwa hiyo, nilitaka kusema hayo yote ili Mheshimiwa Waziri avitupie jicho vikundi hivyo ambavyo Serikali yenyewe ilivianzisha na aangalie njia ya kuvi-*promote*. Nina uhakika vitasaidia sana kuleta mapinduzi huko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema katika mchango wangu wa maandishi, maana sikutegemea kupewa nafasi ya kuongea, niliongelea suala la ajira ambalo liko chini, vilevile ya Wizara hii. Tulitunga hapa kwa kifupi sana, Sheria ya *Tanzania Investment Act* ya mwaka 1997. Sheria hii pamoja na mambo mengine, inaweka *Immigration quota* kwa makampuni ambayo yanawekeza hapa Tanzania kwamba, Bwana ukianzisha *Economic Activity* yoyote hapa, wageni wanaoajiriwa hapa wasizidi watano. Lakini usimamiaji umekuwa mbovu utafikiri hakuna sheria na mimi hili litanifanya nisiunge mkono hoja hii. Nataka nipate maelezo kutoka kwa Waziri ni kitu gani kinawafanya wageni hapa, tuna sheria ambayo hairuhusu wageni kuwa zaidi ya watano ni kitu gani kinafanya hayo makampuni yanakuwa na wageni zaidi ya 20/25 katika kampuni moja? Huko ndio kuongeza ajira? *(Makofi)*

Nina mifano hai hapa, ninaomba ku-*declare interest*, nilikuwa Mkurugenzi wa *NBC*. Mwaka 2000, *NBC* wamekuwa wana-*benefit* chini ya *investment package* tulizonazo hapa na wakijua kabisa kwamba ni wataalam watano tu *approved* mwaka 2000. Leo hii mwaka 2007, *department* zote za *NBC* zinaongozwa na *South Africans*. Wako 13 na wameomba mwaka huu *extension* na viongozi wetu hapa mta-*approve*.

Mimi leo siliungi mkono hili, mnataka kutuangusha! Watanzania wangapi wenye ujuzi katika *Financial Sector,* tunawakosesha kazi katika hili. Ninamwomba Waziri anipe majibu ya uhakika kabisa ni kitu gani kinatufanya tuwaangushe watu wetu tuliowasomesha kwa shida. Leo hii Mheshimiwa Nimrod E. Mkono hapa anapiga kelele kuhusu hii mikopo kurudishwa, tunasomesha vijana kwa shida sana, lakini wanasoma, wanawekwa pembeni. Pengine hatujui Kiingereza kuwajibu kwamba, bwana muda umefika nenda nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo *NBC* tu, nenda *Mobitel*, wamejaa wazungu. Leo nachukua gazeti, kuna Mzungu amerudishwa *Airport* tena baada ya kuwawaacha *Immigration Officers*, akatoka akaingia mjini. Hii nchi imekuwa ya kila mtu na ndio maana sasa hivi Kariakoo wamejaa mpaka wauza karanga kutoka China. Halafu tunaongea kuongeza ajira kwa Watanzania! *We are not serious.* Mheshimiwa Waziri, naomba hili alijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie hapo kabla sijapigiwa kengele. Asante. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima wa afya na kunijalia kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Nimpongeze Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yote ya Wizara inayoongozwa na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya na wanazoendelea kuzifanya kwa kuandaa Bajeti ya mwaka 2007/2008, Bajeti ambayo imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kutekeleza Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara katika kutekeleza majukumu yake imeendeleza programu ya kuunga mkono wananchi katika kuunga nguvu miradi ya kupunguza umaskini (MKUKUTA), imejitahidi kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo shilingi bilioni 10.5

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara katika programu ya kuongeza kipato kwa wananchi imeweza kuvisaidia vikundi mbalimbali katika Wilaya na Mikoa ya Tanzania Bara na Visiwani. Naiomba Serikali kutokana na nia nzuri kwa wananchi wake katika kipindi hiki cha Bajeti kiwafikirie sana wakulima wa Mwani katika kuwapatia soko ili waongeze kipato kwa sababu kazi wanayoifanya ni kubwa lakini bado kipato chake hakiridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma kinatoa mafunzo mazuri ya muda mrefu na mfupi na kinasomesha wanafunzi wa pande zote mbili za Muungano yaani Tanzania Bara na Visiwani, lakini jambo la kusikitisha chuo hicho hakina mwakilishi kutoka Zanzibar nikiwa na maana kuwa chuo hakina Mzanzibari katika bodi kama ilivyokuwa hapo zamani. Waziri akitoa majumuisho anieleze ni sababu zipi zimefanya nafasi hiyo ifutwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naushauri mfupi kuhusu kuendesha chuo hiki hasa wakati wa usajili wa wanafunzi, nakiomba chuo kufungua ofisi yake Zanzibar itakayoweza kuwafanyia usaili wanafunzi waliopo Zanzibar ili wanafunzi wengi waweze kumudu kujiunga na chuo kwa sababu utaratibu uliopo sasa wa kufuatilia usaili Dar es Salaam na Dodoma kunawafanya wanafunzi wengi kushindwa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wake wote kuandaa Bajeti hii na kutuletea hapa Bungeni tuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kurudisha kampuni ya ndege ya *ATCL* katika milki ya Serikali, wakati Serikali inapanga kubinafsisha

mashirika yake lazima iwe macho na makini sana kwani yapo mashirika yanayogusa usalama wa nchi moja kwa moja hivyo kuyabinafsisha kwa wageni ni kuiweka nchi matatani kwani tunatoa mianya ya nchi kuweza kuingiliwa muda wowote na kufanyiwa hujuma mashirika kama ya ndege, *TAZARA* ni vizuri yakawa chini ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mashirika mengi hapa nchini yakiwa chini ya Serikali Watanzania wengi walikuwa na ajira na hata wanafunzi waliokuwa wanatoka vyuoni walikuwa na uhakika wa kupata ajira kwenye mashirika hayo, Serikali imebinafsisha mashirika hayo bila kuandaa mazingira mazuri na kuwezesha sekta binafsi. Waliochukua mashirika hayo wamekuwa wanapunguza watu kazini na kuajiri watu kutoka nje kuendana na matakwa yao, matokeo yake wasiokuwa na kazi wamekuwa wengi, vijana wamekuwa wakihangaika na hivyo kuwepo na wasomi wamachinga na wazururaji, Serikali ichukue tahadhari wakati wa kubinafsisha mashirika yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwawezesha wajasiriamali wadogo wadogo bado halijawekewa mipango madhubuti, wajasiriamali wamekuwa wanafanya kazi kwa hali ngumu sana, kwanza hawana fedha za kuweza kuendesha shughuli zao pia hawana ujuzi wa kutosha ili kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kutoa elimu kwa wajasiriamali wote, pia iwapatie mikopo kwa masharti nafuu ili waweze kuendesha shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha shilingi bilioni moja zilitolewa na Serikali kwa ajili ya kuwezesha wajasiriamali. Fedha hizi zimepelekwa Benki ya *CRDB* na *NMB*. Hali halisi ni kwamba fedha hizi haziwanufaishi walengwa, masharti yanayotolewa na Benki hizi ni magumu mno na wanaoweza kupata mikopo hii ni matajiri tu wenye uwezo na siyo watu wa chini. Pia Benki imekuwa inawanyima wajasiriamali fedha hizo kwa vigezo kwamba hawajaelimishwa jinsi ya kufuatilia mikopo hiyo. Naomba Waziri alieleze Bunge kuwa iliwaandaa vipi hawa wajasiriamali kabla ya kupeleka hela hizo huko Benki ambapo wameshindwa kuzipata?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuwawezesha wakulima kulima kwa tija, Serikali ina mpango wa kuwakopesha wakulima matrekta kwa kupitia mfuko wa pembejeo, pia kuwapatia ruzuku ya mbolea, wakulima wengi wana kipato kidogo sana hawawezi kuthubutu kuchukua mkopo wa shilingi milioni 45 wa trekta, pia mawakala waliopewa kazi ya kusambaza mbolea kwa wakulima wengi wao wanatoa huduma hizo mikoani na Wilaya. Wananchi wa vijijini wanapata wakati mgumu wa kufuata zana hizo Wilayani na Mikoani. Serikali iangalie utaratibu wa kufikisha pembejeo hizo ngazi za Kata na Vijiji ili kwa kupitishia kwenye vyama vya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera ya idadi ya watu, ni ukweli usiofichika kwamba sasa hivi Serikali haijui idadi ya watu wake kamili, idadi inayotumika ni ya makadirio tu, kutokana na sensa zilizopita na hata hivyo tangu watu walipohesabiwa hadi majibu yanapotolewa watu wengi sana wamekuwa wameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bora Serikali ikapata idadi kamili ya wananchi wake kwa wakati ili kuweza kuweka mipango mizuri ya maendeleo. Pia kutokana na idadi ya watu kuwa kubwa na Serikali kuwa na uwezo mdogo wa kuwahudumia, ni vizuri sasa Serikali ikaweka sheria ya kudhibiti idadi ya watoto kwa familia moja, familia iwe na watoto ambao itawamudu na siyo watoto wengi na kusema kila mtoto anakuja na riziki yake na haswa vijijini wapo wanafamilia wanapata watoto hadi kumi wakati uwezo wao ni mdogo sana. *Government should take social responsibilities by regulating population in order to provide good social services and good life for all people.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali sana wawekezaji waje wawekeze katika mikoa ya nchi yetu, lakini tunakataa wawekezaji kuwekeza kwenye vivutio vya utalii kama kwenye *National Parks* na kwingine kwani tunapenda sana *nature* ya vivutio vya utalii iendelee kubaki pale pale, utajiri Mungu ametupa sisi na vizazi vijavyo.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na ngumu wanayofanya kwa kuhakikisha Watanzania wote wanapata maisha bora, ikizingatiwa Wizara hii ndiyo mhimili wa uchumi wan chi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi nianze kwa kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa vijana wengi nchini na hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam bado hawajashirikishwa ipasavyo kuhusiana na suala la kujiajiri wenyewe na hasa kuhusu MKUKUTA, je, ni hatua gani za dhati za kuwatambua vijana ambao wanakaa vijiweni bila kazi maalumu hali ambayo wakiachiwa wataweza kuzalisha tatizo kubwa ambalo litakuwa ni hatari kwa jamii na Taifa? Je, ni hatua gani za makusudi za kuanzisha mafunzo maalumu kwa vijana hawa (wajasiriamali) na hatimaye kuwajengea viwanda vidogo vidogo kwa kuwapatia udhamini wa Serikali *(government guarantee)?*

Kwa kuwa wataalamu wa kuchambua miradi *(proposal)* katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, wana umuhimu mkubwa na hasa kwa wakati huu kwa maana ile ile ya kuwawezesha vijana na wanawake kwa kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ambao wengi wao wako katika Mkoa wa Dar es Salaam, je, wataalamu hawa muhimu wamejiandaaje katika kuandika *proposal* nyingi zaidi huko duniani (nchi wahisani) kwa lengo la kuwakaribisha wawekezaji kuja nchini kujenga viwanda vidogo vidogo ambavyo vitakuwa maalumu kwa vijana na wanawake, hali hii itatusaidia kuongeza ajira nyingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo msingi wa uchumi wa nchi hii na inalazimika iwe na mkakati wa kuwa na takwimu sahihi na za kina. Jitahada ziongezwe zaidi ili kupata takwimu sahihi; takwimu zilizopo hazina uwiano na hali halisi.Wizara ishirikiane na ofisi za Serikali za Mitaa na wajumbe wa mashina kwa lengo la kupata taarifa sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Wizara hii kwa utendaji wake mzuri. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na kaka yangu Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa jinsi wanavyosimamia kazi. Pia nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa ahueni na kurudi tena hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile nilikuwa safarini sitakuwa na mengi ya kueleza isipokuwa nilipoenda Malawi tarehe 30 Julai, 2007 hadi 1 Agosti, 2007 nimegundua kuwa taarifa za kiuchumi hasa utalii hazipo katika balozi zetu kiasi cha kuwawezesha watendaji wetu kuweza kuvutia watalii na kuwaelekeza fursa zilizopo Tanzania. Aidha, wafanyakazi walionyesha mahitaji ya elimu au semina kuhusu utekelezaji wa *economic diplomacy*. Nadhani hii ni kwa nchi nyingi kwa misingi hiyo naomba nifahamishwe kama tayari utaratibu huo upo au ni lini utafanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa pole Mheshimiwa Naibu Waziri na ninamtakia afya njema. Aidha, naipongeza Wizara na watumishi wote kwa kazi ya kuratibu uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Wizara kwa kuwapatia fedha wazalishaji wa chumvi, naomba kushauri kuwa mradi huu uwe endelevu hadi kuhakikisha kuwa bidhaa yote inayozalishwa imepata soko la uhakika, kupatiwa mashine za kukausha *(citygrex)* mashine kutoka Canada ili kuongeza uzalishaji na kuongeza kipato na kupanua mradi huu katika maeneo yote yanayoweza kuzalisha chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Waziri atupatie taarifa juu ya tathmini ya *TIC* kujua hasa kati ya watu au makampuni yaliyowekeza nchini ni mangapi yaliyotekeleza kwa mujibu wa maombi yao na taarifa ya walioshindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu gani ambao umeanza kuandaliwa wa kuhamisha shughuli zitakazobakia za *PSRC* baada ya Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri uongozi wa *NIC* ubadilishe bodi ili inenepeshwe kabla ya kubinafsishwa kwa utaratibu uliopendekezwa na kamati ya fedha. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwani ndiyo inayotoa dira kwa nchi yetu jinsi gani nchi yetu iendeshwe kiuchumi, Wizara hii ikifanya vibaya katika mipango ya nchi maana yake nchi itakwenda mrama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la uwekezeji, naomba Wizara iwe makini sana katika kuweka dira ya jinsi na wapi pa kuwekeza. Wageni wengi wamekuwa wajanja kwa kuja kuwekeza kwenye madini hali inayopelekea kuwa madini yakiisha nchini uwekezaji nchini utalegalega kwani madini yanafaida kubwa kwao. Ni bora sasa

Serikali iweke mkazo kwa wawekezaji kuwekeza katika sekta zenye tija na kwa wananchi wake mfano kuwekeza kwenye kilimo cha biashara na chakula. Vile vile uwekezaji kwenye miundombinu na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ubinafsishaji liangaliwe upya kwani uzoefu unaonesha kuwa nchi yetu imepata hasara sana katika uuzaji na ubinafsishaji wa mali za nchi. Mfano hai ni kampuni ya *ATCL* ambayo sasa Serikali imeamua kuanza upya kuifufua wakati Serikali ingekuwa mbali mno. Serikali iwe macho katika ubinafsishaji wa mashirika yaliyosalia mfano, *TRC*, *TANESCO* na *NIC*. Hivi karibuni Serikali imeridhia kampuni kutoka India ya *RITES* kuhodhi *TRC,* lakini ni vema Serikali iwe macho yasijetokea yale ya *ATCL.*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni kuwa sifa zipi zimezingatiwa na Serikali itachukua hatua gani ikiwa *RITES* hawatatimiza lengo vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu haina programu maalumu ya mipango, tunayo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA, *Mini Tiger Plan 2020,* MKURABITA na MKUMBITA, kwa maoni yangu naona imekuwa mipango mingi ambayo utekelezaji wake umekuwa hafifu kwa sababu tunatumia programu nyingi badala ya kujikuta kwenye moja au mbili. Hali hii inapelekea Watanzania wasielewe tunafuata dira ipi. Vile vile hawaelewi hiyo mipango ya programu hizo inatekelezwaje?

Mheshumiwa Naibu Spika, naomba Waziri atuelimishe juu ya hilo kwani linachanganya. Mfano, MKURABITA inaonyesha imeshindwa kutoa majibu au matokeo yaliyokusudiwa, utekelezaji wa majaribio haya hautoi picha kamili kwa Mkoa wa Mbeya na Dar es Salaam pekee ila ijitanue zaidi. Je, *evaluation, monitoring* ikoje katika mipango yote hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kukopesha wananchi ni dhana nzuri lakini maandalizi hasa ya bilioni moja kila Mkoa hayakufanywa vizuri kwani hata Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alibainisha Waziri udhaifu uliopo juu ya utoaji wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuzalisha wamachinga zaidi kwa sababu wengi wanachukua mikopo ni watu wasio na mtaji, mikopo hiyo ndiyo mitaji na wala hawana elimu ya ujasiriamali hivyo si rahisi pesa hizo kurudishwa kama ilivyokusudiwa, ukizingatiwa wamachinga na wafanyabiashara ndogo ndogo kama mama lishe hawana maeneo ya biashara kwani wametimuliwa mjini eti kwa sababu wanachafua miji. Kwa nini Serikali isitoe mikopo katika nyanja nyingine mfano kwa wanataaluma kwa nia ya kutoa huduma kwa jamii kuliko ilivyo sasa mikopo imetolewa kwa wachuuzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, wanasheria kama kikundi wakiwezeshwa wanaweza kufungua kampuni ya kutoa huduma za uwakili na msaada mwingine wa heshima kwa wananchi. Vile vile, waliohitimu masomo ya biashara kupewa mikopo na kufungua vituo vya ushauri wa masuala ya biashara, itakuwa faida kwa jamii na vile vile kwa vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasemaje juu ya hili jambo/ushauri huu wa uboreshaji njia za utoaji mikopo? Je, Serikali haina mpango wa kufungua utaratibu wa kufungua Benki ya Biashara ya Wananchi (Taifa) itakayotoa riba nafuu kwa Watanzania maskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango kwa ujumla pamoja na utoaji wa takwimu, mipango mingi ya nchi inaonesha kuna hali ya kukurupuka, mfano ujenzi wa sekondari za kata, majengo yamejengwa lakini hayana vitendea kazi, maabara, vitabu vya kutosha, walimu na nyumba za walimu. Je, kabla ya ujenzi huo hakukuwa na mpango wowote?

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizopo sasa za wanafunzi inaenda sambasamba na idadi ya shule za *form five* na *form six* zilizopo, ili watakaomaliza shule hizo za kata na kujiunga na *form five* na hatimaye *form six*. Kinachosikitisha zaidi ni kwamba wananchi wamechangia ujenzi wa shule hizo lakini hakuna mahali takwimu zinaonesha wananchi wamechangia kiasi gani katika ujenzi wa shule hizo. *Recognition* ni muhimu kwani inatia moyo na kwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi? Tumekuwa tukishuhudia Bungeni Mawaziri wakijipongeza ama kuomba pongezi baada ya utekelezaji wa jukumu lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya ubinafsishaji inapangwa bila kujua jinsi gani wafanyakazi hawakuwepo watalipwa. Mfano wafanyakazi wa kiwanda cha Uvinza, ni miaka nane sasa wafanyakazi 383 waliofanya kazi kabla ya kiwanda hakijabinafsishwa na kuendeshwa na *Nyanza Salts Mines* hawajalipwa mafao yao, Serikali kabla ya kubinafsisha iwalipe wafanyakazi stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *Kigoma Special Economic Zone, secretariate* ya pamoja na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma umeshaandika *concept paper* nzuri sana, naiomba Wizara isaidie utekelezaji wa mkakati huo utakaogharimu shilingi bilioni tatu tu. *Kigoma Special Economic Zone* ni muhimu sana kwani itafungua biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani za Kongo, Burundi, Rwanda na hata Zambia. Vile vile wananchi watajikomboa kiuchumi.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake inayofafanua masuala mbalimbali yanayosimamiwa na Wizara yake, kazi zilizofanyika hadi sasa ni nzuri na zinatoa matumaini kwamba siku itafika ambapo hali za Watanzania zitakuwa nzuri kuliko ilivyo hivi sasa.

Napenda kuipongeza Serikali kwa hatua inazochukua za kuboresha maisha ya Watanzania kupitia mipango yake mbalimbali, kwa wananchi wa Dar es Salaam wakiwamo wakazi wa Jimbo la Ubungo, juhudi na mikakati madhubuti zaidi inahitajika ili kuwafikia, kwa mfano, Serikali ilitenga shilingi bilioni 21 kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo za kilimo. Kwa kuwa wakazi wengi wa Dar es Salaam sio wakulima, hawakufaidika na ruzuku mwaka huu Serikali imetenga shilingi bilioni 19 kwa ajili hiyo

naipongeza Serikali kwa hatua hii yenye lengo la kukuza uzalishaji katika kilimo lakini ni dhahiri kwamba unahitajika mpango tofauti ambao utawawezesha wananchi wa Dar es Salaam kuboresha maisha yao kwa kuongeza uzalishaji katika viwanda vidogo na vya kati na kukuza biashara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, Serikali ilianzisha utaratibu wa kuwapatia wananchi mikopo kupitia *CRDB Bank* na *NMB*. Mikopo hii ingeweza kuwasaidia wakazi wa Dar es Salaam kwa bahati mbaya Mkoa wa Dar es Salaam ulitengewa shilingi bilion 7 sawa na mikoa mingine ya Tanzania Bara kuzingatia ukweli kwamba asilimia 10 ya Watanzania wanaishi Dar es Salaam na nilivyotangulia kusema hawafaidiki na ruzuku inayotolewa kwa pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungetegemea kwamba Mkoa wa Dar es Salaam ungetengewa fedha za mikopo kwa kuzingatia wingi wa wakazi wake, mazingira maalumu ya Jiji la Dar es salaam na ukweli kwamba haupati sehemu ya fedha za ruzuku ya pembejeo na mipango kama *PADEP, DASIP* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba uandaliwe mpango maalumu utakaolenga kuinua hali za maisha za wakazi wa Dar es Salaam hususani kuwawezesha waanzishe viwanda na biashara tusipofanya hivi mapema, umaskini utazidi kukua miongoni mwa wakazi wa Jiji, jambo ambalo litaathiri maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya kuinua hali za maisha ya Watanzania ni nzuri sana na inastahili pongezi, tatizo kubwa ni kwamba mipango iliyopo haijaweka utaratibu wa kumfikia mlengwa na kuiwezesha kufaidika na mipango hii haitoshi kutoa ruzuku ya mbolea kwa mfano inabidi kuhakikisha kwamba mkulima ana shamba lenye ukubwa wa kumwezesha kuzalisha mazao mengi kumwezesha kuondokana na umaskini, inabidi pia kuhakikisha kwamba unapata utalaamu na mahitaji yote mengine ya kilimo na kwamba kunakuwepo usimamizi wa kuhakikisha kwamba anafanikiwa. Mipango ya jumla na ya Kitaifa inaweza isiwe wa manufaa yanayokusudiwa. Naunga mkono.

**MHE. DANIEL. N. NSWANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, hata hivyo ningependa kuuliza maswali madogo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Mkoa wa Kigoma na hasa Kasulu itaingizwa katika programu ya *(SELF)* katika hizo Wilaya 83 zilizonufaika (ukurasa wa 15 wa hotuba) ambapo shilingi bilioni 10.5 zilitumika, napenda kujua mgawanyo wake ukoje kwa kila Wilaya? Kuhusu elimu kwa umma inayotolewa na mashirika ya *SELF, IGP* ni lini yataelekezwa katika Mkoa ulio nyuma kama Kigoma na hasa Wilaya ya Kasulu yenye wakazi zaidi ya 700,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kusomesha wataalamu wa Kitanzania wenye vipaji maalumu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali *(EO Scholarship Fund)* ukurasa wa 31 wa hotuba. Hadi sasa ni Watanzania wangapi na wa kada gani wamepata mafunzo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wataalamu hao wako wapi Wizarani, *Private Sector*, Halmashauri au  Sekretarieti za Mikoa? Napenda kupata ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwa ziada ya yale niliyoyasema hapa Bungeni.

Kwa nini *EWURA* bado inashindwa kudhibiti mafuta na bei yake? Hivi ni suala la kisheria? Je, *Fair Trade* inafanyika au tumeachia iwe *Free Trade?*

Mheshimiwa Naibu Spika, je, kwa nini tusiandae mkakati wa kuwaombea *sponsorship,* vijana wetu kama wanavyopewa wengine wa vyuo vikuu; mipango huwezi kuikwepa katika maendeleo ya nchi hii na ipewe uzito unaostahili sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mipango endelevu ya wananchi kuwezeshwa kiuchumi kwa ku-*float* hisa kwa sekta mbalimbali kama walivyofanya *NMB*; na makampuni mengi, je, kwa nini mabenki mengine yasifanye hivyo? Je, kwa nini hata makampuni ya simu yasifanye hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Waziri anaweza kutuambia nini azma ya baadaye ya *Dar es Salaam Stock Exchange* kwa sasa haionekani ikitekeleza majukumu yake kutokana na uwezo wake kidogo kifedha na kutokana na kutokuwa na mtandao nchi nzima. Taasisi hii ingepewa msukumo ili iwe na chachu ya kusaidia maendeleo ya mipango yetu bila kusubiri misaada toka nje kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri afuatilie suala la kuwapatia vijana ardhi nje ya Dar es Salaam kwa hiari yao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi suala la *investment facilitation committee* kwa nini halifanyi majukumu yake ya kusimamia masuala yote yenye uhaba katika *investment* mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa *investors* wanapokuja walazimike kuwapa stahili ya wananchi haki zao. *Shares* (hisa) ziwe wazi na zisiwe kama geresha. Naunga mkono hoja hii.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi kwa hotuba nzuri ya Wizara kwa kuwa imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa kuboresha maisha ya wananchi ni pamoja na Wizara hiyo kusimamia suala la fedha za mkopo kwa kila Mkoa zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fedha hizo zikitolewa kwa mikoa kwa kutumia utaratibu wa benki za *CRDB* na *NMB*, wananchi wa Mkoa wa Kigoma walijikuta wakiambiwa kuwa fedha zimekwisha kabla hawajapata fedha hizo. Aidha, napenda

kueleza tu kuwa wakati fedha hizo zikitolewa na benki zilizochaguliwa ilizingatiwa mikoa ya Pwani tu wakati mikoa ya Bara imejikuta haikupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia hoja ya kuimarisha mafunzo kwenye Chuo cha Mipango ili kuweza kuwa na watalaamu ambao baada ya kumaliza masomo watakwenda kufanya kazi Mikoani na Wilayani ambako ndiko wananchi wanalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maafisa mipango walio wengi hapa nchini hawana uwezo mzuri wa kusimamia mipango kama maelekezo ya Wizara yalivyo, ni vyema kwa makusudi mazima hawa watu wapewe mafunzo ili wafanye kazi kama maelekezo yanavyotolewa na Wizara. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama jina la Wizara linavyojieleza, Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, ningependa kujua Wizara imewezesha Watanzania wangapi kutoka kwenye dimbwi la umaskini kwa kupitia mpango wa MKUKUTA na MKURABITA?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa kipaumbele na hata upendeleo kwa wawekezaji toka nje ya nchi badala ya Watanzania je, Wizara yako haioni sasa ni wakati wa kuwapa Watanzania kipaumbele na upendeleo maalumu kama wafanyavyo *South Africa?*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni watalaamu wachache sana wanashiriki kikamilifu katika ukuzaji uchumi wa nchi. Makampuni mengi ni ya kigeni hata pale ambapo Watanzania wanapaswa kushiriki kwa mujibu wa sheria wanakuwepo kama kusindikiza tu. Tanzania kama hatutajipanga hatuwezi kufaidi chochote kutokana na raslimali zetu nyingi kama madini, gesi na hata kama tutapata mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iwashirikishe Watanzania wawe na hisa siyo chini ya 40%. Nchi yoyote haiwezi kujengwa na watu wa nje.

Mheshimwa Naibu Spika, jimbo la Vunjo lina vikundi 40 vya *VICOBA* yaani *Village Community Bank,* vikundi hivi wanakopeshana wenyewe na kuweka hisa, tayari wana zaidi ya mikoa 30 Benki ya *NMB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara yake inipe utaratibu wa kuwawezesha wafikie lengo la kuanzisha Benki pamoja na kutuletea wataalamu wa kutoa mafunzo ya ujasiriamali. Lengo ni kuwa na *Community Bank* ifikapo mwaka 2010.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ya Mheshimiwa Dr. Alhaji Juma Ngasongwa, napenda nimpongeze sana kwa jinsi alivyo mahiri kwa utoaji wa hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika pia natoa pole sana kwa Naibu Waziri kwa ugonjwa uliompata na sasa amerejea Bungeni na akiwa na afya njema, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, pole sana na karibu tena Bungeni.

Napenda kuwapongeza pia Katibu Mkuu Balozi Charles Mutalemwa na Naibu Katibu wake Bibi Joyce Mapunjo, wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu uko kwenye mpango wa miundombinu katika uwezeshaji, mipango ifanywe vizuri katika upande wa barabara ya reli na umeme wa gridi hasa maeneo yenye uchumi wa kutosha, mfano eneo la Mkoa na Mchuchuma katika Mkoa wa Iringa/ Ruvuma, maeneo hayo ni muhimu sana kwani huko kuna makaa ya mawe na chuma. Serikali ikiweka mipango mizuri nchi hii itakuwa na utajiri wa kutosha baada ya kufanya uchambuzi yakinifu. Pia maeneo ya Mtwara na Lindi ambako kuna gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mipango mingine ni kuangalia na kufanya utafiti wa nishati mbadala katika utoaji wa umeme badala ya mafuta na maji. Tuone uwezekano wa kutafuta mwekezaji wa ndani na nje wa kutumia nishati ya upepo pale Makambako Mkoa wa Iringa kuna nguvu kubwa sana ya upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Dodoma kiimarishwe sana kwa kuwa na wakufunzi wa kutosha na wenye utaalamu, maslahi yao yaboreshwe kwenye mishahara, usafiri na mikopo ya nyumba na magari. Pia suala la kukaimu kwa *Principal* wa pale lisichukuliwe muda mrefu kwani wataalamu wapo wa kutosha, Chuo kiwe na *Principal* siyo kukaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi na mpango wake wa kuanzisha shahada ya kwanza katika maendeleo ya fedha na mpango uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Mungu ibariki Wizara, Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka maelezo kuhusu fursa iliyotolewa na China ya shilingi bilioni tano za Afrika, ni miradi ipi iliyoombwa na uthibitisho kuwa maombi yamepelekwa, nina wasiwasi sana na uzembe wa baadhi ya watendaji kutokuwa na changamoto au kushabikia fursa kama hizi, viongozi wa nchi nyingi wamepeleka maombi ya miradi mbalimbali kwenye kipindi muafaka, kwa nini sisi tumechelewa na vigezo vya kuibua miradi hii hufanywa na nani?

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya majukumu makubwa ya Wizara hii ni kuweka mazingira bora ili kuwezesha sekta

binafsi kushamiri na pamoja na mambo mengine kuongeza ajira. Wakati tunakipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa kuwa *aggressive* katika kutafuta wawekezaji, nalazimika kuelezea kutoridhishwa kwangu na usimamizi wa shughuli za kiuchumi hasa zilizo mikononi mwa wawekezaji wageni.

Tarehe 9 Septemba 1997, Rais Mstaafu Benjamin Mkapa, alisaini Muswada wa Uwekezaji na kuwa Sheria Namba 26 ya mwaka 1997 yenye *short title*: *Tanzania/Investmeny Act, 1977*. Sheria hii pamoja na mambo mengine inaweka *Immigration Quote* ya watumishi wa kigeni hadi watano katika kipindi cha mwanzo cha mwekezaji.

Kifungu hicho cha 24 cha sheria hiyo linaongeza kuwa kila ongezeko la mfanyakazi mgeni ndani ya *Immigration Quote* lazima liridhiwe na kituo cha uwekezaji kwa kushirikiana na uhamiaji. Lengo Kuu la Bunge katika sheria hii, lilikuwa ni kuona idadi ya wageni ikipungua kadri muda unavyokwenda ila pale tu ambapo kuna teknolojia mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kuona kuwa katika eneo hili, *TIC* imeshindwa kabisa kudhibiti hali hii licha ya kuwa na madaraka chini ya sheria, tuna makampuni mengi ya kigeni yaliyowekeza nchini ambapo idadi ya watumishi wageni inazidi kuongezeka badala ya kupungua tena nje ya *immigration quote!* Mfano, mwaka 2000, *NBC Ltd.*, ilianza na *expatriates* watano, leo hii wako 13 wakiongoza idara zote za kibenki na zisizo za kibenki, *NBC* wala haina *succession plan* kwa waswahili kushiriki katika menejimenti ya benki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri anieleze ni kitu gani cha ajabu sana kwa Serikali yenye hisa 30% katika Benki hiyo kuruhusu wageni waajiriwa kuongezeka na huku wataalamu wa Benki wazalendo wanazeeka kwenye nafasi za ukarani tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, *NBC* ni moja tu ya makampuni kadhaa, ikiwemo *Mobitel* yenye idadi kubwa ya wageni kinyume cha sheria ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaunga mkono hoja hii mpaka nipate maelezo ya kina.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dr. Alhaj Juma Ngasongwa pamoja na Naibu Waziri wake, pongezi pia kwa Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya kuwawezesha wananchi kupitia shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa inaendelea. Hata hivyo inakabiliwa na matatizo kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bado masharti ya Benki ni magumu kwa walengwa na hasa urasimu uliopo. Walengwa walitazamiwa kuwa ni wananchi wa kipato cha chini, lakini wengi wao hawatafaidika na wale wenye nacho ndiyo wanaofaidika. Wananchi wa

vijijini hawajapata mikopo hii ikilinganisha na wenzao wa mijini, ipo hatari wananchi hawa wakakosa mikopo kama Serikali haitachukua hatua za makusudi za kuwezesha wananchi vijijini kupata mikopo hii kwani wanadai hawana mtandao wa kufanya kazi hadi vijijini.

Kuhusu *SACCOS* bado ni tatizo hasa Jimboni kwangu kwani kata nyingi na vijiji havina *SACCOS* kwa kuwa Halmashauri yangu haina watumishi wa kutosha yaani maafisa ushirika ambao watasaidia kuunda vyama vya ushirika/*SACCOS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikubaliani na mtazamo wa mabenki kuwa hata *RC* hatakiwi kujua maendeleo ya mikopo eti ni siri. *RC* ni kiongozi wa ngazi ya juu mkoani hivyo anastahili kufuatilia na kujua maendeleo ya mikopo Mkoani kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilieleza masikitiko yangu kuhusu Posta kwamba suala hilo limekuwa la muda mrefu, Serikali iliahidi kulikamilisha mapema lakini hadi sasa shirika hili litatatuliwa matatizo yake ya msingi. Ikiwa ni tatizo la mtaji, madeni yatokanayo na *EAPTC,* pia pensheni za watumishi wake kwa kuwa madeni yalikwisha hakikiwa na hazina mwaka jana, je, posta itafutiwa lini madeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa kuirejesha *ATCL* kwa Watanzania, hata hivyo *seriousness* ya Serikali kufufua *ATCL* bado haionekani.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kuipongeza Wizara hii kuwa dira ya uchumi na uwezeshaji. Kwa kuwa haiwezekani kukuza uchumi bila mikakati ya kupunguza umaskini, ni muhimu kwa Wizara hii kutambua na kujua tatizo linaloikabili nchi na kukusanya takwimu, kufanya uchambuzi na tafiti mbalimbali na hatimaye kutoa elimu kwa Wizara mbalimbali na hatimaye wananchi kwa ujumla. Ili mikakati ya uchumi ifikiwe ni afadhali kutoa elimu kwa maafisa mipango Wilayani nao wafike kwenye kata na vijiji kuelezea mipango ya kupunguza umaskini, bila umaskini kupungua, uchumi hautakuwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa mkopo wa kuwawezesha wajasiriamali kupata mikopo ili kupunguza makali ya umaskini ni wazo zuri sana. Lakini kwa Wilaya zingine imekuwa kama historia. Maeneo mengine wamekwisha maliza shilingi bilioni moja, maeneo mengine hawakupata. Napenda kusema kuna upendeleo mkubwa kwenye mkopo huu, kwanza kutoa elimu kwa *SACCOS* kuna Wilaya ambazo hawakupata, hivyo hawatarajii kupata mkopo kienyeji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwaacha baadhi ya wananchi bila kufaidika na mkopo huu na kuendelea kutoa mkopo kwa maeneo mengine ni hatari kubwa kwani ni kuongeza tofauti kubwa kati ya walionacho na wasionacho. Napenda kutoa ushauri ili kupunguza umaskini ni muhimu kuwa na masoko ya kuuzia mazao, ni afadhali kuongeza na viwanda kwa ajili ya kuuzia mazao yao, kwa mfano kujenga viwanda kwenye maeneo yanayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza ya mkopo imeonekana kwamba kuna masharti magumu ukilinganisha na uwezo wa *SACCOS* za mijini na za vijijini, naomba masharti hayo yapunguzwe. Kuna changamoto nyingi ambazo zinastahili kuangaliwa kama Waziri alizoeleza kwenye ukurasa wa 19 hadi 20. Changamoto hizo ni uelewa mdogo wa wananchi kuhusu dhana ya mikopo, vitendea kazi kwa wajasiriamali, upungufu wa maafisa wa mikopo kwenye wilaya, kata na vijiji na ukosefu wa matawi ya mabenki katika baadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali isaidie kukabiliana na changamoto hizo ili fedha hizi ziweze kuzunguka na kukopeshwa wananchi wengine wanaosubiri kukopa. Napenda kutoa taarifa kwamba Wilaya ya Longido ni miongoni mwa Wilaya ambazo hazijapata mikopo. Serikali sasa waangalie hizo changamoto kwani ndiyo kikwazo cha wananchi kutopata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MOHAMMED A. ABDULAZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana na hotuba ya Waziri, ukurasa wa 13 aya ya 18 kuhusu mkataba wa utafiti wa upandaji wa miti ya karatasi katika mikoa ya Lindi na Mtwara. Habari hii ni faraja kubwa kwa wananchi wa mikoa hiyo miwili ambayo ilifikia hatua ya kudhani kuwa Serikali imetusahau wananchi wa mikoa hiyo.

Sasa hivi tuna imani kubwa na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kuwa imedhamiria kwa dhati kueneza maendeleo katika maeneo yote ya nchi yetu. Aidha, ziara ya majuzi ya Mheshimiwa Waziri ya kutembelea mkoa wa Mtwara na mwekezaji mwenye dhamira ya kujenga kiwanda cha simenti huko Mtwara tunafurahishwa na kuridhika sana na jitihada hizi za Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi zangu kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Kituo cha Uwekezaji hapa nchini, taarifa zinazopatikana kwa wawekezaji mbalimbali zinaonesha kuridhishwa na huduma zitolewazo na kituo. Hii inatujengea sifa nzuri na sifa nzuri hizo nazo pia ni kivutio kwa uwekezaji, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, malalamiko ya rushwa na ucheleweshaji wa kushughulikia maombi ya wateja hivi sasa yamepungua sana na hii ni sifa nzuri, tunaomba Serikali ikisaidie kituo kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Wizara iongeze kasi katika mchakato wa utengenezaji wa kanuni za biashara *(Bussiness Activities Registration Act).* Naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Alhaji Juma Alifa Ngasongwa, na pia nitumie fursa hii kumtakia afya

njema Waziri, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, baada ya kupona kutokana na kuugua. Nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuchangia kwa ufupi hasa kwa Wizara hii nyeti na mhimili wa Taifa letu kiuchumi na mipango mizima ya Serikali. Wizara hii ni nyeti, mategemeo ya Wizara hii kwa nyanja zote za Serikali ni makubwa. Wizara hii ikiandaa mipango mizuri basi kila Wizara itafanya kazi vizuri na uhakika na hivyo hatua ya mipango ya Serikali kumgusa kila mwananchi itafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado napata taabu ya kuamini idadi ya watendaji waliopo katika Wizara hii kama kweli wametosheleza kiutendaji. Ni muhimu sasa Wizara kuwa na watendaji wa kutosha tena waliobobea katika masuala mbalimbali kuwa na watafiti *(Researchers)* ili mipango na mikakati ya kukuza uchumi wetu iende kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara isimamie kwa karibu taasisi ilizozianzisha kwa nia ya kuunga mkono nguvu ya wananchi katika kupanguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo *(Small Enterprenuers, Loan Facility - SELF)* ni kwa kiwango gani imewafikia wananchi, kwa nini *SELF* haipo Iramba? Sasa ni wakati muafaka ije Iramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu programu ya kuongeza kipato *(Income Generation Programme)* ni kwa nini iwe katika mikoa michache tu? Tunaomba Waziri atueleze ana mpango gani wa kuipanua programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikakati ya MKURABITA MKUKUTA, MKUMBITA, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Mkakati ni mzuri sana bado elimu kwa wananchi kufahamu haijafahamika vizuri, naomba Wizara itafute utaratibu mzuri ili kutoa elimu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itafute utaratibu mzuri wa fedha za uwezeshaji, maarufu kama Mfuko wa JK. Urasimu na utaratibu katika Wilaya nyingi sio mzuri na hivyo ulisababisha wananchi kushindwa kujipatia mikopo hii nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI ABDI H. MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wa Wizara kwa hotuba nzuri na naunga mkono hoja. Naomba ufafanuzi kuhusu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi malengo ya Ilani ya CCM ya 2006 – 2010 ambayo ni *specific* kisekta yatafikiwa kwa uhakika kwa kila Kijiji, Kata, Wilaya, Mkoa na Taifa bila kuwepo mkakati wa mpango wa miaka mitano *(five year indicative plan)?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa uwezeshaji, badala ya kuzigawa kimkoa je, isingekuwa vyema zaidi kuzigawa Kiwilaya kwa kutumia *factor* ya idadi ya watu ili kupata mgao sawia nchi nzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina mkakati gani wa kuwezesha iwepo hali *(regime)* ya mikopo ya muda mrefu na riba ya *digit* mbili kwa wajasiriamali wananchi ili kuongeza kasi ya uwekezaji wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itaweka viwango vya ubia *(Minimum Local Participation)* kisheria kwa miradi inayoanzishwa na wageni?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiw Dr. Alhaji Juma Ngasongwa, kwa kuwasilisha vizuri hotuba ya Bajeti yake. Napenda pia kumpa pole Naibu Waziri wake Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa ndwele. Aidha, nawapongeza Mawaziri hao na watendaji wa Wizara kwa kusimamia vizuri sera za uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mmoja tu nao ni kuwa Chuo cha Takwimu cha Afrika Mashariki kilichopo Changanyikeni Dar es Salaam ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa, hivyo Serikali kupitia Wizara hii naomba ikipe kipaumbele. Aidha, naomba *diploma* zinazotolewa na chuo hicho zitambuliwe na vyuo vikuu vyetu. Utaratibu ufanywe ama watoe shahada au vyuo vyetu kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wawape nafasi ya kuingia mwaka wa pili Chuo Kikuu kama wanavyofanya *Makerere University.*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani chuo chetu cha takwimu kitambuliwe na *Makerere University* kwa kuwadahili wanafunzi wanaomaliza chuoni hapo mwaka wa pili huku sisi wenyewe tukitaka waanze mwaka wa kwanza. Ni vyema utaratibu au mazungumzo kati ya Wizara (mmiliki wa Chuo) na uongozi wa vyuo vyetu vikuu hasa *University of Dar es Salaam* ili kukipa hadhi inayofanana na Chuo cha Makerere, kwani ile Kamisheni ya Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki si ipo na kushughulikia vyuo vyote vya Afrika Mashariki. Sasa kwa nini Tanzania isithamini chuo hiki kama wafanyavyo jirani zetu wa Uganda.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ya Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008. Hata hivyo nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji wa shamba namba 208 la *NAFCO* Magamba, Mbozi. Shamba hilo liliwekwa chini ya *PSRC (specified)* kwa ajili ya kubinafsishwa tangu mwaka 1996. Shamba hilo limeshatangazwa mara kadhaa ili libinafsishwe, lakini hadi naandika mchango huu hakuna kinachoeleweka. Mwaka jana katika nyakati tofauti kwa kupitia michango yangu hapa Bungeni, niliomba Serikali isitishe mpango wake wa kubinafsisha shamba hilo ili badala yake wananchi

wanaolizunguka shamba hilo na ambao wengi wao walihamishiwa katika maeneo yao ili kupisha uanzishwaji wa shamba hilo wapewe mashamba hayo kwa kuuziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika kusema kwamba majibu ya Serikali katika swala hili yamekuwa ya kukatisha tamaa sana. Sasa naomba kujua je, bado Serikali inasimamia kauli zake za nyuma za kubinafsisha shamba hilo kwa watu wengine au taasisi nyingine nje ya Wilaya na hivyo kuwanyima wananchi ambao wanalizunguka shamba hilo na ambao wengi wanakabiliwa na shida kubwa ya ardhi? Kama Serikali inashikilia msimamo wake huo, ni lini sasa shamba hilo litapata mwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kulikuwa na sababu gani za kuwazuia wananchi hao kuendelea kulima mashamba hayo kwa utaratibu wa kukodisha kama walivyozoea kwa kisingizio cha kumkabidhi mwekezaji ambaye mpaka leo hayupo? Ningependa pia kujua mwekezaji atakayepewa shamba hilo atalinunua kwa kiasi gani cha fedha? Na je, kiasi hicho ni kwa faida au hasara? Je, kama mwekezaji atapewa, anategemewa kuzalisha tani ngapi za mahindi kwa mwaka na Serikali inategemewa ipate kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mgao uliotolewa na Serikali wa shilingi bilioni moja kwa kila mkoa, tayari Mkoa wa Mbeya umeshatumia kiasi chote cha fedha ambacho kilitengwa, na kwa kuwa bado wananchi wa mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbozi bado wana ari ya kuendelea kukopa; sasa je, wananchi hawa waendelee kusubiri hadi lini? Kwa kuwa inaonekana wananchi wa baadhi ya mikoa bado hawajatumia mikopo hiyo kwa kiasi kikubwa, je, isingekuwa busara kuzielekeza fedha hizo katika Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Mbozi ili wananchi hao waendelee kukopa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuibinafsisha Mamlaka ya Reli ya Uhuru - *TAZARA* bado kwa sehemu kubwa limebaki kitendawili kikubwa sana. Suala hilo lilianza kuzungumzwa kwa zaidi ya miaka kumi sasa lakini hakuna mkakati wowote wa maana. Mashamba mengi yamebinafsishwa lakini *TAZARA* bado, kulikoni? Naomba sasa Waziri atueleze mpango kamili au ratiba inayoonyesha ubinafsishaji wa shirika hilo muhimu katika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo moja kubwa tulilonalo katika nchi hii ni kuwa na vipaumbele vingi sana ambavyo utekelezaji wake hauonekani kwa urahisi na wala siyo endelevu *(sustainable)*. Lakini pia na ufuatiliaji wake unakuwa mgumu sana. Hivyo napenda kushauri kwamba ni vizuri tuwe na vipaumbele vichache ambavyo utekelezaji wake utaenda sambamba na uwezo wa Serikali kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeshauri twende kwa utaratibu wa kufanya jambo moja au machache, kuyamaliza na kuhamia maeneo mengine *(elimination system)*. Nchi nyingi duniani zinatumia utaratibu huu na zinafanikiwa sana. Tukumbuke usemi usemao, *if you want to do everything at a time, you will end up doing nothing*. Natumaini nimeeleweka. Ahsante.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu

Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na wataalamu wake wote wa Wizara hii na taasisi zake zote kwa hotuba nzuri na kazi nzuri kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara kwa jitihada zake za kupanga, kusimamia na kuratibu maendeleo ya uchumi wa Taifa letu pamoja na kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hata hivyo bado ipo haja kubwa kwa Wizara kuongeza usimamizi, uamshaji na ufuatiliaji wa shughuli zake mbalimbali na pamoja na kuona kwamba Wizara imeona umuhimu wa suala hili muhimu kama ilivyoelezwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi lipewe umakini zaidi. Kwanza kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa elimu na ufahamu wa kutosha kuhusu programu mbalimbali zilizopo ili waweze kufaidika na hatimaye kuishi maisha bora na kujikwamua kiuchumi kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu mbalimbali unakwenda kwa kasi ya ganzi na urasimu mkubwa sana. Mifano hai ni *TASAF* ina urasimu mrefu mno. MKUKUTA na MKURABITA ni programu zinazotekelezwa kwa kasi ya kinyonga. Pamoja na jitihada za MKUMBITA*,* bado urasimu bandarini na kwenye forodha za mipakani na viwanja vya ndege kuna vizuizi vingi sana na hivyo kuleta kero kubwa kwa wananchi na hasara kwa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shilingi bilioni 21 kwa ajili ya wajasiriamali hazipatikani kwa urahisi kufuatia elimu ndogo kwa wananchi na urasimu mkubwa unaotumiwa na benki katika kukopesha *SACCOS,* benki za wananchi na wajasiriamali. Ipo haja kubwa ya kuboresha utekelezaji wa mipango maalumu kama vile *Mini Tiger, SEZ* na *EPZ*. Mpaka sasa utekelezaji upo nyuma ya matarajio.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masikitiko makubwa kwamba pamoja na mipango kuashiria kuwepo *SEZ* na *EPZ* katika mkoa wa Tanga, bado hapajawa na dalili ya hayo kufanyika mkoani Tanga katika miaka hii ya karibuni. Ipo haja ya kuwepo Muswada *(Draft)* wenye vigezo mahsusi kwa mikataba mbalimbali na wawekezaji katika sekta mbalimbali ili Tanzania ifaidike ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pawepo utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kwamba ubinafsishaji unaleta manufaa kwa Taifa na wananchi na pia wale ambao ubinafsishaji umewapatia fursa za kuviendesha viwanda, migodi na shughuli mbalimbali ambazo zimebinafsishwa kwao zinaendeshwa kama inavyostahili, kwa faida ya wao na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja na kuitakia Wizara na asasi zake utekelezaji mwema.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri ya kuandaa, kusimamia shughuli zote za Wizara. Aidha, natoa pole kwa familia ya

Mheshimiwa John Magufuli, Mheshimiwa Samuel Sitta kwa kuondokewa na mzazi na mjomba, Bwana alitoa na Bwana ametwaa, jina la bwana libarikiwe. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza mradi wa *TASAF II* Bukombe kutokana na mradi huu tunategemea kukamilisha ujenzi wa hosteli tisa katika sekondari zetu kati ya sekondari ishirini. Pamoja na pongezi hizi yapo matatizo ya lini mafundi kulipwa hela? Mwananchi yuko Bukombe Vijijini ili alipwe ni lazima afuatwe mkaguzi anayekaa Shinyanga. Utaratibu huu unasababisha urasimu unaochelewesha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ifanye yafuatayo, ilete mkaguzi wa mradi huu Bukombe, kwani kasi tuliyonayo isije ikakatisha tamaa wananchi. Naomba Serikali kwa kuwa mgawo wetu umekwisha waangalie uwezekano wa kutusaidia fedha nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la *SELF,* naomba Serikali ili wajasiriamali wetu wafaidi naomba *SELF* ifanye huduma zake mkoani Shinyanga kwani tuna imani na utendaji kazi wao, pamoja na nia na lengo lao la kuwawezesha kiuchumi wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anapohitimisha hoja yake anieleze ni lini *SELF* itaanza kufanya kazi mkoa wa Shinyanga na Wilaya ya Bukombe? Pia anieleze kwa nini mashirika kama haya yanachukua muda mrefu sana kuyafikia maeneo ya Kanda ya ziwa hususan mkoa wa Shinyanga?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali katika Bajeti ijayo mikoa itakayopewa vipaumbele katika sekta mbalimbali, mkoa wa Shinyanga usisahauliwe. Nasema hivyo kwa sababu katika Bajeti hii ya mwaka 2007/2008 upande wa barabara mikoa sita iliyopewa vipaumbele Shinyanga haimo, hii si hali nzuri kwa sababu barabara nyingi hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Bukombe yenye barabara zenye urefu zaidi ya kilometa 450 ni kilometa takribani 158 tu ndizo hupitika, zingine hakuna; iweje maeneo kama haya yasitiliwe umuhimu katika kupanga vipaumbele vya Serikali Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo naomba nimkumbushie Mheshimiwa Waziri masuala yangu yanayohitaji majibu/ufafanuzi wakati wa hitimisho lake, mkaguzi wa mradi wa *TASAF II* anayekaa Shinyanga na kuhudumia mkoa wote na Nzega anasababisha ucheleweshaji wa malipo kwa mafundi, kwa nini wasiongee au kila Wilaya awepo au kukasimu madaraka kwenye Serikali ya Wilaya kuondoa usumbufu kwa fundi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawo wetu wa Bajeti ya *TASAF II* inawezekana umekwisha. Je, Serikali iko tayari kutuongeza mgawo mwingine kwa sababu wananchi wameitikia mwito wa kuibua miradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mradi wa *SELF* haupo mkoani Shinyanga na Wilaya ya Bukombe? Ni lini utaanza kazi kule ili Watanzania wote wanufaike na maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Waziri atoe majibu ya hoja zangu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kati ya Wizara muhimu katika ukuaji wa uchumi wetu. Pia ina jukumu la kubuni sera, kuendeleza uwekezaji katika nchi yetu. Pia inahusika na masuala ya takwimu, kuleta maendeleo ya nchi nzima na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika,Wizara hii ni lazima iwe na takwimu sahihi katika ngazi zote kuanzia vijijini hadi Taifa. Kuwepo pia na ukusanyaji wa taarifa sahihi, uchambuzi na matokeo ya uchambuzi huo yafanyiwe kazi. Kama hii ingefanyika sahihi tusingekuwa kama tunashitukizwa kwa mfano ujenzi wa shule za sekondari. Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ingekuwa tayari imewajulisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni wanafunzi wangapi wanaotegemewa kuingia sekondari ili kuwa na mpango mzuri wa kujenga madarasa, kuwepo na maabara yenye vifaa, pia kuwa na walimu wa kutosha. Siyo kama ilivyo, inaelekea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi haikuwa na takwimu sahihi pamoja na kuwa na mpango wa *Mini Tiger Plan 2020*. Swali je, ule Mpango wa Maendeleo ya Taifa ndani ya miaka mitano, mitano umeishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kujitahidi iwezekanavyo kutafuta wawekezaji nchini, lakini hapa inabidi tumsaidie Mheshimiwa Rais ili wawekezaji hawa wasijekuwa matapeli wa kuzoa fedha zetu na kuzipeleka nje ya nchi. Kwa mfano mwekezaji anayekuja kuwekeza katika utalii *(Tours operator)* kabla hajawekeza inabidi aende *TIC,* apewe masharti ya uwekezaji mfano katika sekta hii mwekezaji anahitajika alete nchini *USD 500,000* na anunue magari kumi mapya apeleke na *write-up* ya *project* yake. Cha kusikitisha wawekezaji hawa hawafuati masharti haya kwa sababu hakuna wafuatiliaji. Walifika *TIC* wakishalipa ile *fees USD 500* wanapewa *certificate* wanaenda *TRA* wanapewa *Tax exceiption,* wanaanza biashara.

Napenda kutoa ushauri ufuatao, *TIC* na *TRA* washirikiane, wawekezaji hawa wasipewe *licence* mpaka fedha zionekane nchini na magari yawekewe masharti yote yatimizwe ndio wapewe *licence*. Mfano ile hoteli iliyoungua Arusha karibu na *Airport (Ritz)* mwekezaji kutoka *South Africa* alikuja akakopa hapa hapa akajenga hoteli yenye makuti akaachwa, akaondoka. Je, fedha zile alizokopa zilisharudishwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuangalie vizuri wakati wa ubinafsishaji kama una faida na Taifa letu. Wizara hii ilitakiwa ijue *South Africa* katika ubia ilioingia na nchi yoyote kwenye *Airline* haijawahi kufanikiwa. Kwani Wizara ilikuwa haijafanya utafiti na kuona haya hadi kufanya *ATCL* kufikia hapo ilipo? Hata ubinafsishaji wa *NBC Ltd.* (Benki ya Biashara) kwa mtazamo wangu mimi isingebinafsishwa kabisa sababu ilikuwa ni benki pekee iliyowajali walalahoi, ilishaendeleza shughuli za *Micro Finance*

lakini benki zilizobakia haziwajali watu hawa wa chini, ndio inapelekea watu kuhimizwa kujiunga na *SACCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri tubinafsishe biashara tu na majengo yabaki dhamana *(collateral)* ya Serikali kwa sababu wawekezaji wanauza yale majengo wanapata *working capital* na wanatumia fedha zile zile zetu badala ya kuingiza/kupata *(FDI)* inakuwa hatuingizi fedha za kigeni za kutosha. Hivyo wakati tunabinafsisha *National Insurance Corperation (NIC)* tuwe makini katika hili, tujali maslahi ya Taifa mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko ya uchumi duniani utandawazi *(globalization)* ndio neno la kila leo katika nchi nyingi na Tanzania ni nchi mojawapo inabidi tuingie kwenye utandawazi sababu hatuwezi kuwa kisiwa peke yetu bila kuwa-*join*. Ninavyoamini mimi utandawazi ni mfumo wa kibepari na sisi Tanzania tupo katika mfumo wa ujamaa na kujitegemea. Sasa sielewi utandawazi huu wa ubepari na yaliyopo katika Katiba yetu. Tukumbuke Tanzania zamani tulisema ubepari ni unyama, leo hii tusemaje? Hivi huo usemi upo tena au umepotea?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maswali, ni mikoa mingapi ina wataalamu wa Takwimu? Je, katika ubinafsishaji ni nani anayefuatilia kama masharti yametimizwa/*monitoring/evaluating* na kucheki *assets* zilizobinafsishwa?

Je, sababu ya utandawazi Tanzania tunafuata ubepari au ujamaa na kujitegemea au naomba ufafanuzi *(globalization)* utandawazi unafuata siasa ipi, ubepari au ujamaa na kujitegemea? Kwa nini takwimu za kujenga shule kwa nguvu za wananchi hazionyeshwi kwenye *budget* wananchi walichangia kiasi gani badala yake zinaonekana fedha za kigeni tu? Je, ule mpango wa maendeleo ya Taifa wa miaka mitano, mitano umeishia wapi?

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa kwa kazi nzuri anazosimamia za uchumi na uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ndiyo dira ya Wizara zote, hivyo nashauri wataalamu wa mipango wawe wazalendo katika kuinua uchumi wa nchi yetu na kupanga mipango inayotekelezeka kwa kufuata Ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, neno uwezeshaji ni pana, tunaomba Mheshimiwa Waziri watoe elimu ya kutosha juu ya kuwawezesha Watanzania. Wananchi wengi hawajui watawezeshwaje kwa kupewa mitaji, kwa kukopeshwa au kivipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie Chuo cha Mipango, Dodoma. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutoa fedha za ujenzi wa maktaba na bweni, ujenzi huu unaendelea vizuri sana. Nina ombi, kwanza, Mkuu wa Chuo sasa athibitishwe, amekaimu muda mrefu sana na kazi zake ni nzuri sana, pili, fedha ziongezwe zaidi katika ujenzi wa mabweni mengine maana wanafunzi wa *Diploma I* na *II* wako mitaani. Mazingira ya kusoma si mazuri, mantiki ya elimu hawataipata vizuri maana jioni wanakusanyika na watu wa tabia mbalimbali na tatu, Wizara ilete mkakati mpya wa

kuongeza vyuo vingine vya mipango, wajenge chuo kingine, tusitegemee chuo kimoja tu cha Dodoma, kama kweli tunataka tupate wachumi na wanamipango wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anifikishie salaam kwa Naibu Waziri Mheshimiwa Gaudence Kayombo, ambaye alikuwa India kwa matibabu. Namwombea kwa Mungu apone. Nashukuru leo yupo Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya naunga mkono hoja hii, Mheshimiwa Waziri apewe pesa zote bila mabadiliko.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango maalumu wa kuboresha maendeleo Tanzania, utekelezaji huu wa ndani na nje kwa miundombinu ya wawekezaji hairidhishi na bado haiendani na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na sera zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara hii kupitia Mheshimiwa Dr. Alhaj Juma Ngasongwa, ndio Serikali yaweza kurekebisha kwenda na wakati na awamu ya Serikali ya Nne. Naiomba Serikali kuzidi kuweka Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUKUTA) na ufuatiliaji na utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira nchini mwetu kwa wananchi bado tuko nyuma ya ufinyu, kwa hiyo, Serikali itilie mkazo mabenki ya *CRDB, NMB* na mabenki mengine kutoa mikopo kuwezesha wananchi kujiajiri wenyewe. Miradi inayoleta maendeleo mijini na vijijini kama *TASAF, PADEP, ADSP* na kadhalika, maandalizi yazidi ili miradi hii iwe inaleta tija na wanaotupa waone tunatumia inavyotakikana, Serikali isimamie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta binafsi, naomba zipewe nguvu na mipango Serikalini, miundombinu na kupatiwa uwezeshwaji wa viwanja, mikopo, ili waweze kufikia malengo kwa faida ya Taifa letu. Pia kuzingatia Tanzania ni ya Serikali mbili za Muungano kwa hiyo, maslahi yawe sawa Tanzania Bara na Zanzibar (Visiwani) na Mheshimiwa Dr. Alhaji Juma Ngasongwa, anafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake yote. Maoni yangu ni kwamba pamoja na mikakati mizuri ya Serikali ya kutaka kujenga uchumi imara ili kuboresha maisha ya wananchi, bado kuna haja ya kuongeza nguvu katika kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue uamuzi wa makusudi wa kuwawezesha wananchi (wazawa) ili waweze kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi yao. Mipango ya MKUKUTA, MKURABITA na MKUMBITA itafanya kazi vizuri kama taasisi za fedha zitakuwa tayari kutoa mikopo kwa wananchi ambao tayari wana ubunifu na nia ya kuingia katika mfumo mzima wa kuchangia kukua kwa uchumi wetu. Tusiache mpango huu uwe kwa watu wachache tu, tutachelewa kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ianze utaratibu wa kutawanya maendeleo katika nchi nzima na sio Dar es Salaam peke yake ambako kunaonekana kumejaa na pia itapunguza tofauti ya maendeleo kati ya mkoa na mkoa. Naunga mkono hoja.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mimi nina maombi mawili tu; ni lini Serikali itafikiria kushawishi mwekezaji katika zao la matunda? Nchi yetu ina matunda mengi, kwa mfano Lushoto, Geita, Tabora, Morogoro, Ukerewe na Biharamulo. Kwa kifupi naomba jitihada zifanyike ili kuwe na kiwanda cha kuzalisha *juice* kutokana na matunda yetu. Geita matunda ni mengi sana kwani hayana pa kuyauza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kiwanda cha kusindika *juice* Wilayani Geita. Nina hakika kiwanda hiki kitaingiza pesa nyingi na kitawezesha wananchi kuzalisha matunda yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri aishauri Wizara ya Nishati na Madini ipeleke umeme maeneo yanayozalisha, siyo tu kupeleka ili mradi inapeleka umeme popote. Naomba kuwe na mpango wa kupeleka umeme machimbo ya Rwangasa, Nyangusu na Katoro. Umeme huu utalipa na utasaidia kuwezesha wananchi na kuleta pesa za kigeni. Naomba majibu na naunga mkono hoja.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza uundwaji wa *Singida Special Development Corridor.* Mpango huu utaiwezesha Singida kama mkoa wa kati na wa mapito makuu *(transit center)* kupaa kiuchumi. Mipango ya Serikali kujenga barabara za lami Singida - Arusha, Singida - Mwanza, Singida - Dodoma na Singida - Mbeya, itafanya *transit commerce* kupitia Singida *(interstate commerce)* kukuza Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa.Singida chini ya mpango huu itapata kuvutia uwekezaji katika maeneo yafuatayo:- utalii wa ndani na nje; ujenzi wa *Agro Processing Industries* hasa mazao ya asili kama asali, ufuta na kilimo na mifugo; madini na uchunguzi wa mafuta na gesi; sekta ya mabenki (fedha) kwa ajili ya ku-*finance transit commerce;* usafiri wa anga; bandari kavu na *human resource development (investing in people, capacities, education and training).*Naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya 18, ukurasa wa 13 wa kitabu cha hotuba kuna maelezo kuhusu utafiti katika maeneo yanayofaa kupandwa miti ya kutengeneza karatasi na *woodchips* katika mikoa ya Lindi na Mtwara, nashauri katika vijiji sita na maeneo yaliyoainishwa tathmini ya mazingira ya kina *(EIA)* ifanywe ili kuainisha athari nyingine zinazoweza kujitokeza licha ya unyonyaji maji, kabla ya utekelezaji upandaji miti.

Katika kifungu cha 27, ukurasa wa 19 kumeainishwa changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Licha ya changamoto hizo kuna zile ambazo Wilaya za pembezoni kama Ludewa, changamoto nyingine zilikuwa ni pamoja na kuchelewa kupeleka maofisa mikopo kwenye mabenki ya mbali. Hata walipopelekewa mikopo ilisimamishwa lakini afisa mikopo aliyeletwa alikuwa hana uzoefu. Nilitegemea maafisa

wenye uzoefu wangepelekwa kwanza maeneo ya pembezoni na siyo kuanzia mijini na kusahau maeneo ya pembezoni.

Katika kifungu cha 34, ukurasa wa 24 wa kitabu cha Bajeti, kituo kilihamasisha wananchi wa mikoa ya Ruvuma, Mara na Rukwa kuwekeza katika fursa zilizopo ndani ya mikoa hii. Kwa vile katika mkoa wa Iringa hususan Wilaya ya Ludewa kuna mipango ya kuanza kwa migodi ya Mchuchuma na Liganga ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vya kuyeyusha chumvi Liganga. Naomba uhamasishaji uliofanyika mikoa ya Ruvuma, Mara na Rukwa sasa uhamie mkoa wa Iringa hususan Wilaya ya Ludewa ili wananchi waanze kujiandaa ili wafaidi zaidi kutokana na migodi hii.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Waheshimiwa Wabunge, walipofika wale Wabunge wa Ethiopia, katika kitu walichoshangaa sana Tanzania ni jinsi tulivyoweza kuchukua Dola mahali popote wakati wowote, walishangaa kabisa nilikuwa nao. Kwa hiyo, nadhani tuko tofauti kidogo. Sasa nitamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, aweze kuanza kujibu hoja hizi, atachukua dakika kumi kutokana na afya yake si nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nizungumzie kuhusu hoja ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako kama unavyoelewa sikuwepo hapa Bungeni kwa muda mrefu. Ningependa kutoa maneno ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ningependa kuwapeni salaam za kutoka kwa wafanyakazi wa Ubalozi nchini India, ambao wanafanya kazi nzuri sana pamoja na kuhudumia wagonjwa wanaokwenda kule. Nilipofika India nilikuta wagonjwa 15 na mimi nikawa wa 16. *(Makofi)*

Pili, niliporejea Tanzania, nilipofungua Televisheni, nilikusikia Naibu Spika, ukitaja majina ya Wachezaji wa Timu ya Bunge watakaopambana na *NSSF* na timu hii ilishinda, napenda kuchukua muda huu kuwapongeza pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Viongozi wetu wa nchi, Mheshimiwa Rais, pamoja na Mama Salma Kikwete, waliokuja kunitembelea pale Hospitalini, pamoja na Waziri Mkuu na Mama Regina Lowassa, ambao pia walifika pale Hospitalini, pamoja na kwamba muda wao katika kazi kwa kweli ni mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kuniponya, lakini pia ninashukuru kwa kuugua kwa sababu nilikuwa sijui kama nchi hii inapenda watu wake kwa kiasi hicho mpaka ambapo niliugua, nikakuta mapenzi ya Watanzania ni makubwa sana. Nilipokwenda nchini India nilifikiri nitakuwa peke yangu kwa sababu tu ni Naibu Waziri, lakini nilikuta Watanzania ambao wamepelekwa na Serikali, wengine ni wafanyabiashara binafsi, wengine ni wafanyakazi wa chini sana kutoka Wizara

mbalimbali kuanzia Jeshi, Wizara ya Afya na Wizara nyingine. Nikagundua kwamba, matatizo hutufundisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi kubwa inayofanya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uhai wa Watanzania. Napenda pia kumshukuru mke wangu, ambaye alinisindikiza huko India kwa kazi kubwa aliyoifanya. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kwa kuhakikisha kwamba, familia yangu inaendelea vizuri na kwa kuhakikisha anaongea na wapiga kura kule Mbinga wawe katika hali ambayo siyo ya hatari, ya kuona kwamba, Mbunge wao sasa amepotea. Namshukuru sana Mheshimiwa John Komba. Lakini, pia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa sala zenu, kwa kunitembelea na kwa kunitakia mema kila wakati na hata nilipofika hapa na kwa wingi wa makofi ambao umeonekana sasa hivi. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naondoka pia kulikuwa na kongamano la Roho Mtakatifu kwa wale Wakristo kule Dar es Salaam na hapa Dodoma. Walipopata taarifa za ugonjwa wangu, waliomba na kusali sana. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana, kwa sala zao na sala zenu, Mungu amejibu na mnaniona hapa niko timamu. Kwa namna ya pekee pia napenda kuwashukuru wapigakura wa Jimbo la Mbinga Mashariki, kwa uvumilivu wao na kupitia muda huu, napenda kuwaarifu kwamba nimerejea na niko salama na nitawatumikia kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nirejee kwenye hoja ya Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Kwanza, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao mizuri sana. Napenda niwahakikishie kwamba, michango hii imechukuliwa kwa umakini wake na itazingatiwa si tu katika kujibu maswali kama atakavyojibu mtoa hoja, lakini cha muhimu zaidi katika utendaji wa kazi za kila siku katika Wizara katika kutimiza malengo yake yaliyoainishwa kama ambavyo imesomwa leo asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia jambo moja ambalo limeelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi, nalo ni juu ya uanzishwaji wa Benki za Wananchi *(Community Banks)*. Jambo hili ni muhimu sana katika uchumi wetu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mlivyosema. Sheria zetu zinaruhusu uanzishwaji wa benki hizi na sera iliyoko ni kwamba, wananchi wenyewe wanabaini tatizo na wanaandaa mipango ya kuweza kuanzisha benki hizi kama ambavyo Mikoa mingine kama vile Ruvuma katika Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Iringa, Mkoa wa Kagera na Mkoa wa Kilimanjaro. Ninazo taarifa Mkoa wa Mtwara pia kwa Wilaya ya Nanyumbu wako katika hatua ya mbali kidogo katika kuanzisha Benki ya Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kuwaomba na kuwasihi Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo hatua mbalimbali tumezichukua kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge wa Mbinga Vijijini, anahamasisha wananchi kuanzisha kiwanda

cha mbolea, vivyo hivyo tunaweza tukahamasisha wananchi kama vile ambavyo tumehamasisha wananchi kuanzisha *SACCOS* kwa wingi sana.

**NAIBU SPIKA:** Mbeya Vijijini, siyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Mbeya Vijijini.

**NAIBU SPIKA:** *Okay*, siyo Mbinga.

**NAIBU WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukachukua nafasi zetu kama Wabunge na mimi namshukuru Mungu, nikiangalia *CV* za Wabunge katika kila Mkoa, zimechanganyika, zimesheheni uwingi wa taaluma mbalimbali. Tunaweza tukahamasisha wananchi kuanzisha Benki hizi maadamu Serikali sasa imeshaweka mazingira mazuri na sheria ambayo tumepitisha mwaka jana ya kuanzisha hizi Benki za Wananchi, basi na tuanze kufanya hivyo, kwa sababu Sheria na Sera zinaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba na mimi niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yao waliyotoa hapa Bungeni. Tumeandaa majibu marefu sana, hatuwezi kuyafikia. Kwa hiyo, tutajitahidi kadri ya uwezo wetu, lakini kama kawaida yetu, baadaye tutaandaa majibu mazuri zaidi ili Waheshimiwa Wabunge, waweze kugawiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo ada yetu hapa Bungeni, naomba niwataje wafuatao ambao wamechangia hoja hii hapa Bungeni kwa kuzungumza, nao ni 14. Wa kwanza ni Mheshimiwa Adam K. Malima - Makamu Mwenyekiti Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto – Msemaji Mkuu wa Upinzani, Mipango na Uchumi, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Sameer I. Lotto, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, ambaye namshukuru sana kwanza kwa kutoa salaam za kutupongeza wote kufuatia afya yake, lakini kubwa zaidi ni kwamba, amepata nguvu na amerudi, maana nilikuwa peke yangu hapa, nimepata nguvu na namtakia aendelee kuwa na afya njema. Tulikuwa tunafuatilia sana afya yake alipokuwa India kwa kupiga simu, alikuwa anaendelea vizuri na tunashukuru sana kwamba, amepata afya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa njia ya maandishi, hao nao wako 31. Tunaanza na Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Janeth M.

Massaburi, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Mhonga S. Ruwanya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Michael L. Laizer, Mheshimiwa Mohammed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Juma H. Killimbah na Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu. Wote hawa ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Sasa maelezo, kama nilivyosema ni hoja nyingi, haiwezekani tukapata muda wa kuyaeleza yote, lakini labda tuanze kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu kasi ya utekelezaji wa Mpango Maalum wa kuharakisha maendeleo nchini, kwa lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwa kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji na kujenga miundombinu inayovutia wawekezaji kuwa ndogo. Ni kweli kwamba, Mpango huu ambao tunauita *Mini-Tiger Plan 2020,* shabaha yake ni kuharakisha maendeleo ya nchi yetu. Shabaha hii bado iko, tatizo tulilopata ni la uhaba wa fedha. Kwa mfano, lile eneo tunaliita la Benjamin William Mkapa, *Special Economic Zone* tungeliweza kulimaliza mwaka jana, yaani mwaka wa fedha uliopita. Lakini kwa sababu ya uhaba wa fedha, tumeshindwa na pale kitu kinachotucheleweshа mpaka sasa ni kuweka kituo cha umeme, maana pale tumeshapata maombi 13 kama nilivyosema kwenye hotuba. Maombi 13 ya kujenga viwanda, lakini huwezi kujenga viwanda kama huna umeme wa kujitegemea katika eneo la *Special Economic Zone*. Fedha hizi sasa tumezipata, ndio tunaendelea nazo kujenga ili tukamilishe na ndio maana nikasema tutakamilisha mwaka huu wa fedha wa 2007/2008. Hivyo, hoja ya msingi hapa si kwamba kuna uzembe, hapana. Hoja ya msingi hapa ni kwamba, upungufu wa fedha ndio unafanya mradi huu uchelewe.

Lakini hapo hapo labda niongeze kusema, ule Mpango wa *Special Economic Zone* ulisema tutaanza kwanza na Mabibo, Dar es Salaam, halafu tutakwenda Tanga, Kigoma na Mtwara. Yote haya kutegemeana na upatikanaji wa fedha na sehemu kadhaa nyingine tutazifikia, mradi tu tupate fedha. Sasa mwaka huu wa fedha tumepata milioni 600, kwa ajii ya kuanzisha *Special Economic Zone* ya Kigoma. Tungetaka tupate zaidi, lakini ndio uwezo wetu. Kwa hiyo, tutakwenda na huo kwanza. Lakini vilevile tunatafuta uwezekano wa kuianza *Special Economic Zone* ama ya Bagamoyo, ama ya Tanga, ambazo zote ziko katika mipango yetu. Kwa hiyo, hapa hoja ni pesa tu, siyo jambo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Kighoma A. K. Malima, alizungumzia suala la majukumu ya Wizara ya kuratibu mikakati ya uchumi kwamba, inahitajika tuwe na uwezo wa kitaalam *(Capacity Building)*. Naliunga mkono suala hili, lakini *Capacity Building* ni jambo ambalo si la kulimalizia. Ukilianza, unaendelea nalo

kwa sababu ni *(process),* mchakato. Lakini kwa sasa hivi Wizara ina uwezo mkubwa wa kusimamia miradi yetu na kuipanga.

Kitu cha msingi hapa ni ya kwamba, tutaendelea kuimarisha uwezo wa mafunzo kwa ajili ya watalaam wetu. Kwa mfano, kuna watalaam wetu wanapata *attachment* kwenye taasisi mbalimbali za utafiti wa kiuchumi ndani ya nchi na nje ya nchi kwa mfano, kuna baadhi ya watalaam wamepata fursa ya kukaa na *REPOA* na *ESRF,* kwa ajili ya kupata mafunzo. Pia watalaam wetu wamekwenda mpaka kwenye Chuo cha Benki ya Dunia, vilevile *IFM* na pia kwenda kwenye *Micro-Economic Finance Management Institute,* kwa ajili ya kuongeza utalaam wao. Lakini vilevile tumekuwa tukipata *technical assistance* ambazo pia imesaidia kuboresha kiwango cha utaalam katika watumishi walioko Wizarani. Vilevile tafiti nyingi zinazofanyika na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, zinafuata utaratibu wa viwango na ubora unatambulika Kitaifa na Kimataifa na ndiyo maana kiko Kitengo katika Ofisi ya Takwimu kinachoitwa *Statistical Methods, Standards and Coordination Unit.* Kitengo hiki hakipitwi na vitengo vingine katika nchi zetu za Afrika ni kitengo kizuri na kinafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, kitaallam watu wetu wanajitahidi.

Kuna hoja nyingine ya masharti magumu ya Benki ya *NMB* na *CRDB,* kuna ukweli, lakini vilevile kuna ukweli kwamba, masharti yanayotumika kukopesha hizi fedha za uwezeshaji ni nafuu zaidi kuliko zile za kwao na hii inatokana na kukubaliana na Serikali kuhusu masharti nafuu ambayo yanaweza kutumika katika kukopesha wananchi hao. Ndiyo maana nimesema pale mwanzo katika hotuba kwamba, karibu asilimia 82 ya fedha ambazo zilikuwa zimetengwa zimekopeshwa na marejesho kwa zile fedha ambazo zinatazamia kurejeshwa ni asilimia 95. Kwa hiyo, kazi hii inakwenda vizuri. Tunapenda tuongeze kasi na tutaongeza kasi. Ndiyo maana katika awamu ya pili ya mpango huu, tutatumia zaidi benki nyingine tofauti na *CRDB* na *NMB,* kwa kupeleka kwenye benki nyingine ambazo zitateuliwa, Serikali na vyombo vingine vya fedha baada ya kutambuliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Suala la *Community Bank* limeshajibiwa. Fedha za mikopo za uwezeshaji zigawanywe katika miradi ya uzalishaji kilimo. Hili nalo halina matatizo, tunaliunga mkono na ndiyo shabaha yetu kwamba, pale hasa maeneo ya vijijini fedha hizi ziende katika sekta ya kilimo, uvuvi na sekta ya ufugaji. Kwa hiyo, hili halina matatizo.

Elimu ya ujasiriamali itolewe na hili nalo tunalitoa, kabla ya kuanzisha mradi huu, tuliwafundisha pale Wilayani maofisa watatu mpaka wane, sehemu nyingine mpaka watano, maafisa ambao shabaha yetu waende kuelezea namna na kuongoza ugawaji wa hizi fedha katika mikopo na kutoa mikopo katika kutumia fedha hizi. Kwa hiyo, hili jambo tumelifanya, lakini vilevile lazima viongozi tuendelee na sisi kuhamasisha. Mimi nakumbuka wakati tunazungumzia suala hili la fedha, shilingi bilioni 21, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema, kwake kule kulikuwa na tatizo la *SACCOS,* lakini tukakubaliana kwamba, kila mahali ambako kuna matatizo ya *SACCOS,* tuzianzishe na kweli tumezianzisha na kuna taarifa nzuri kuonesha kwamba, *SACCOS* hizi ziko na zimeanza kunufaika. Tutaendelea kuhimiza na katika hili niseme kwamba, vikoba hatukuvipuuza kwa sababu pale tunazungumza ushirika, ushirika una sehemu nyingi, *SACCOS* ni

ushirika maalum kwa sababu ni wa kuweka na kukopa. Lakini hatukupuuza ushirika wowote. Ushirika wa wafugaji, ushirika wa wakulima, ushirika wa wafanyabiashara, ushirika wa viwanda vidogo, wote tumewatilia mkazo waweze kupata *access* ya mikopo hii. Kwa hiyo, hakuna ushirika wowote uliodharauliwa.

Halafu ubinafsishaji wa mashirika yaliyosalia ya *TRC, TANESCO* na *NIC,* ambayo nayo yabinafsishwe kwa uangalifu. Hili tunalikubali na ndiyo tumekuwa tukisema hivyo, tutakuwa waangalifu sana kubinafsisha mashirika haya na ndiyo maana kwa mfano, Shirika la Reli hatulibinafsishi kwa maana ya kubinafsisha, bali tunabinafisha kwa kukodisha. Yule mkodishaji anachangia asilimia 51 na sisi Serikali asilimia 49. Hisa hizi zote zimeshalipwa na mtu wa kwanza kulipa hisa hizo ni sisi Serikali, kuonesha kwamba sisi tuna *commitment* ya kuboresha huduma za reli nchini. Sasa wenzetu wa *Right of India* nao wameshatoa mchango na kwa hiyo, sasa hivi tunakidhi masharti ya Benki ya Dunia ya kutukopesha Dola za Kimarekani milioni 44, ambazo zitasaidia kukarabati reli. Hivi ninavyosema, wataalam wa India wapo tayari nchini, wanafanya tathmini mbalimbali, pamoja na tathmini ya kukarabati reli yetu hasa katika sehemu ianziayo Dar es Salaam mpaka Dodoma na sehemu ya kipande cha Itigi, kwa lengo la kuwezesha kurudisha huduma ya reli nchini, kwa sababu bila reli kama tunavyokubaliana ni tatizo. Kwa hiyo, hili suala halipuuzwi na Serikali hii tumejizatiti kulishughulikia kikamilifu.

Halafu maandalizi yanayofanywa na *TASAF II* ya kuandaa uratibu wa kupima mafanikio ya mradi wa kuhusisha wadau mbalimbali ukamilishwe. Hili nalikubali, kazi hii imeshaanza, tumefikia mahali pazuri tukikamilisha taarifa hizi zitatoka. Kwa nini tunafanya tathmini hiyo kwa sababu kwanza ni matakwa ya mkataba wetu na hawa wahisani wetu wa *World Bank,* kwa hiyo, lazima tufanye tathmini. Lakini ya pili sisi wenyewe tunataka tujue matokeo ya utekelezaji wa mradi huu, ambao umeleta manufaa makubwa katika jamii nchini mwetu.

Kazi za MKURABITA, kweli zinachelewa lakini hazichelewi kwa jeuri, zinachelewa kwa sababu ya uhaba wa fedha. Mradi ule unategemea sana fedha kutoka Norway. Kwa hiyo, kila zinapopatikana, tunazitumia na ndiyo sasa tunaendelea na Mkoa wa Dar es Salaam na Mbeya, kazi hii inafanyika na mimi nina hakika tukijitahidi hivyo tutaendelea kutekeleza vizuri.

Dhana ya kuendeleza na kukarabati miundombinu ni ya kipaumbele, hili nimeshajibu. Kwa kweli tunaweka kipaumbele katika kukarabati reli hii. Suala la kubinafsisha *NIC* hili nalo liko katika hatua nzuri tunaendelea vizuri na mimi nina hakika katika miezi mitatu mpaka sita ijayo, suala hili litakuwa limekamilika. Suala hili lazima tukubaliane kwamba, biashara ya bima ni ngumu kwa sababu pamoja na kwamba, wananchi wanachangia fedha zao na zinashikwa na Shirika la Bima lakini Bima kuna majengo. Kwa hiyo, katika kubinafsisha Shirika la Bima, lazima tuwe waangalifu, namna gani ya kufanya maana biashara ile kama hakuna fedha unafanyaje. Kwa hiyo, majengo yale ni *asset* mojawapo muhimu katika suala zima la kubinafsisha na naomba hili tulitazame kwa uangalifu namna hii.

Kuhusu elimu ya ujasiriamali itolewe kuhamasisha wananchi hususan vijijini ili kupata mkopo na kulipa. Hili pia alilizungumza Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, tunalikubali na ndiyo maana nimesema pale, tumechukua hatua ya kulishughulikia katika ngazi ya Wilaya. Lakini pia ni muhimu viongozi wote tushiriki katika kuwaelimisha wananchi ili kuwahamasisha waweze kuelewa nini malengo ya Mfuko huu na nini malengo ya elimu ya ujasiriamali ili tuweze wote kuwahamasisha wananchi wetu kwa pamoja.

Suala la tathmini kwa rasilimali tulizokuwa nazo Mchuchuma, Liganga, *Gas* na pia Mheshimiwa Anne K. Malecela, amezungumzia suala la wanyamapori, utalii, bandari, madini yote haya yanafanyika. Hakuna mtu anayeyapuuza, ndiyo maana tuna chombo kinachoitwa Shirika la Maendeleo ya Taifa *National Development Cooperation (NDC), i*kiwa ina tathmini rasilimali hii ya taifa na kuziuza ili wenye uwezo waweze kuja kuwekeza katika sekta hizi. Sasa hivi tumefikia mahali pazuri sana, kwa sababu tumekubaliana Serikali pale tumtafute mshauri ambaye akishauri namna ya kuboresha kutekeleza miradi mikubwa. Miradi hii inahitajika fedha nyingi, sisi kama Serikali hatuna fedha hizo. La pili, sisi tumejitoa katika biashara kwa hiyo, lazima sasa kazi hii ifanywe ama na wananchi wenye uwezo au ifanywe na watu wa kutoka nje ambao wana uwezo.

Kuna ufinyu wa bajeti katika Chuo cha Mipango. Ni kweli Serikali nzima kuna ufinyu wa bajeti kwa kila idara. Lakini hapa tumejitahidi kweli, ndiyo maana nikazungumzia juu ya ujenzi wa maktaba, nikazungumzia juu ya ujenzi wa majengo ya taaluma, pia nikazungumzia juu ya ujenzi wa majengo mengine kwa ajili ya kuimarisha chuo. Kwa hiyo, jambo hili halikupuuzwa lakini kwa kuzingatia uwezo wetu wa fedha ndiyo tunatekeleza majukumu yetu.

La mwisho, kuhusu hili ni kukifanya chuo hiki kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Mimi nadhani ilitolewa tayari maelezo hapa kwamba, vipo aina za vyuo tunavihitaji, chuo hiki ni cha *middle cadre technicians*. Sasa mkiwaondoa na hiki ni chuo kimoja katika nchi, mkikiondoa hiki mkifanye Chuo Kikuu, hii kada ambayo inakwenda Wilayani, inayokwenda kwenye Tarafa na Kata hutaipata. Mimi naomba kada hii ibakie kufundishwa katika Chuo hiki cha Mipango. *(Makofi)*

Halafu kwamba Wizara itoe idadi ya mashirika ambayo yamebinafsishwa na idadi ya ajira zinazotengenezwa kutokana na ubinafsishaji uliofanywa. Kwanza, idadi ya mashirika yaliyobinafsisha nilishasema. Mashirika 336 na mali za mashirika, makampuni 660 yamebinafsishwa mpaka leo. Ajira za watu kwa sasa hatuwezi kuzitoa kwa sababu hizi zinahitaji utafiti kidogo. Hii tutaifanya kwa kuzingatia ile taarifa yetu tunayofanya. Sasa hivi tumeanzisha taarifa ya *PSRC* kumaliza muda wake na *PSRC* inamaliza muda wake Desemba mwaka huu. Kwa hiyo, taarifa ile tumeanza kuiandaa, taarifa ile ndiyo itaonesha watu wangapi waliajiriwa na watu wangapi wamepunguzwa. Lakini ni muhimu la kusema kwamba, uchumi huu una uwezo zaidi kuliko miaka kumi iliyopita kwa sababu leo makusanyo haya yanayofikia shilingi bilioni 259,060 haingeweza kupatikana kama uchumi huu haukuongezeka, hii ni kwa mwezi kutokana na uchumi wetu kukua. Moja ya hatua ya kukuza uchumi huu ni ubinafsishaji.

Chukua mfano wa *TBL* kwa mfano, miaka ile ya 1990 – 1995, mchango wake kwa Hazina ulikuwa shilingi bilioni 4, 5, leo inafika zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa hiyo, ukitazama hivyo, utaona hata ajira hapa pia imeongezeka kwa sababu amejenga viwanda vingine cha Mwanza, Arusha amepanua cha Dar es Salaam, kwa hiyo, hapa tu kwa *implication* ajira imeongezeka na hiyo siyo kwa *TBL* tu hata ukienda kwa *Tanzania Cigarette Company, Tanzania Cement*, vyote hivi vimeongezeka. Kwa hiyo, hili jambo siyo kama liko sehemu moja. Ubinafsishaji uliobaki kwa mashirika yaliyobaki upewe uwe wa uangalifu, hili tumekubali na tunaendelea kulitekeleza kama nilivyosema huko nyuma na hii hoja imeletwa na Mheshimiwa Kabwe Z. Zittto. Penye ubia na wageni ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa, Watanzania wanafaidika na ubia huo kwa kiasi cha kutosha, hili tunalikubali na ndivyo imekuwa ikifanyika kwa mfano, *NMB, DAHACO*, Saruji ya *Wazo Hill*, Saruji ya Kiwanda cha Tanga, Sigara, *TBL* na kadhalika. Huko kote tumehakikisha kwamba, wananchi wananufaika, hakuna kuonewa katika nchi yao. Ajira 88,713 zilikuwa zimepatikana hadi mwaka 2005, si za mashirika yaliyobinafsishwa tu bali zinahusisha na mashirika ambayo hayakuwa yamebinafsishwa. Kama nilivyosema mwanzo, haya yanahusisha mashirika yaliyobinafsishwa, lakini vilevile na mashirika mengine. Lakini sehemu kubwa ni katika viwanda vilivyobinafsishwa.

Serikali ichukue maamuzi mahususi ya kulinda wawekezaji wa viwanda vya ndani mfano, viwanda vya kuzalisha magunia na zao la mkonge. Hili tunakubaliana na Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, ulinzi wa viwanda vichanga ni muhimu na inayokubalika katika kujenga Sekta ya Viwanda. Tanzania kama mwanachama wa Shirika la Biashara la Ulimwenguni *(World Trade Organization)*, inawajibika kuzingatia taratibu na sheria zinazoongozwa mfumo wa biashara Ulimwenguni kutokana na taratibu hizo. Mfumo huu unatambua na kutoa nafasi kwa nchi zinazoendelea, kutumia sera na kulinda viwanda vichanga kwa kipindi cha muda mfupi, wakati viwanda hivyo vinajenga uwezo wa ushindani. Maana yake hapa ni kwamba, huwezi kuwa na ulinzi wa kudumu. Kwa hiyo, tutalinda pale tunapoanza lakini baadaye lazima viwanda hivi vikamilike ili viweze kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwamba Serikali ieleze masharti ya mkopo wa shilingi bilioni 45 kutoka Benki ya Dunia, zilizotolewa kwa ajili ya kuwezesha mashirika kama vile *TICRA, CCAA, SUMATRA* na mashirika mengine ya usimamizi. Utekelezaji wa mradi wa ubinafsishaji na uendelezaji wa sekta binafsi *(Privatization and Private Sector Development Project),* unaendelea vizuri kwa mujibu wa makubaliano na mkataba kati ya Serikali na Benki ya Dunia. Utekelezaji wa Mradi huu uko katika hatua ya mwisho, ambayo inahusu ukamilishaji wa kazi zilizobaki za ubinafsishaji, pamoja na uundwaji na kuzijengea uwezo mamlaka ya udhibiti *(EWURA)*, Tume ya Ushindani wa Haki Kibiashara *(Fair Competition Commission),* Mahakama ya Ushindani *(Fair Competition Tribunal),* fedha hizi zitaendelea kutumika katika kazi hizi.

Halafu ilisemwa kwamba, kuna haja ya kuwa na chombo cha kuratibu masuala yaliyobakia katika zoezi la ubinafsishaji. Hili tunalitafakari na wakati muafaka ukifika, Waheshimiwa Wabunge mtafahamu, kwanza hili lazima lije Bungeni kwa sababu haliwezi kutoka tu hivi hivi.

Kwa sababu ya muda, nitaruka baadhi ya hoja. Suala la *EPA* ambalo amelileta Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, limeelezwa vizuri na Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi na mimi nampongeza sana. Bahati nzuri Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, alichukua nafasi ile ambayo mimi niliishikilia mwaka 2001, nilikuwa ndiyo Mjumbe wa Pili kuwa katika *European Union and ACP Joint Parliamentary Assembly*. Kwa hiyo, maneno haya ni sawa, lakini kama Waziri wa Biashara wa zamani, hili suala lina historia yake. Labda niseme kidogo, suala la *EPA Configuration* katika nchi yetu linatokana na hali halisi. Uamuzi wa Mamlaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa mwaka 2003, ilikuwa kwamba, sisi tuwe peke yetu kama Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Lakini tulipokwenda kwenye Mkutano wa *ACP Heads of State and Government,* uliofanyika Fiji mwaka 2003, wenzetu wale wawili wakaamua kwenda *ESA*, kwa sababu wao ni Wajumbe wa *COMESA*. Sisi hatuko *COMESA*, kwa hiyo, sisi tukaenda *SADC*. Hiyo ndiyo *configuration* iliyofanyika. Kuna baadhi ya nchi zimekwenda *ESA* na baadhi ya nchi zimekwenda *SADC*. Lakini vilevile kuna ukweli kwamba, katika *COMESA* kuna nchi nyingine hazimo katika *ESA,* ndiyo maana kuna watu wanatania kwamba, *ESA* maana yake ni *COMESA minus COM,* ndio unapata *ESA*. Kwa hiyo, si kweli kwamba, sisi kama nchi, tumezembea hata kidogo, tunaendelea kushiriki katika mjadala huo na vilevile kama alivyosema Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, suala la *regional integration* wanalazimisha *European Union,* kama mnakumbuka walikuja hapa mwaka 2004 wakasema ya kwamba, Tanzania mtoke *SADC* muingie *COMESA,* kwa sababu *East African Community* ndiyo mahali pazuri pa Tanzania kuliko *SADC*.

Sasa watu wote tunajua historia ya Tanzania kuwa katika *SADC* kwa sababu imeanza na wakati wa *front line state*. Sasa leo sisi ndiyo tulikuwa *Champion* wa *front line state* na baadaye tukau-*transform* ushirika ule kuwa wa kiuchumi wa *SADC* sisi ndiyo tuwe wa kwanza kuhama jamani jambo hili linawezekana? Haliwezekani ndiyo maana sisi tuko *SADC*. Sasa tunaendelea kuzungumza kama utakuwa wakati muafaka tukaungana katika Afrika Mashariki kwamba mahali pazuri pa *EPA* kwa Afrika Mashariki ni Jumuiya ya Afrika Mashariki, basi tutakuwa humu pamoja. Lakini hakuna muda kuishi kwa sababu kuna uwezekano pia wa kuahirisha mazungumzo haya. Kwa hiyo, haya siyo *water type* siyo kama amri ya muda sawa sawa. Kwa hiyo, mimi nasema hili tunalifanya vizuri na kuendelee kulijadili namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja za maandishi. Mkakati gani wa kuwezesha kuweka hali *(regime)* ya mikopo ya muda mrefu na riba ya *digit* mbili kwa wananchi ili kuongeza kasi ya uwekezaji wa wananchi. Hili amelileta Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama. Benki za Biashara zilizopo hazitoi mikopo ya muda mrefu, ndiyo maana Serikali imefanya mkakati wa kuiwezesha *TIB* iwe Benki ya Maendeleo, ambayo itakuwa inatoa mikopo ya muda mrefu. Kwa hiyo, hili jambo halikupuuzwa tunashughulikia kikamilifu. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Shamba la Magamba nafikiri tumeshajibizana mara nyingi. Lakini ngoja nijibu tena leo hapa na nakuomba usishike

kifungu au shilingi. Kwa sababu hii ni sera yetu, iko katika Ilani ya Chama chetu. Katika sekta ya kilimo, tuna mikakati ya aina mbili; kwanza mashamba madogo madogo ya wananchi, haya mashamba tutaendelea kuyaheshimu, tutaendelea kuyasaidia kwa hali mali. Kwa mfano, suala la pembejeo, suala la mbolea, suala hata la kilimo cha trekta, yote haya yanazungumzwa katika kuendeleza kilimo hiki na ndiyo maana kuna Mradi mkubwa wa *ASDP*, kuna Mradi wa *PADEP*, kuna Miradi ya *DADPs,* yote hii shabaha yake ni kuimarisha kilimo hiki kidogo.

Pia kuna *National Irrigation Master Plan,* yote haya ni kuboresha kilimo cha wakulima wadogo wadogo. Lakini vilevile tumekubaliana, tutakuwa na mashamba makubwa. Sasa mashamba makubwa ndiyo hayo, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, alitaja mfano wa Mbarali. Mimi nilikwenda na Waziri wa Kilimo, tukatoa maelezo na wananchi wakakubali, kwamba ni kweli haki ya Serikali kuendeleza mashamba haya kama mashamba makubwa. Isipokuwa tuliwaomba wawekezaji wale, wawashughulikie na wakulima wadogo wa umwagiliaji. Nao pia sasa wanawasaidia. Kwa hali ya sasa, kwa habari nilizokuwa nazo mimi katika mashamba yale ya Mbarali, mambo ni bora zaidi kuliko ilivyokuwa miaka miwili iliyopita. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sera hii lazima tuendelee nayo tusiikatae. Mbozi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, hawana tatizo kubwa la ardhi, kama lipo basi tutalishughulikia hilo tatizo. Lakini mimi nadhani kuwa na *strategy* namna hii ni nzuri kwa taifa letu. Wao tulishawapa mashamba mengine ambayo waliyatumia kwa ajili ya kilimo. *Actually* tuliweka masharti nafuu sana mpaka leo bado wanalipa kidogo kidogo, lakini si neon, tuendelee kuwaambia wananchi hao.

Lingine, je, wewe Waziri utakwenda kule kuangalia? Mimi niko tayari kwenda na tutakwenda na Mheshimiwa Mbunge kule ili tukawaeleze wananchi kwa sababu suala hili ni maelezo tu, tumefanya Mbarali wananchi wamekubali, tumefanya kule mashamba ya *West Kilimanjaro,* kwa hiyo, mimi nina hakika kabisa hili tutalifanya na hatuna wasiwasi.

Halafu Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, suala la *SELF,* kwa nini haijafika jimboni kwangu. Sawa sawa kama nilivyosema katika hotuba, *SELF* mpaka sasa inakwenda Mikoa 12 tu. Lakini tutajitahidi kadri uwezo utakavyopatikana kuweza kusambaza huduma hii katika Mikoa yote. Je, *TASAF* kwa nini inachelewesha malipo, *TASAF* inachelewesha malipo basi hili suala tutalishughulikia, kwa sababu kwa kweli sehemu kubwa ya kazi zilizokuwa zinafanyika na *TASAF* pale ni kuwasaidia sehemu ya gharama. Sehemu ya gharama nyingine wao wenyewe wanatamiza. Sasa kama sehemu ile ya kwao hawakuitimiza, lazima miradi itachelewa na hili ni jambo la kulitilia mkazo pale pale katika ngazi ya Kijiji ama Kata ambako mradi unatekelezwa. Lakini sisi katika *TASAF* tuko tayari wakati wote. Mgao wa bajeti wa *TASAF* Bukombe umekwisha? Je, Serikali ipo tayari kuongeza mgao mwingine? Tunatoa pongezi kwa Wilaya ya Bukombe, kwa kuweza kuhamasisha wananchi wake na kuibua miradi kulingana na mgao wa fedha. Changamoto kubwa waliyonayo ni kuweza kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo kwa ukamifu ili iweze kujibu kero zao. Serikali kwa upande wake, itaangalia kwa ujumla,

uwezo wake namna ya kuendeleza dhana ya ushiriki wa jamii katika utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, amezungumzia kwamba, Serikali inachukua hatua gani kuwatambua vijana ambao wanakaa vijiweni bila kazi maalum.

Serikali kupitia vyombo vyake mbalimbali, inafanya kampeni ya kuhamasisha wananchi wake wakiwemo vijana wa vijiweni ili waweze kuanzisha miradi ya uzalishaji mali na kujipatia kipato. Aidha, vijana wanahamasishwa kujiunga katika vikundi kama vile Vikoba na *SACCOS* ili waweze kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali na hatimaye kupata mikopo.

Mheshimiwa Lekule M. Laizer, ili kupunguza umaskini ni muhimu kuwa na masoko ya kuuzia mazao yaliyozalishwa na wajasiriamali. Hili tunalikubali ni jukumu muhimu na viko vyombo kadhaa ambavyo vinashughulikia masuala ya kuuza, kusaidia kuuza bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo. *SIDO* ni mojawapo, kwa hiyo, jambo hili halikupuzwa lina mkakati nzuri wa kuweza kushughulikia. Vilevile kule Longido, Bahi, Chamwino, Chatu, Kilindi, Kilolo, Kishapu, Misenyi, Mkinga, Mkuranga, Nanyumbu, Namtumbo, Siha, Simanjiro na Tunduru, wataweza kusaidiwa kwa kujengewa masoko ili yaweze kusaidia wananchi kuuza bidhaa zao.

Idadi ya wataalam waliopo Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, haitoshelezi kulingana na majukumu yao. Mheshimiwa Juma H. Killimbah, nakubali kwamba hawatoshelezi lakini hii haina maana kwamba, kazi haifanyiki. Kwa sababu kama mlivyoona ule mpango tuliupitisha hapa na vipaumbele vile vitano tulivyokubaliana hapa, vinatokana na Wizara ya Mipango ambayo baadaye ikaenda kwenye Serikali na Serikali ikaamua hivyo. Kwa hiyo, kupanga kwa sasa kusimamia utekelezaji kwa sasa kazi inafanyika. Ni kweli kwamba na kama nilivyosema pale mwanzo, hii kazi ya *capacity building* ya kuwa na wataalam haiwezi kuwa na mpaka, lazima itakuwa ni *continuous.*

Kwa mfano, mwaka peke yake, wataalam waliotoka Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, kwa kuteuliwa kuwa Makatibu Wakuu au Maafisa Tawala wa Mkoa, ama kwenda kwenye Idara nyingine au Wizara nyingine walikuwa zaidi ya saba. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, ukiondoa hawa lazima kuwe na *training,* ajira kwa watu wengine. Kwa hiyo, hili jambo la *capacity building* tutaendelea kulifanya na haliwezi kuwa la muda mdogo.

Hili la Mheshimiwa Juma H. Killimbah, pia amezungumzia suala la MKURABITA na MKUKUTA. MKUMBITA hili nafikiri tumelieleza, maana yake kwa kweli ni Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania. Lengo lake ni kuifanya nchi yetu iwe na uwekezaji mkubwa zaidi. Kwa hiyo, hili jambo linafanyika na MKUKUTA tunajua wote na *TASAF.* Kwa hiyo, hii mikakati ni sehemu ya utekelezaji wa Sera yetu ya Dira ya Maendeleo ya 2025.

Labda hapa pia niweze kulijibu suala la Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe kwamba, kwa nini sasa Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa uje na mpango wako kama ilivyokuwa *Marshal Plan,* lakini sisi tayari tunao mpango. Mpango wetu ni Dira ya Maendeleo ya 2025, ambayo malengo yake ni kutufikisha kuwa *middle income country* inapofika mwaka 2025. *(Makofi)*

Utekelezaji wa *Mini-Tiger Plan,* utekelezaji wa MKUKUTA, utekelezaji wa MKUMBITA, utekelezaji wa *TASAF*, yote haya shabaha yake ni kutufikisha kule na ndiyo maana tunakuwa na bajeti ya kila mwaka ili tufike huko. Kwa hiyo, mpango upo, kinachotakiwa sasa ni kufanya. Naona Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, anakataa lakini

**NAIBU SPIKA:** Alisema Mheshimiwa Job Y. Ndugai, aliyekuambia ulete.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Wote hawa ndiyo na Mheshimiwa Job Y. Ndugai pia na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe. Kwa hiyo, hoja hapa ninachosema ni nini. Hoja ni kwamba, mpango huu lengo lake ni kutuondoa hapa tulipo ili tufike huko tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, suala la *Environmental Impact Assessment,* tunalikubali ni la kisheria kwanza. Kwa hiyo, hili litaendelea kutekelezwa. Kule tunakosema kule katika kupanda miti ile, siyo kupanda miti *actually* ni kufanya majaribio ya kupanda miti ya mikaratusi ambayo hainyonyi sana maji. Kwa hiyo, hiyo ni hatua ya kwanza kufanya *testing* je, inafaa? Kama itafaa mambo yote ya *Environmental Impact Assessment* yatafanywa kama sheria inavyotaka ili kuanza kutekeleza. *(Makofi)*

Mpango wa Taifa wa miaka mitano mitano umeishia wapi? Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mpango huu uliisha kwa sababu kama mnakumbuka, miaka ile ya 90 tulikuwa na matatizo ya kiuchumi. Ndiyo matatizo yale yakatupeleka kwenye *cash budget* na ikatupeleka kwenye miaka mitatu mitatu ya mpango. Lakini sasa hali ni nzuri sisi tunajiandaa kurudisha mpango wa miaka mitano. Hili kwa kweli ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Rais mwenyewe ameshatuelekeza Wizara ili tulitazame namna ya kulitekeleza suala la kupanga miaka mitano mitano. Kwa hiyo, hili litashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iunde *special development corridor* kwa ajili ya Singida. Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, hii dhana ya *special development corridor* hii ya Singida imo kwa sababu tuna tatu katika nchi. Ya kwanza ni Mtwara, mwenzangu ananikumbusha nne, ya kwanza ni ya *Mtwara Development Corridor,* ambayo inahusisha mikoa kama sita hivi, ambayo inaanza Pwani, inachukua sehemu ya Morogoro, inakwenda Iringa mpaka Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Lindi na Mtwara. Hiyo ndiyo Mikoa ya *Mtwara Corridor.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna *Central Development Corridor* inayochukua Mikoa ya Kati, Dar es Salaam mpaka Kigoma, Shinyanga na Mwanza. Halafu kuna *Northern Corridor,* ambayo ndiyo inayochukua Tanga mpaka Arusha. Kwa hiyo, *corridor* kama *system* ya kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iko tayari na hivyo kwa maana hiyo basi, Singida nayo imo. Hoja hapa ni lini utekelezaji wa miradi

fulani ambayo inahusu Singida inaanza. Lakini iko ya barabara inayopita kuanzia Dodoma, Singida, Shelui mpaka Shinyanga ni sehemu ya hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu ya Reli ya Kati, ndiyo hiyo nilikuwa nazungumza kwamba, tumepata mkopo ambao utakarabati reli hii ili treni sasa ifike Dar es Salaam. Kwa hiyo, hiyo nayo ni sehemu ya Singida. Lakini kuna barabara nyingine, barabara ambayo tunaifikiria na tunaitafutia fedha, barabara ya Manyoni, Itigi, Igalula, Tabora, Urambo mpaka Kigoma. Ndiyo kuna barabara nyingine tunaitengeneza sasa hivi, tumeanza kuitengeneza ya Babati mpaka Singida. Kwa hiyo, Singida kwa maana ya *Special Development Initiative (SDI),* imo na miradi ya kutekeleza imeshaanza na mingine inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ianze utaratibu wa kutawanya maendeleo katika nchi nzima na siyo Dar es Salaam peke yake, ambako kunaonekana kumejaa na pia itapunguza tofauti ya maendeleo kati ya mikoa na mikoa. Hii imeletwa na Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, tunaikubali na *actually* tunaitekeleza, kama mtakumbuka nilizungumza pale vigezo vya kutoa fedha. Nikasema moja ni hali ya umaskini. Ya pili, nikasema inahusu uwingi wa watu, ama idadi ya watu. Ya tatu, nikasema inahusu ukubwa wa eneo, lakini lazima utoe maeneo ya hifadhi au maeneo ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hizi tatu hizi lengo lake ni kuwezesha miradi hii isambae nchi nzima. Lakini lazima tukubaliane vilevile kwamba, kwa hali ilivyo ya sasa hivi Dar es Salaam, lazima itakuwa kivutio kikubwa sana cha wawekezaji. Kwa mfano, juzi tu hapa nilipokuwa nimekwenda Mtwara, tumechukua muda mkubwa kuwa-*convince* kwamba, badala ya kujenga kiwanda kingine cha saruji, wale wawekezaji kutoka Nigeria, Dar es Salaam mkajenge Mtwara. Mtwara ina bandari, *deep port,* ambayo kwa kiwango kile inapata hata ya Dar es Salaam lakini ya pili kuna *limestone* pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukaenda nao. Kwa kweli wamekuwa *convinced, inshallah* wanaweza kuja. Lakini lazima tukubali kwamba, miradi hii mikubwa inakwenda kwa kizingatia kanuni za uchumi. Kama uchumi unaruhusu, yaani kwa maana ya kupata faida, ndiko watakwenda. Lakini huwezi ukampeleka mtu akajenge kiwanda jimboni kwangu kule Ulanga. Ni ngumu sana, kwa sababu kwanza kuna mto pale kuna feri, ile feri peke yake ni kikwazo tayari. Kwa hiyo, lazima tukubaliane kwamba, kuna baadhi ya maeneo miradi ya aina fulani haitakwenda, kuna baadhi ya eneo miradi fulani itakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampeni ya kuondoa umaskini bado haijawa na hamasa kubwa. Mheshimiwa Devota Likokola, mimi nasema ina hamasa kubwa. Tunazungumza suala la kuondoa umaskini. Tunazungumza kila siku suala la MKUKUTA, kama ni jambo la kuondoa umaskini na tumetoa semina hata humu Bungeni kuhusu MKUKUTA na tunaendelea kutoa semina sehemu mbalimbali katika nchi yetu. Lakini vilevile Ilani ya Chama chetu ni kampeni kubwa sana, tumetumia wakati tunaiuza kwa ajili ya kuondoa umaskini nchi yetu kwa ajili ya kukuza uchumi. Sasa hizi kampeni

lazima ziendelee hazina kikomo hizo lazima tuendelee nazo na siyo mtu mmoja tu anaweza kufanya, lazima tufanye wote, Wabunge, watendaji katika Serikali hata watendaji katika chama chetu lazima waende, hata Wabunge kwa ujumla wao, lazima tuendelee kulishughulikia suala hili ili tuweze kupata maendeleo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, wanawake tumewasahau? Hapana, wanawake hawakusahauliwa. Kwa mfano, nilisema pale *SELF,* asilimia 60 ya wanaofaidika na *SELF* ni wanawake. Hata hii mikopo hii ya ujasiriamali, hii ya shilingi bilioni 21, walionufaika wengi ni wanawake. Kwa hiyo, hakuna katika nchi yetu kubagua wanawake, tunaendelea nalo ingawa napenda kumpongeza sana yeye, kwa juhudi alizofanya katika kuanzisha Vikoba na uendelee navyo. Maana Vikoba vile vinasaidia sana kuleta maendeleo katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe na *timeframe* ya utekelezaji wa Ilani ya CCM na ijulikane. Ndugu yangu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, *timeframe* ya Ilani ni miaka mitano, *obvious, timeframe* ya MKUKUTA ni miaka mitano. Kwa hiyo, *timeframe* iko na sisi wote tunatekeleza ili kufikia *timeframe* ile lakini kitu muhimu ambacho nataka kusema ni nini? Kupanga ni kuchagua, kama alivyotufundisha Mwalimu Nyerere, hatuwezi kutekeleza miradi yote na ahadi zote mwaka wa kwanza na mwaka wa pili. Lazima tupange mwaka wa kwanza tutafanya hili, mwaka wa tatu tutafanya hili, mwaka wa nne tutafanya hili na hatimaye mwaka wa mwisho. Haiwezekani katika hali yetu ya rasilimali tutekeleze miradi yote na ndiyo maana kwa mfano, mwaka huu wa fedha tumeamua vipaumbele vitano. Elimu, Afya, Maji na Miundombinu. Nilisahau, mbili ni miundombinu, maana kwanza ni elimu, miundombinu ilikuwa namba mbili, halafu afya, maji na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele hivi tumepewa kwa makusudi kutokana na uhaba wa rasilimali tuliokuwanayo ili tuanze navyo hivi. Tumetenga shilingi bilioni 777, kwa ajili ya miundombinu. Haijapata kutokea. Kwa hiyo, hata ile ya kupanga trilioni moja, kwa ajili ya elimu, haijapata kutokea pia. Kwa hiyo, mambo haya tunayafanya kwa vipaumbele na mimi nina matumaini kabisa kwamba, tukifanya hivi tutafikia malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho maana muda unaisha ni la Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, ushauri kwanza wa kuwa na *millenium town.* Hili tunalijua, tumelianza kulijadili. Lakini mimi nafikiri tufurahi kwanza na tutekeleze vizuri ile *millenium village* ya Mbola, ile ambayo kwa kweli inaelekea tunafanikiwa pale. Kwa hiyo, tuendelee kuipanua ile kwa maana ya ku-*re-implicate* siyo tu Mbola yenyewe, sehemu nyingine za Mkoa wa Tabora nazo tuzifanye hizi kwa utaratibu ule ule ili tuweze kufikia maendeleo tunayotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile la pili la kusema sisi ni Wizara ya Mipango ni *think tank* ni kweli *think tank* ya nchi yetu. Sisi ndiyo tunaoandaa kwanza mipango kabla ya kwenda kwenye Serikali na ndiyo jukumu letu. Lakini hatutumii siku zote sisi wenyewe, tunatumia *consultants*, wapo wanakuja na tutaendelea kuwatumia. Tunatumia wataalam wengine katika Tanzania ambao wapo, kwa mfano, *Economic and Social Research Foundation, REPOA, Economic Research Bureau* ya Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam, hawa wote tunawatumia kwa lengo la kuboresha kazi zetu na mimi nadhani kazi zetu ziko *so far* zinakwenda vizuri kutokana na hili jukumu la kushirikisha watu wote katika kupanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Kama nilivyosema, hoja zilikuwa nyingi na muda mfupi, lakini tutajitahidi kuandaa maelezo yote haya ili tuweze kuwapeni na muweze kujua majibu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Naona hoja imetolewa na kuungwa mkono ili tufikie uamuzi sawasawa, tunaendelea na hatua nyingine.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 66 – Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji**

Kif. 1001 – *Administration and General* .... .... Sh. 14,763,070,900.00

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. Tunaanza na Mheshimiwa Ameir Ali Ameir. *(Makofi)*

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza. Wakati nilipokuwa nachangia kwa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri aje anifahamishe kuhusu uwakilishi wa Chuo cha Mipango. Hapo zamani katika Bodi yao ilikuwa lazima kuna na mtu wa Zanzibar. Lakini kwa kipindi kirefu hivi sasa hakuna. Nilimwomba akija anifafanulie vipi ile nafasi imefutwa kwa Zanzibar? Asante.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, kama ifuatavyo: Ni kweli kwamba, alitoa hoja hii kwenye karatasi zetu, kwenye mchango wake kwa maandishi. Lakini kutokana na muda sikuweza kufikia. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, sina hakika kama tumeufuta, lakini kama tumeufuta mwakilishe yule wa Zanzibar basi tutaurudisha.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *vote* hiyo hiyo namba 66, mshahara huo huo wa Waziri. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri tena ya kistaarabu kuhusiana na suala la *EPA,* nakushukuru sana kwa kutenga shilingi trilioni 600 kwa ajili ya *Kigoma Special Economic Zone.* Ni mwanzo mzuri huko mbele, naamini kwamba tutapata fedha zaidi. Sasa nilikuwa nataka maelezo katika vitu viwili, ambavyo nilivieleza katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza nilisema kwamba, kwa mujibu wa Sheria ya *TIC,* sehemu ya 7 ya Sheria hiyo, uteuzi wa Bodi ya *TIC* umewekewa sifa maalum za kuzingatiwa na nikawa nimeeleza kwamba, uteuzi ambao umeufanya hivi karibu wa Bodi ya *TIC,* umekiuka hizo sifa na nikatoa mfano kwamba, umemwondoa katika Bodi ya *TIC* Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, kitu ambacho ni muhimu sana kwa eneo la uwekezaji na nilikuwa naomba nipate maelezo kuhusiana na suala hilo na umetumia vigezo gani kuweza kuamua jinsi ambavyo uliamua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilizungumzia suala la aidha kufanya *extension* ya *PSRC* ili kumaliza zile kazi ambazo niliziainisha katika hotuba yangu ama kuwa na chombo maalum kwa ajili ya kushughulikia kazi ambazo hazijamalizika za *PSRC.* Umenijibu vizuri kwamba, Sheria lazima ije Bungeni. Lakini ni kwamba, *PSRC* kama jinsi ambavyo Waziri mwenyewe amesema, inamaliza mwezi Desemba na tumebakiza Bunge moja tu la mwezi Novemba na mpaka sasa tunavyozungumza, hatujaona Muswada wa aidha, *extension* ya *PSRC* au uanzishaji wa chombo haujasomwa kwa mara ya kwanza na kwa vyovyote vile, Miswada ambayo tunajadili Novemba, ilisomwa kwa mara kwanza katika Bunge hili.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba *commitment* ya Mheshimiwa Waziri, katika suala hili na jinsi gani ambavyo tutalifanya ili kuweza kuepuka madhara ya muda kwisha kabla kazi hazijakamilika au zile mali ambazo *PSRC* inazisimamia zisije zikapotea kama jinsi ilivyotokea kwa *LART.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, maswali yake mawili kama hivi. Kwanza, kuhusu uteuzi wa Bodi ya *TIC*. Si kweli kwamba, kulikuwa na njama mbaya ya kumwondoa Katibu Mkuu wa Ardhi, hoja pale ilikuwa kwamba, Katibu Mkuu wa Wizara ni mkubwa sana kuwa katika Bodi. Kwa hiyo, tulitaka na halafu kwa muda wake wa kukaa kwenye Bodi ni jambo ambalo siyo *practical* sawa sawa. Kwa hiyo, tulimwondoa ili aingie mtu ambaye anaweza akapata muda mrefu zaidi. Hili pale *TIC* tuna balaa lingine, hata Mbunge ambaye tumemteua pale, naye vikao vingi hashiriki na kuna maombi ya kusema tubadilishe lakini tunafikiri si vizuri kumbadilisha Mbunge wakati huu. Kwa hiyo, hili suala ni la kuimarisha utendaji tu na mwenye kutazama utendaji bora katika Taasisi zilizoko chini ya Wizara ni Waziri muhusika na mimi nilifanya hivyo kwa nia njema ya kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *PSRC,* nimesema hapa tunajua kwamba, *PSRC* itakwisha muda wake Desemba 31 na kwamba Serikali inatafakari namna ya kuiwezesha *PSRC* ama chombo kingine chochote kifanye hiyo kazi. Kwa sababu kazi hizi zilizobakia hazitakamilika ifikapo Desemba 31. Kwa hiyo, hili jambo siyo kama nilishalijibu na naomba nilirudie kwamba, mipango ya namna gani shughuli hizi za *PSRC* zitatekelezwa baada ya muda wa *PSRC* kwisha. Lakini nataka kukupa taarifa kwamba, Serikali tayari imeshaomba zile fedha ambazo tulipewa kwa ajili ya kuendeleza shughuli za *PSRC,* tumeshaziomba na tumeshakubaliwa na *World Bank* kwamba, tuendelee nazo. Kwa hiyo, fedha ziko na namna gani ya kuendelea, tutaamua hapo wakati utakapokuwa muafaka.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. *Vote* ya 66.

**MWENYEKITI:** Tumeruhusu uendelee tu, mshahara wa Waziri.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Katika kuchangia kwa maandishi, nilijaribu kushauri kupanua wigo wa Sera ya Uwekezaji, nikaangalia upande wa wakulima kwamba, katika nchi yetu kuna nafasi kubwa sana ya kuweza kuendeleza hili zao la matunda na nikataja Wilaya ambazo zinaweza kutoa matunda mengi ikiwemo Geita, ambayo ambayo ina mananasi mengi na watu wameshafanya *research* na kuona kwamba, inatoa mananasi mazuri sana, ambayo nafikiri katika ulimwengu ni *first class.* Nikawa nimeshauri kwamba, kutafuta wawekezaji au kuanzisha kiwanda ambacho kinaweza kusindika kwa sababu sasa hivi watu wana-*move* kunywa vinywaji vikali, ukikuta kwenye sherehe tunapata *juice* kutoka Afrika ya Kusini, tunapata vinywaji kutoka Uganda, Kenya, lakini kwetu matunda yetu ni kama hatuyafanyii kazi. Sikupata majibu labda hakuiona, lakini nilikuwa nimeshauri kwamba, tupanue wigo wa kutafuta namna gani tunaweza kufanya na sisi wakulima wetu waweze kuzalisha.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungama kweli nililiona hili limeandikwa kwenye makaratasi yetu haya, lakini hatukuweza kufikia. Mimi kwanza ni Bwana Shamba wa siku nyingi pale Geita, mwaka 1967 nilikuwa pale kwa hiyo, haya mananasi ninayajua, ingawa mananasi ya Kinole ni matamu zaidi kupita yale ya Geita, lakini mananasi ni mazuri. Kwa hiyo, suala la kuhimiza wawekezaji tunaendelea nalo. Tunahimiza kweli sisi wawekezaji wa kila aina. Kwa mfano, pale Morogoro ndiyo sasa hivi wanajenga kiwanda cha matunda. Pale Korogwe nako wamechukua eneo lile la zamani la Tangold ili wajenge kiwanda cha matunda kwa ajili ya kukamua. Morogoro pale watakamua mananasi na machungwa, machungwa yale ya Matombo yale ni matamu sana. Kwa hiyo, kiwanda hiki kitafanya kazi hiyo, lakini vilevile kile cha Korogwe. Kwa hiyo, mimi naomba tuendelee kuhamasisha na ndiyo maana tumefungua Ofisi ya Kanda Mwanza, kwa ajili ya Kituo cha Uwekezaji, ili tuhamasishe wawekezaji waje kuwekeza katika maeneo mbalimbali katika uchumi wa mkoa.

Ni muhimu hapa kusema kwamba katika viwanda hivi vya ku-*process* matunda ni *small to medium*. Hivi tusingoje watu wa nje, tufanye wenyewe kwa ushirika ama kwa makampuni ya wananchi kama tulivyokubaliana au wananchi wachache kujichagua na kupanga na kuanza kuzalisha ku-*process* hayo.

Asante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Asante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mshahara wa Waziri. Katika mchango wangu nilikuwa nimeongelea kuhusu makampuni mengi tunayo yaliyowekeza hapa nchini, ambayo yanapata *investment incentives,* lakini idadi ya watumishi wake wa kigeni, nazidi kuongezeka kinyume cha sheria ambayo inaweka *immigration quarter* ya watumishi watano na jinsi kifungu cha sheria kinavyoonekana, inaonesha kwamba, kila baada ya muda ile idadi ipungue, Watanzania wa-*take over* na nikatoa mfano wa *NDC* kwamba, mwaka 2000 ilianza na *expatriates* watano, badala ya kupungua sasa wako 13 na sisi Watanzania katika suala la kusomesha kwa upande wa *banking,* tumejitahidi sana. Sasa nilitaka kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri ni kitu gani cha ajabu sana kwa Serikali yenye hisa asilimia 30 ndani ya *NBC* kushindwa kusimamisha sheria tuliyotunga sisi mwenyewe ya hao wenzetu kubakia wachache, vijana wetu waliosoma wanawekwa pembeni tu kuwa makarani mpaka wanazeeka.

Halafu swali la pili ambalo linataka ufafanuzi, niliulizia kuhusu wataalam wa fedha na wachumi wanasema kwamba, panapotokea *dollarization* katika uchumi, dola kutumika, ujue kwamba, hapo kuna mfumko wa bei mkubwa, yaani fedha ya nchi imeanza kupungua thamani na watu wa ndani wanapata *confidence* kwenye fedha ya nje. Lakini Mheshimiwa Waziri, mara kwa mara yeye mwenyewe ndiye anatupa vigezo vya *inflation* kwamba ni kati ya 6 na 7, sasa hiyo siyo *inflation* kubwa. Hizo *figures* Mheshimiwa Waziri anazotupa ni sahihi au si sahihi? Sasa kama ni sahihi mbona dola inakumbatiwa na Serikali yenyewe vile vile?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa fursa hii, niweze kumjibu ndugu yangu pale, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, maswali yake yote mawili. Kwanza, lile la *quota* ya wafanyakazi, hasa *NBC*, maana yake yeye anaizungumzia sana na mimi nizungumzie kidogo, *NBC* walikuja mpaka kwangu ku-*appeal* utaratibu wetu. Mara ya kwanza kuomba *permit* ya kufanya kazi wanaomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana.

Wale waliwakatalia, wakafanya *appeal* kwangu, nikaandikiwa barua na wataalamu wangu kwamba, kwa kweli tuwaruhusu kuongeza muda, kwa wale ambao wako tayari, lakini Wizara ya Kazi ikawa *very committed* kwamba, lazima watoke kwa sababu hawa sio wataalamu na kwa kweli si wataalamu lakini ilivyokuja kwetu sisi tunafanya mambo mawili; moja *economic* lakini *also political experience*. Hawa benki hii pamoja na kwamba sisi tuna asilimia 30 pale, lakini wao ndiyo wanayo-*image* na ndiyo wanaoiendesha ile benki.

Katika ile *calibre* ambayo wanataka watu wale wabaki ni kwamba, *calibre* ile inahitajika. Kwa hiyo, ili kuacha kufanya uhasama katika jamii yetu tukakubali tuongeze watu wale wanne mpaka Septemba mwaka huu na wengine mpaka Juni. Nadhani sasa wameshaondoka na mmoja ndiyo atafika mpaka Septemba. Ndiyo hao wanne ambao wamefika kwangu, nimewashughulikia kutaka waondoke, lakini sina hakika kama kuna wengine kumi na tatu wamebaki pale, ninawajua wanne waliokuja kwangu na hawa ndiyo tulisema wabaki kwa sababu wao hawakuja kwangu mara tatu. Tulikubaliana na Mwenyekiti wake kwamba, tukifanya hivyo, huduma hasa ile ambayo walikuwa wanataka kuieneza ya *credit,* itafanyika. Kwa hiyo, mimi nikakubali tuongeze hiyo mpaka mwezi Septemba, 2007 na kufikia Desemba, wote hawa wataondoka na watachukua nafasi hizo Watanzania, kama tulivyokubaliana nao.

La pili, la *dollarization,* kwanza mimi nafikiri tuna *overstate*, labda niseme kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Naomba tutumie muda mfupi sana.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Siku zote wanakubaliana mambo na ndiyo maana kuna *two Cambriges* katika dunia; *Cambrige* ya Uingereza na Martha Chosence kule Marekani, ukisoma zile *literature economics,* siku zote hawa wanabishana kuhusu *economic theory*. Kwa hiyo, ubishi huu tutaendelea nao. Lakini mimi naweza kusema hivi, kuna ku-*overstate* kwamba *economic* ya Tanzania *is dollarized*, si kweli, sehemu ndogo tu ambayo ni *dollarized.* Hivi kweli kule vijijini tunabadilisha vitu vyetu kwa *dollar*? Sehemu kubwa ya nchi yetu hata hiyo *dollar* ya simu inayozungumzwa ni shilingi elfu tano, haijaongezeka zaidi ya hapo.

Kwa hiyo, mimi nasema vile vigezo vyetu tunavitumia vya *inflation* na *GDP Growth,* vimefanyiwa utafiti na taasisi zaidi ya nne. Msifikiri inafanywa na Wizara ya Mipango peke yake, hapana tunakaa Ofisi ya Taifa ya Takwimu wanakuja pale Benki Kuu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango, lakini *also* tunatumia *consultants* kutoka *economic and social research foundation* na *economic research bureau,* hawa wote tunakaa ndiyo tuna *agree on the national account,* ambazo ndizo zinatoa hizo *figures* za *the GDP growth* na za *inflation*. Kwa hiyo, hizi ni *full size, I can not guarantee this and I can not take my life on this figures* kwamba, *these are correct figures.*

**MWENYEKITI:** *You don not have to take your life*.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala alilolisema Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, juu ya *dollarization of the economy,* limezungumzwa na Wabunge wengi katika Kikao hiki cha Bunge. Kwa hiyo, tunafikiri tutatoa taarifa kamili ya Serikali kupitia Waziri anayehusika, kulielezea jambo hili na kulifafanua vizuri ili Wabunge waelewe na wananchi kwa pamoja waelewe. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Vote* hiyo hiyo, nami nilikuwa naomba Waziri anipe maelezo kidogo, amesema uchumi unakua kwa asilimia 6.2 kwenda mpaka 7 na nadhani tunaenda mpaka 8. lakini ukiangalia *population*

*growth* nayo ni 2.9. Kwa hiyo, ukitaka kupata asilimia halisi ya ukuaji wa uchumi, maana yake lazima uchukue hiyo utoe ile ya *population growth.* Kwa hiyo, nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri, ajaribu kuelezea hii *scenario; how does it work?*

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu ndugu yangu, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, kuhusu ukuaji wa uchumi katika Taifa letu. Katika mwaka huu wa fedha, tuna-*peg GDP Growth* ya uchumi wetu 7.3 *percent* na tuna matumaini kwamba, ifikapo mwaka kesho itaongezeka mpaka 7.7 *percent* mpaka kwenda 8 *percent*. Hiyo kwa kweli mimi nafikiri tutafikia *level* ile ya *8 percent, 9 percent* itakapofika 2010, ingawa *slight* iko chini kuliko ile *target* yetu ya Ilani ya Uchaguzi.

*We are on the right track*, ingawa pia kuna *optimism* kwamba, tunaweza tukapata zaidi. Sasa hii *growth* ya *population* ina-*affect GDP Growth? Yes it does,* lazima ndiyo maana tumetoa ile sera ya idadi ya watu ya mwaka 1992, tukaiandika upya mwaka jana, tukaitoa na ikazinduliwa. Kutakuwa na mkutano mwaka huu wa kuzungumzia suala la idadi la watu. Juzi tu hapa nilizungumzia suala hili la *growth* ya *population*, hilo lazima Watanzania tulizingatie, hatuwezi kuweka vima vya watoto, kule China mtoto mmoja kwa kila familia, lakini sisi hatuwezi kufanya hivyo, suala hili lazima tukubali sisi wote Viongozi wa Serikali na Waheshimiwa Wabunge kwamba, tunazaliana zaidi, tunachelewesha *GDP Growth* yetu na ili tusifanye hivyo, tupunguze kuzaliana.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote* nilitaka kujua katika ukurasa wa 31 wa Hotuba ya Waziri, amezungumzia baadhi ya matunda yaliyopatikana kutokana na Serikali kukaa na sekta binafsi. Baadhi ya matunda hayo amesema, naomba uniruhusu nisome kwamba, ni pamoja na kuanzisha kwa Mfuko wa Kuwasomesha Wataalamu wa Kitanzania, wenye vipaji maalum unaofadhiliwa na wenye makampuni makubwa nchini, pamoja na Benki ya Dunia na Serikali. Nilitaka kujua na pengine anipe ufafanuzi kwamba ni kwa namna gani, wanapata hao wataalamu wa Kitanzania, wenye vipaji maalum na ni kwa utaratibu gani na unapatikana wapi, maana yake ni kitu kipya ambacho nimekiona kwangu mimi binafsi, nilitaka kufahamu?

Lakini la pili, mengi yamezungumzwa na Wabunge mbalimbali, mimi nilitaka kufahamu tu kwa kifupi, *what is the current rate of inflation* ili tunapozungumzia mipango tuweze kujua *currently inflation* iko vipi?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nijibu hili fupi kwanza, hili la pili, *current inflation* ni *6 percent*, ilikuwa 7.3 mwezi Machi ikashuka mpaka *5 percent* mwezi Mei, sasa Juni, Julai, hii imekwenda juu kidogo inafikia *6 percent*. Lakini *basically,* nataka kusema kwamba, shabaha yetu tuwe *single digit*, ikiwa *two digits* ndiyo ina matatizo kwa uchumi wetu. Kwa hiyo, tukiwa 6, 7, 8 hapa sio mbaya, kwa sababu ni *single digit,* lakini tutaendelea ku-*control* na ili iwe chini ya asilimia 6 au chini ya asilimia 7.

Hili la *scholarship fund*, ambayo ni *fund* imewekwa, ingawa inaitwa *CIOS* lakini ni *fund* ambayo wao ndiyo ile mikutano niliyozungumza ya *Tanzania National Business*

*Council,* pamoja na *Domestic Investor* na *International Investor,* wao ndiyo walisema moja ya vikwazo katika utekelezaji wa shughuli wa sekta binafsi ni *mind set* ya Watumishi wa Serikali, ambayo inazingatia zaidi hali ya uchumi wa zamani badala ya kuwa *market oriented* ku-*facilitate private sector.* Wakija pale *sector,* unawachangamkia unawapokea vizuri, unazungumza nao, halafu ili waweze kuwekeza, hawa ndiyo waliyoibuni hii fani na wao ndiyo walikuwa wa kwanza kuchangia *dollar* 200,000 na wakalazimisha kwamba, Serikali mchangie. Serikali tukakubali tukachangia *dollar* 200,000 na *World Bank* wakasema na wao watachangia *dollar* 200,000. Kwa hiyo, sasa hivi tayari tuna *dollar* 600, lakini lengo lenyewe tuwe na dola 2.3 milioni, kwa ajili ya kusomesha watu hawa, lakini watu hawa watakaosomeshwa ni watu gani? Watakaosomeshwa ni Makatibu Wakuu, wale *top niche*, ambao ukiweza tu kuwapeleka na hizi ni *short term training programs in a form of seminars* na *discussions*, wenyewe wanaita *discovery tours* ili wataalamu hawa waelewe uchumi wa soko unakwendaje.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri inatosha, maana muda hauwezi kutosha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi naomba nipate ufafanuzi kwenye masuala mawili madogo; kwanza, naomba niweke *record* sawasawa kwamba, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, kama nilivyokiri kwamba, Mbozi hakuna uhaba wa ardhi. Sikusema hivyo, nilisema kwamba katika majibu ya Serikali huko nyuma, iliwahi kusema kwamba, *land pressure* kwa Mbozi ni kati ya asilimia 68 kwa 70, hayo yalikuwa majibu ya Serikali na mimi nikasema inawezekana pengine hizo taarifa zilikuwa za nyuma sana, haziwezi kuwa na ukweli. Lakini pia kwa sababu Waziri amesema atakuja Mbozi, nadhani hata akipita tu barabarani, anaweza akaona hali ilivyo kule.

Sasa naomba tu Waziri pengine aniweke sawa, amesema atakuja na mimi nafurahi kwamba atakuja, lakini pia naomba niseme kwamba, mimi sikatai shamba lile kubinafsishwa. Hilo naomba niwe wazi kwamba sikatai, ninachosema ni kwamba, hata wananchi wale wa Mbozi kama wangefikiriwa, wana uwezo pia wa kulinunua lile shamba na wakalima katika kiwango kile kile ambacho Serikali Kuu ingetegemea walime. Sasa naiomba basi Serikali inipe maelezo, inasema nini baada ya kuleta maombi kwa mara kadhaa na kama msimamo wa Serikali ni ule ule, basi Mheshimiwa Waziri atueleze anakuja lini kule Mbozi ili azungumze na wale wananchi na wajue hatma ya mwisho kuhusu yale mashamba. Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili dogo tu kumekuwa na suala la kuibinafsisha *TAZARA,* Serikali imekuwa inatoa tamko lakini hakujawa na ratiba kamili kama ilivyo kwa mashirika mengine na sijasikia mpango wowote hapa kwamba, pengine *TAZARA* ina mpango huu, zaidi ya kusema kwamba, tutakwenda China tuzungumze na Wachina kuhusu kufuta madeni, waweke vitabu vya *TAZARA* kwenye hesabu sawa ili pengine liweze kuuzika. Waziri anataka kusema nini kwa sababu mpaka leo nilipochangia, wafanyakazi wa *TAZARA* wengine wameniandikia kwenye simu zangu, jamani tunakufa tunaomba basi Serikali ichukue hatua za haraka kuhusu *TAZARA.* Kwa hiyo, naomba pengine Mheshimiwa Waziri atupe maelezo, kuna mipango gani ya Serikali juu ya kuinusuru *TAZARA* kwenye hali mbaya iliyopo sasa hivi?

**MWENYEKITI:** Kuinusuru au kuibinafsisha, naomba kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili la *land pressure*, nilichosema sio yeye. Nilisema mimi ninavyoamini na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wanaamini kwamba, eneo lile halina *land pressure,* ndiyo nilichosema sio kwamba yeye anasema hivyo.

Lakini la pili, shamba lile lazima masharti yake ni kubinafsisha *large scale,* kwa hiyo, kama kuna wananchi wamejitolea kulinunua ili liendelee *large scale estate,* hilo linaweza kuzungumzika. Lakini hatuwezi kuuza ili liwe *parcelled* katika vishamba vidogo vidogo, hapo ndiyo tunarudi nyuma kabisa, kwa kweli shamba lile zuri liendelee kuwa *large scale*.

Kuhusu *TAZARA,* sisi kama Serikali, tunapenda ibinafsishwe ama ikodishwe, sio kubinafsisha kwa kweli ni kukodisha, maana reli zote tunakodisha. Tatizo tunalolipata, hili Shirika ni *multilateral,* ni mataifa mawili. Kwa hiyo, mijadala hii tunayozungumza nao, tunaendelea nao na wenzetu tukishaelewana, basi tutaendelea kubinafsisha. Mimi najua kabisa *concern* ya wafanyakazi wa *TAZARA,* najua hata mambo wanayofanya si mazuri lakini lazima tuendelee kushauriana na wenzetu wa Zambia, vinginevyo hatuwezi kwenda mbele.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie. Amezungumzia suala *EPZ*, najua nia nzuri ya Serikali, ametaja maeneo mengi akasahau Kibaha, najua ni bahati mbaya lakini eneo la *EPZ* - Kibaha sasa hivi ni hatari kwa Wananchi wa Kibaha. Kuna mapori, watu wakitaka kwenda Halmashauri, wanapotaka kwenda kwenye vijiji vile vya Pangani na kuendelea, wengi wanaumizwa, wanapigwa na wengine wanauawa mpaka tunakuta maiti, njiani. Sasa kama Serikali haina pesa; je, wana mkakati gani kuhakikisha yale mapori yanafyekwa, kwa sababu sasa hivi hata askari wanasaidia lakini wapo wachache wanashindwa? Wananchi wa Kibaha wamenipgia simu, wananambia nimwulize Waziri lile eneo la *EPZ* watu wanakufa, wananyanyaswa na kuna wanawake mpaka wamefanywa vibaya.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, kama ifuatavyo: Kwanza, lile la *EPZ*, lile eneo la Kibaha ni la *EPZ*, sio *Special Economic Zone.* Mimi nafikiri kunahitajika kufafanua, kuna *Export Processing Zone* na kuna *Special Economic Zone*. Sasa hii sikuitaja kwa sababu haiko chini ya Wizara ya Mipango, hiyo ni *Epecial Economic Export Processing Zone,* iko chini ya Wizara ya Viwanda, lakini hata hivyo, naweza kujibu.

Nia yetu pale ilikuwa kuwaendeleza kama sehemu ya viwanda na sasa hivi hapa kuna watu wamejitokeza, wanataka kuchukua tamko ili waunganishe mabasi na baadaye *tractors.* Kwa hiyo, mimi naomba tuendelee kuvuta subira ili tuweze kupata haya

manufaa. Maana yake mji bila viwanda, hauwezi kuwa mji, utakuwa matata kabisa, kwa hiyo, mji na viwanda vinakwenda pamoja kwa lengo la kutoa ajira kwa wafanyakazi.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niweke rekodi sawa, wakati Waziri anajibu alisema kwamba, *TASAF* hawapeleki hela, sio kweli *TASAF* wanapeleka hela na katika Wilaya ya Bukombe, wamekuwa waungwana sana katika kutekeleza miradi yetu. Swali langu lilikuwa kwamba, miradi inayotekelezwa na wananchi, wanapofikia hatua ya kulipwa wanapata shida sana ya kupata malipo yao. Tarehe 31 Julai, nilipokuwa na wataalamu, tulipowahoji wakasema kuna mtaalamu mmoja anayekaa mkoani, anatembelea wilaya zote mpaka Wilaya ya Nzega, mpaka yeye huyo aje akague mradi, ndipo pale malipo yaje.

Sasa ufafanuzi ninaoutaka ni kwamba, kwa sababu Serikali ni hiyo hiyo moja, kwa nini wasi-*deligate power* pale Halmashauri, wakasimu pale Halmashauri wawepo wa kukagua hiyo miradi ili isiendele kukwama na hatimaye *TASAF* Makao Makuu wakaona kama pesa haitumiki?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Emannuel J. Luhahula, kwa kuweka rekodi vizuri lakini nataka kusema kwamba, kuhusu ucheleweshaji wa malipo unaotokana na *TASAF,* hasa kazi zilivyokwenda. Hili tutalishughulikia kwa kweli hawatakiwi wachelewe na ninavyojua mimi, *TASAF* inafanya vizuri na inatekeleza vizuri miradi yake. Lakini kama kuna ucheleweshaji unaotokana na urasimu wa Afisa huyu wa Mkoa na *TASAF,* basi huyu tutamfuatilia ili tujue kiini cha ucheleweshaji.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina nia ya kuzuia mshahara wa Waziri, nataka maelezo, Serikali ya China ilitoa fursa kuwa Afrika kuwapatia bilioni tano U$D katika miradi mbalimbali nilitaka kujua tu ni miradi ipi ambayo tuliyoiomba ambayo tungefanikiwa kuipata.

Swali langu la pili, kwenye vikao vyetu vya Kamati, tuliletewa taarifa kuwa Mradi wa *Kidunda Dam* ili-*appear* pale kuwa Mradi huu umeombwa *EMCC* na Mradi huu umeombwa vilevile kwa upande wa China, nilitaka kujua Mradi huu ataufadhili nani ambao unategemea kuleta maji katika Mkoa wa Dar es Salaam?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Mussa A. Zungu, kwa swali lake, miradi ambayo tumeiomba ni mingi ni zaidi ya 24 na baadhi ya miradi kwa sababu Wachina hawatoi miradi yote kwa pamoja, wanatoa kwa *stages*, kwa mfano, huo unaosema wa maji kama *extension* ya Chalinze kwenda mpaka Ngelele kule jeshini na kwa Wananchi, utakuwa *financed* kwa taarifa Wachina wamekubali mradi huu. Kitu ambacho cha Kidunda huu ni Mradi mkubwa, hoja ilikuwa iombewe fedha za *EMCC* na nadhani bado tunaendelea na maombi yale.

Mradi mwingine waliotupa ni ule wanaouita *Centre of Agricultural Excellence,* ambao wameteua *research extension* ya Ifakara, ambayo wanataka iwe *centre* kwa ajili

ya utafiti wa kilimo cha mpunga na pale patakuwa sio tu utafiti lakini pia kuwafundisha Wachina wanaamini kwamba, *extension officer* mzuri ni mkulima mwenyewe, unakwenda pale unawafundisha halafu akitoka kule ama yeye mwenyewe ana-*practise* yale aliyofundishwa au anawasaidia wakulima wenzake kubadilisha kilimo chao, hilo nalo limekubaliwa.

Lingine ambalo tumekubaliwa *quickly* ni hili la afya, watajenga *centre* ya *excellence medical health,* ambayo wamekubali ijengwe Dar es Salaam, lakini si Dar es Salaam kwenyewe ni karibu na Dar es Salaam, kuna *site* ambayo wameiteua Wizara yetu ya Afya, kwa hiyo ni mojawapo ya mradi ambao wameuteua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*… … … … … .... ... Sh. 424,031,700

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 – *Policy Information Development*… .. … … Sh. 608,451,000

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru katika Wizara zote, *subvote* 1003, inakuwa ni *Policy and Planning*, lakini katika Wizara hii inaonesha ni *Policy Information Development*, nikiamini kwamba, Wizara hii ndiyo ya Mipango; je, Mipango yao iko katika kitengo gani au *sub-vote* gani?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Susan A. L. Lyimo, kama ifuatavyo: Hiki kifungu cha 1003 kinaitwa *Policy Information Development* ni idara muhimu sana, huwezi kupanga bila kuwa na *information,* ile ni sehemu ya *policy.* Kwa hiyo, *planning* ipo katika maeneo mawili; kwanza, kuna ile programu ya 50 ya *investment, public investment planning*, ndiyo inafanywa pale, lakini zile idara haziko namna hiyo ni muhimu sana pale kusema kwamba, katika Wizara ile wale wote ni *planners* tu, kwa hiyo, ukitaka kupanga vitu wote wale wanashiriki, lakini labda kwa *specific planning within the ministry,* basi hii ya *policy* ndiyo inafanywa, lakini zote zinafanywa.

**MWENYEKITI:** Maana kwa kuwa *function* ya Wizara hii ndiyo *planning*, kwa hiyo, ina *detail* ile ile *planning*, inanyumbua mpaka *information* na vitu vingine.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Micro-Economy*… … … … … … … … .... Sh.762,192,700

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* 20, 260100 - *Communication, Information*, *Supplies and Services, especially* hapa kwenye

*communication.* Wakati Waziri anatoa maelezo alikuwa anazungumzia mahusiano kati ya ukuaji wa idadi ya watu na ukuaji wa uchumi na akasema kwamba, ukuaji wa idadi ya watu unaathiri ukuaji wa uchumi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba aweke sawa sawa, kwa sababu nadhani ukuaji wa idadi ya watu, hauna uhusiano na ukuaji wa uchumi ila una uhusiano na pato binafsi la mtu. Nilikuwa naomba a-*clarify* hiyo, kwa sababu ni *information* muhimu sana.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Nimeandikiwa *note,* ukizungumza kwamba, ina-*affect per capita income, at the end of the day* lazima ita-*affect GDP,* maana *income* kwa *capital* ni *total*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *External Sector*… … … … .... … … … … Sh. 830,882,400

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Social Services and Human Resource Development* ..... ... .... .... .... .... .... .... .... .... Sh.1,001,609,400

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Mimi natazama katika kifungu hicho hicho, kifungu kidogo 260100, ukiangalia kama ni *planning,* unachoingiza kwenye *planning* yako lazima kitoe matokeo, ni kama sisi walimu, *curriculum* ukiitengeneza lazima utapata aina fulani ya watoto watakaokuwa wamepitia ile *curriculum*.

Sasa ukiangalia hapa ni kwamba, katika kifungu hicho kwa miaka mitatu ni kwamba, kulikuwa na hizo halafu imepanda ika-*double,* sasa mwaka huu imekwenda pesa nyingi katika kifungu hiki cha *Communication Information, Supplies and Services*.

Ukiangalia chini huko tuliko kwenye mawilaya, huoni ile ni mipango inayoonesha kuweza kutumia hizi pesa tukapata hayo matokeo. Kwa hiyo, mimi ningependa maelezo, hasa kwa sababu tukitazama hii mipango, lazima uilinganishe na mipango iliyoko mikoani na wilayani. Sasa huu mfumko wa mpango wa *Communication, Information and Supplies* katika *Human Resources Development, Social Services and Human Development Resources,* ambazo mimi nikiangalia katika Wilaya nadhani na ya Misungwi na hii ya mwenzagu hapa kila mara ni kama *cut and paste,* ikiwekwa mwisho Ukerewe itakuwa ya mwisho milele. Kuna *cut and paste*, lakini pesa zinafumka haraka haraka katika hiyo *cut and paste,* huo sio mpango. Lazima mtaalamu awe anafanya *cut and paste* na kompyuta hizi ni kazi rahisi, kwa hiyo, naomba maelezo hapo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, usituhutubie wewe uliza swali.

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Ndiyo nauliza sasa, ninaomba maelezo yanayoonesha huo mfumko usiowiana na mipango ya mikoa na wilaya?

**MWENYEKITI:** Kwanza kabisa, hii ipo chini, *poverty eradication* halafu haijafumka imeshuka sana, ilitoka milioni 31 sasa iko milioni 4 tu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunazungumza vifungu tofuati. Nafikiri anazungumzia Kifungu 3001 - *Social Services and Human Resource Development.*

**MWENYEKITI:** Hiki kimeshapita, jibu hilo.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Sasa nijibu lipi ni hili la *communication* au? *(Kicheko)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Jibu langu.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Huyu alichelewa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ngoja kwanza. Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude I. Mongella, anauliza kwenye kifungu 3001, kifungu kidogo 260100 – *Communication,* ndiyo zimeongezeka toka shilingi milioni 16 mpaka milioni 259. Naomba jibu.

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimwa Mwenyekiti, hiki kifungu lazima kiongezeke hivi, kwa sababu hili ndiyo *key element* katika Wizara, maana hapa tunazungumza sio tu *social services,* kama *division* katika Wizara ya Mipango, lakini lile suala la *Human Resources Development.* Kama mtakumbuka kwenye *presentation* ya Kamati ya Fedha na Uchumi, walizungumzia *technical capacity building*. Kwa hiyo, hapa ndiyo penyewe pa ku-*train* wataalamu wale wa *Human Resources* ili waweze ku-*manage not only* Wizarani, lakini hata kwenye Wizara nyingine, kwa sababu sisi ndiyo tuna-*produce planners*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Poverty Eradication* … … … … … ... Sh. 1,194,403,500
Kif. 3003 - *Economic Empowerment* … … … … .... ... Sh. 540,922,700
Kif. 5001 - *Public Investment Planning* … … … ... .... Sh. 610,268,400
Kif. 5002 - *Growth Strategies* … … … … … … ... ..... Sh. 705,821,300

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 66 - Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji**

Kif. 1001 - *Administation and General* ... ... ... ... .... Sh. 13,925,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy Information Development* .. … .. ... Sh. 3,564,400,00

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub-item 6335 - Renovation of POPP Building.* Ninaomba maelezo kidogo, kwa sababu ninajua *renovation* labda ni masuala ya kurekebisha majengo, lakini ukiangalia unaona kwamba, kuanzia miaka ya nyuma ilikuwa shilingi milioni 100, shilingi milioni 300 na mwaka huu wametengewa shilingi milioni 350. Ninaomba kujua hiyo *renovation* ni ya namna gani mpaka kila mwaka wanatengewa fedha kiasi hiki?

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo kwamba, nadhani anajua jengo iliko Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ni jengo tulilolirithi kwa Wajerumani. Kwa hiyo, lazima tuendelee kulikarabati ili tuweze kuishi mle na ingefaa labda angetembelea angeona mwenyewe hali halisi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, umekaribishwa kutembelea huko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Macro-Economy* … … … … … … … ... ..... Sh.29,939,000
Kif. 2002 - *External Sector* … … … … … … …. .... .Sh.9,792,411,000
Kif. 3001 - *Social Services and Human Resources dev*..Sh. 1,541,189,000
Kif. 3002 - *Poverty Eradication* ... … … … … ..... .... Sh. 5,573,175,100
Kif. 3003 - *Economic Empowerment* … … … … ..... ....Sh.199,000,000
Kif. 5001 - *Public Investment Planning* … … …. ..... ....Sh. 25,450,000
Kif. 5002 - *Growth Strategies* ... ... ... ... ... … ... .... Sh.18,358,435,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIPANGO, UCHUMI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi, imepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa mwaka 2007/2008, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kuwa, Makadilio ya Matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchimi na Uwezeshaji, sasa yakubaliwe na Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki**.**

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji - kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa napenda kumpa pongezi Mheshimiwa Waziri, unajua yeye huwa anakaa kwenye midahalo kila siku, kwa hiyo, akisema anayajua mambo mengi kabisa, ukimruhusu anaweza akamaliza siku nzima. Kwa hiyo, nampongeza sana kwa kuifahamu Wizara yake vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 81(i), ambayo inasema jumla ya siku zisizozidi siku 35 zitatengwa kwa ajili ya Bunge kujadili utekelezaji wa kila Wizara kwa Mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba, pamoja na kupitishwa kwa Muswada wa Fedha za Matumizi. Siku hizo zinafika kesho. Kwa hiyo, kesho tutakuwa na matatizo ya programu, ili tupitishe Wizara ya Fedha lakini wakati huo huo inabidi tupitishe Muswada wa Sheria za Fedha kwa mwaka 2007/2008, *The Finance Bill* kesho hiyo hiyo. Wakati huo huo itabidi tupitishe Muswada mwingine, ambao unafungasha yote tuliyokuwa tunayafanya sasa, tumeyakubali matumizi yake na makadirio ya fedha zinazohusika. Kwa hiyo, hii yote itafanyika kesho. Sasa kwa utaratibu wetu, hiyo tu Wizara ya Fedha peke yake ni siku, lakini hizo siku hazipo. Kwa hiyo, naomba mjiandae kwa ajili ya *Finance Bill,* halafu na hii Wizara ya Fedha tutaizungumza pengine asubuhi itabidi tuimalize, tuingie *Finance Bill* na *Appropriation Bill* mchana. Ziligawiwa toka siku za mwanzo, huwa mnakuwa nazo.

Kwa hiyo, hiyo ni taarifa ambayo mjiandae wale watakaopenda kusoma. Kesho tuta-*manage* itakavyokuwa, lakini tuna mambo matatu. *Appropriation Bill* haijadiliwi lakini *Finance Bill* na Wizara ya Fedha, lazima zizungumzwe. Kwa hiyo, naomba hiyo mkajiandae.

Baada ya kusema hayo, naomba kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa, Tarehe 10 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*